# Nipashe

Alhamisi Mei 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579925

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13



## Mpina amshukia Dk. Tizeba bungeni

UKURASA 8




# Lissu ataja rasmi tarehe kurudi



UKURASA 2

## Wastaafu wahenyea mafao kwa miezi 4

UKURASA 3



## JK aibua hoja utawala bora

- **Asema** ombwe lake kikwazo kwa maendeleo Afrika, ataja pia umaskini kuwa ni sumu...*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **SIMBA: SEVILLA WATAKAA TAIFA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# 13,600 wakutwa na homa ya ini

**Na Mary Geofrey**

KATI ya wachangiaji wa damu 307,835, waliojitokeza kuchangia damu katika vituo mbalimbali nchini mwaka jana, watu 13,613 (asilimia 4.4) walibainika kuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina ya Hepatitis B na 1,092 virusi aina ya Hepatiti C.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura, virusi vya kundi B na C vinapoingia kwenye mwili wa binadamu kushambulia ini na baadhi hawaonyeshi, hupata athari kwenye ini na wengine kupata maambukizi sugu na wa muda mrefu.

Aidha, takwimu hizo zilieleza kuwa, katika kipindi cha mwaka juzi kati ya watu 233,953 waliojitokeza kuchangia damu, watu 11,417 (asilimia 4.9) walikuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina B.

"Katika jamii, utafiti mahususi ujulikanao kama 'This Tanzania HIV Indicator Survey' uliratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, mwaka 2016/17 ulionyesha maambukizi ya homa ya ina aina ya B ni asilimia 4 miongoni mwa Watanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49," alieleza Sungura katika taarifa hiyo.

Alisema virusi hivyo vya kundi B, C na D huambukizwa kwa njia ya kuongezewa damu yenye virusi vya ugonjwa huo, kujamiiana na wenye maambukizi na kujidunga sindano yenye virusi vya ugonjwa huo.

Alitaja njia nyingine za maambukizi ni majimaji yenye uambukizo kama damu na matapishi kutoka kwa mgonjwa mwenye virusi hivyo na kuingia kwa mtu mwingine andapo ana kidonda au michubuko ya ngozi.

Alisema njia zinazoeneza virusi vya homa ya ini ni zile zinazoeneza Ukimwi ikiwamo mama anapoweza kumuambikiza mtoto wakati wa ujauzito na kujifungia.

"Taarifa hii pia inabainisha na kufafanua ukweli juu ya ugonjwa huu kufutia taarifa potofu zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu ugonjwa huu na namna ya kujikinga," alisema Sungura.

Kuhusu dalili za ugonjwa huo, alisema mtu anaweza kuugua na asiwe na dalili na hufanya hivyo pindi unapokolea mwilini ambazo ni mwili kuishiwa nguvu, kichefuchefu na kutapika, homa ya tumbo. Alisema hatua zinazochukuliwa na serikali ni kutoa chanjo kwa watoto wadogo, kwa watu walio katika hatari ya kupata maambukizi na kwamba wameanza kutoa chanjo hizo kwenye vituo vya afya nchini.

# Lissu ataja tarehe rasmi ya kutua nchini

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Singida Mashariki kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, ametaja tarehe rasmi ya kurejea nchini kuwa ni Septemba 7, mwaka huu.

Lissu ambaye kwa sasa anatembea kwa msaada wa gongo moja amepanga kurejea siku hiyo tarehe ambayo mwaka 2017, alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana.

Septemba 7, mwaka juzi, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 akiwa ndani ya gari nyumbani kwake Area D mjini Dodoma na watu hao wakati akitoka bungeni.

Jana, Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), Patrick Ole Sosopi, aliliambia Nipashe kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chadema, Freeman Mbowe, aliwapa taarifa kuwa Lissu amemwambia kuwa atawasili nchini tarehe hiyo. "Tuliambiwa na Mwenyekiti wetu kuwa Lissu amesema atarejea Tanzania Septemba 7, mwaka huu na atakuwapo kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema.

Katika ukurasa wa Bavicha Instagram, waliandika, "Lissu atawasili nchini Septemba 7, mwaka huu na mapokezi yake yatatangazwa kitaifa."

Gazeti hili lilimtafuta Mbowe kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ujio wa Lissu, lakini simu yake ilikuwa ikiita bila kupokelewa.

Baada ya shambulio hilo la risasi, Lissu ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Tanzania alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Dodoma kwa matibabu ya awali na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa katika hospitali moja mjini Nairobi, Kenya.

Lissu ambaye pia ni Mwanasheria Mkuu wa Chadema, alikaa siku 121 hospitali ya Kenya hadi Januari 6, mwaka jana, alipohamishiwa kwenda hospitali nyingine nchini Ubelgiji ambako Desemba 31, alimaliza matibabu yake ya awali na kuanza ziara nchi mbalimbali.

Januari 19, mwaka huu, Lissu alihojiwa katika kipindi cha Dira ya Dunia cha Idhaa ya Kiswahili ya BBC na kuonyesha nia ya kugombea urais mwaka 2020 kama wanachama na viongozi wenzake wa Chadema watampa ridhaa hiyo.

Januari 21, Lissu alihojiwa kwenye kipindi cha HardTalk kwenye Televisheni ya BBC na mtangazaji maarufu Stephen Sackur, kipindi ambacho kilizua mjadala mkubwa kutokana na namna alivyojibu maswali.

Februari 20, mwaka huu, Lissu alifanyiwa upasuaji wa 23 wa mwisho kwenye goti la mguu wa kulia katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Leuven, Gasthuisberg nchini Ubelgiji na alisema baada ya hapo atarejea Tanzania.



Rais Dk. John Magufuli akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Brigedia Jenerali mstaafu Athuman Hassan Ngwilizi katika Hospitali Kuu ya Jeshi ya Lugalo, jijini Dar es Salaam jana. Ngwilizi alifariki dunia hospitalini hapo Mei 20, 2019. **PICHA: IKULU**

# JK aibua hoja utawala bora, umaskini

**Na Beatrice Moses**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amesema kukosekana kwa umoja, utawala bora na uwepo wa umaskini ni miongoni mwa matatizo yanayozikandamiza nchi nyingi za Afrika, hivyo kuzikosesha maendeleo.

Akizungumza kwenye Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere,Kikwete alisema licha ya kufanikiwa kupata uhuru, nchi nyingi za Afrika ni maskini.

Alisema wakati viongozi kadhaa wa Afrika walipata nafasi ya kukutana kwenye nchi za Ulaya waliunganisha nguvu zao za kiharati katika kutetea Afrika, hatimaye kufanikiwa kusaidia kupatikana kwa uhuru kuanzia mwaka 1950 hadi 1964.

Kikwete aliyekuwa mgeni rasmi kwenye tamasha hilo lililokusanya wasomi wa viwango mbalimbali kutoka katika nchi tofauti, alisema kuna nchi bado zinatawaliwa kijeshi, viongozi wengine wamekaa madarakani kwa muda mrefu.

Alisema kuna wakati viongozi wa Umoja wa Afrika (AU) walianzisha utaratibu wa kujitathmini ambapo viongozi waliitwa na kupewa maoni ya kujisahihisha, wapo waliofanyia kazi na wengine waliyaweka.

Akizungumzia kuhusu umasikni Kikwete alisema katika nchi 30 maskini duniani 27 ni kutoka Afrika.

"Watu wetu wanakabiliwa na umaskini mkubwa sana, haya ndiyo mambo ambayo Afrika inatakiwa iungane kukabiliana nayo, tumetoka mbali na tulikuwa na mafanikio kwenye kujipatia uhuru, lakini licha ya jitihada tumeshindwa kujikomboa kutoka kwenye hali duni," alisema.

Alisema hali ya uanaharakati iliyoanzishwa na waasisi wa nchi za Afrika kabla na baada ya uhuru, walibaini kuwapo kwa matatizo hayo walikubaliana kuyatatua kwa umoja, lakini hadi sasa harakati hazijafanikiwa.

Kikwete alisema katika nchi 54 zilizopo katika bara la Afrika, ni nchi moja pekee ndiyo inatajwa kuwa imeendelea nayo ni Mauritius wakati 27 kati ya hizo zipo katika uchumi wa kati.

Alibainisha kuwa nchi zimekosa umoja hata katika kujitafutia masoko ya bidhaa mbalimbali, kila moja inajitafutia binafsi, hivyo elimu inahitajika ili kuwezesha waafrika kupambana kuunganisha nguvu zao katika kujitafutia maendeleo.

Katika tamasha hilo, Profesa Rwekaza Mukandala, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)mstaafu, alisimikwa kuwa Mwenyekiti wa Kigoda hicho, akimfuatia Profesa Penina.

Katika hotuba yake Prof. Mukandala alisema harakati za

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA

## JPM aongoza wakazi Dar kumuaga Ngwilizi

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewaongoza waombolezaji kuaga mwili wa mwanasiasa mkongwe, marehemu Brigedia Jenerali mstaafu Hassan Ngwilizi, aliyefariki dunia Jumatatu ya wiki hii Hospitali ya Jeshi ya Lugalo alikokuwa akitibiwa.

Mwili wa marehemu Brigedia Jenerali Ngwilizi aliagwa jana hospitalini hapo na baadaye alisafirishwa kuelekea Mlalo Lushoto mkoani Tanga kwa ajili ya mazishi.

Viongozi wengine walihudhuria shughuli hiyo ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo; Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Hussein Mwinyi; Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo na Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Mussa Salum.

Baada ya Rais Magufuli kuwasili hospitali ya Lugalo jana asubuhi alikwenda moja kwa moja kwenye eneo maalum lililowekwa kitabu maalum cha waombolezaji na kuandika. Baada ya hapo alipita mbele ya jeneza la mwili wa Brigedia Jenerali Ngwilizi kutoa heshima zake za mwisho na kisha aliwapa pole familia ya marehemu.

Shughuli ya kuaga ilipokamilika wakati mwili ukiwa umebebwa na wanajeshi kuelekea kwenye gari maalum, Rais Magufuli aliambatana na viongozi wengine, ndugu, jamaa na marafiki kuusindikiza kutoka katika Hospitali ya Lugalo tayari kwa safari.

Katika uhai wake, Ngwilizi alitumikia Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kuanzia mwaka 1968 hadi 1993 katika nafasi mbalimbali hadi Brigedia Jenerali.

Pia, aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Mbunge wa Kuteuliwa na baadaye Mbunge wa Mlalo, Lushoto mkoani Tanga kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2005 hadi 2015. Ndani ya Bunge aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Bunge iliyoundwa Julai 2, mwaka huo, kuchunguza kashfa iliyomhusisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini na Nishati, Eliakim Maswi, akiwatuhumu baadhi ya wabunge kula rushwa kutoka kwenye kampuni ya mafuta. Kadhalika, aliwahi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa -Tamisemi) wakati wa uongozi wa Rais mstaafu Benjamin Mkapa.



Magari yakikwepa shimo kubwa lenye maji katikati ya Barabara ya Chang'ombe, eneo la Keko Magurumbasi, jijini Dar es Salaam jana. Shimo hilo, lililopo kwa muda mrefu sasa bila kufanyiwa ukarabati wowote limekuwa likisababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo, hasa nyakati za mvua. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mbunge ahoji sababu wanaume kupendelewa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Ulanga Mashariki, Goodluck Mlinga (CCM), amehoji bungeni sababu za serikali kuwajali wanaume kwa kuwapa kondomu huku ikisita kutoa bure taulo za kike kwa ajili ya wanafunzi.

Mlinga alihoji suala hilo bungeni jijini Dodoma jana, baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali', akieleza kuwa takwimu za wanafunzi kufanya vibaya darasani ni mbaya kwa wanafunzi wa kike hasa wanaotoka maeneo ya vijijini.

Alisema anaona sababu kubwa ya kufeli kwa wanafunzi wa kike katika maeneo hayo ni kutohudhuria shuleni kipindi wanapokuwa katika siku zao za hedhi.

"Mheshimiwa Spika, Bunge limekuwa likipiga kelele sana serikali namna gani itawasaidia wanafunzi kwa kuwapa taulo za kike bure. "Lakini Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia serikali ina utaratibu wa kutoa vifaa tiba kwa makundi mbalimbali ya wananchi wake ili kuwasaidia kuepukana na magonjwa mbalimbali katika kuboresha afya.

"Kwa mfano, Mheshimiwa Spika, tumeona serikali inatoa bure ARVs (dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi) bure kwa watu wanaoishi na VVU (Virusi vya Ukimwi), wagonjwa wa kifafa wanapewa dawa bure, TB (kifua kikuu) wanapewa dawa bure.

"Hata ... (alitaja jina la dawa inayoaminika inatibu ugonjwa wa malaria) ilitakiwa iuzwe Sh. 20,000, lakini inauzwa Sh. 2,000. Mheshimiwa Spika, serikali inagawa mipira ya kiume bure hadi kwenye zahanati za vijijini.

"Mheshimiwa Spika, kweli serikali yetu inatoa kipaumbele kwa wazinifu, inaacha wanafunzi! Kwanini serikali isitoe taulo za kike bure kwa wanafunzi wetu?" Mlinga alihoji.

Spika Ndugai aliyekuwa anaongoza kikao cha jana, aliitaka serikali kuichukua hoja hiyo na kuangalia namna ya kuifanyia kazi suala hilo.

"Hilo nalo pia limefika serikalini na kwa wakati mwafaka, serikali itaona namna gani ya kuzungumza na Bunge kuhusiana na mambo haya," Spika Ndugai alisema.

Kwa muda mrefu Mbunge wa Viti Maalum, Upendo Peneza (Chadema), amekuwa akihoji bungeni kuhusu serikali kutoa taulo za kike kwa wanafunzi bila malipo.

# Wastaafu wa PSSSF sasa wasotea pensheni miezi 4

**Na Salome Kitomari**

WASTAAFU wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), wameendelea kusotea pensheni yao ya kila mwezi kwa miezi minne sasa.

Wastaafu hao waliozungumza na Nipashe, Aprili mwaka huu, baada ya kugoma kuondoka kwenye ofisi ya PSSSF mkoa wa Ilala, walisema hawajalipwa tangu Februari mwaka huu.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, wastaafu hao walisema majibu wanayoendelea kupewa ni kuwa majina yao hayajaingizwa kwenye mfumo yalisahaulika.

"Hadi sasa hatujalipwa na hatujui lini hasa wataanza kutulipa, wamesema wanaingiza majina yetu kwenye mfumo. Tunapata shida, tunaomba serikali itusaidie katika hili," alisema mmoja wa wastaafu.

Aidha, wastaafu hao ambao wametofautiana miezi ya kudai pensheni ya kila mwezi, walisema waliwasilisha taarifa zao muhimu, lakini bado tatizo la kutoonekana kwenye mfumo limeendelea kuwapo, hivyo kuwafanya waishi maisha magumu kwa kuwa fedha hizo wanazitegemea kwa mahitaji yao ya kila siku.

"Sijalipwa pensheni yangu ya mwezi kwa miezi minne sasa, ila naamini serikali itatulipa, lakini ni vyema kukawa na mawasiliano juu ya lini hasa watamaliza kuweka majina yetu kwenye mfumo na kuanza kutulipa," alisema mstaafu kutoka mkoani Kilimanjaro.

Wastaafu hao walisema licha ya kuchanga kwa uaminifu kwa kipindi chote walichokuwa wanafanyakazi, lakini imefika wakati wa kulipwa fedha zao kila mwezi wamejikuta katika wakati mgumu.

Mmoja wa wastaafu aliyestaafu 2012, alisema alihakiki taarifa zake Februari mwaka huu, lakini hadi sasa anaelezwa tatizo ni uhakiki wa taarifa, na kwamba zimekusanywa na kutumwa Dodoma.

Mwingine alistaafu mwaka

INAENDELEA UK. 8

DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUAJIRI MSHAURI KWA AJILI YA KUFANYA TATHIMINI YA MWISHO YA MRADI NA PIA INATAKA KUINGIA KWENYE MKATABA KWA MUDA WA MWAKA MMOJA NA MTOA HUDUMA YA UTOAJI TIKETI ZA NDEGE.

NYARAKA ZA KUJAZIA MAPENDEKEZO NA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 21.05.2019 HADI TAREHE 04.06.2019 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHIMPAKA SAA 10:30 JIONI.TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0627423991 au barua pepe j.kabore@drctanzania.org

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 05.06.2019 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.itb@drctanzania.orgAU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.

215240801

# Wanafunzi wakiri kufanya mapenzi mbele ya DC

**Na Joseph Mwendapole,**
MKURANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Vianzi, Mkuranga mkoani Pwani, wamekiri mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Philbert Sanga, kuwa kuna wanafunzi wengi wa shule hiyo ambao wana uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wenzao.

Wanafunzi hao walikiri hayo mbele ya DC huyo wakati wa hafla ya kukabidhiwa viti 45 na meza 45 vilivyotolewa na Kampuni ya KIOO Ltd, hafla iliyofanyika kwenye shule hiyo yenye wanafunzi 592.

Baada ya kuwakabidhi viti na meza hizo, Sanga aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii na kuachana na mambo ya mapenzi kwa kuwa wakibainika watafukuzwa shule na kushindwa kufikia ndoto zao.

Hatua ya wanafunzi hao kukiri mbele ya Mkuu wa Wilaya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wenzao ilitokana na Mkuu huyo kuwahoji kama baadhi yao wana uhusiano wa kimapenzi na walimu wao na kukataa, lakini alipowauliza kama kuna wanafunzi wana uhusiano wa kimapenzi na wenzao walikiri kuwapo kwa hali hiyo.

"Nafurahi kusikia kwamba hakuna mwanafunzi mwenye uhusiano wa kimapenzi na walimu hapa Vianzi, lakini je kuna wanafunzi kwa wanafunzi ambao wana uhusiano wa kimapenzi hapa? Alihoji Sanga na wanafunzi wengi kuitikia ndiyoo na hata aliporudia mara ya pili kuwahoji jibu lilikuwa hilo hilo.

Sanga aliwataka walimu wa shule hiyo kuwafukuza shule mara moja wanafunzi watakaobainika kuwa na uhusiano wa kimapenzi wenyewe kwa wenyewe kwa kuwa wakiachwa wanaweza kuambukiza tabia hiyo kwa wanafunzi wenzao.

Mkuu wa shule hiyo, Ashura Manaki, alishukuru kwa msaada huo na kwamba utasaidia jitihada za serikali katika kutoa elimu bure. Alisema utawasaidia kukuza taaluma shuleni hapo kwa kuwa madawati na viti hivyo vimefanya mazingira mazuri ya kusoma.

"Tunawashukuru sana KIOO Ltd, lakini tunaomba isiwe mwisho ili tukidhi mahitaji ya wanafunzi ambao idadi yao inazidi kuongezeka kutokana na mpango wa elimu bure," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Vianzi, Maulid Jongo, alisema kijiji hicho kinathamini sana mchango wa KIOO Ltd .

"Kuna mambo mengi ambayo KIOO wanasaidia kwenye kijiji chetu tunawashukuru ila ombi langu wasituchoke tukienda tena kuwaomba," alisema.

# Kipimo tahadhari ya ebola kufanyika Namanga

**Na Romana Mallya**

KIPIMO cha tahadhari cha ugonjwa wa ebola kinatarajia kufanyika katika mpaka wa Tanzania na Kenya uliopo Namanga kwa muda wa siku nne kuanzia Juni 11, mwaka huu.

Daktari Michael Katende, kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki Idara ya Afya, aliwataka wananchi kutoogopa tukio hilo kwa sababu lengo lake ni kuhakikisha nchi zinakuwa kwenye usalama wa magonjwa ya milipuko.

Dk. Katende alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na chombo kimoja cha habari kuhusu utekelezaji huo utakaoanza Juni 11 hadi 14, mwaka huu, katika mpaka wa Namanga na kuhusisha nchi za Tanzania na Kenya.

"Lengo ni kujua namna nchi zetu zilivyojipanga kukabiliana na magonjwa ya milipuko ikiwamo ebola," alisema.

Alisema wanafahamu kuwa kila nchi ina mikakati yake ya kukabiliana na magonjwa, lakini kitakachofanyika siku hiyo ni kuongeza uelewa zaidi pamoja na kuangalia changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi kabla ya magonjwa kujitokeza.

"Unawaomba watu wanaosafiri na kupita mpaka wa Namanda wasiwe na wasiwasi siku hiyo kwa sababu tunachokifanya ni kujua nguvu yetu ya kukabiliana na magonjwa na changamoto zake," alisisitiza.

Alisema siku hiyo wanatarajia kuwa na watu 250 na huduma hiyo itatolewa kwa nchi hizo.

Pia alisema watakuwa na wageni kutoka nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki na wageni wengine wa mataifa mbalimbali duniani.

"Tunataka tuwe na uhakika nchi zetu tupoje katika kukabiliana na ebola, je, tumejiandaa kwa kiwango gani? Maeneo gani au vitu gani tunatakiwa kuongeza nguvu. Tunatarajia kupata mrejesho ili kujua nini kinatakiwa kufanyika," alisema.

Ugonjwa wa ebola husababishwa na virusi vya ebola ambavyo huambukiza kwa njia zifuatazo; kugusa damu au majimaji kutoka kwa mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo. Kugusa maiti ya mtu aliyekufa kwa ugonjwa huo. Kugusa wanyama (mizoga na wanyama wazima) walioambukizwa kama vile sokwe na swala wa msituni.

Wakati mtu anapoambukizwa hadi dalili za ugonjwa huo zinapoanza kuonekana ni kati ya siku mbili hadi 21 na mara nyingi dalili huanza kuonekana kati ya siku ya nane hadi ya kumi baada ya kuambukizwa, zikijidhihirisha kama dalili za malaria au homa.

Dalili za ebola zinatajwa kuwa ni pamoja na homa, kichefuchefu na kutapika, kuharisha, vidonda vya koo, kuumwa kichwa, maumivu ya misuli, kusumbuliwa na tumbo, kuchoka, kukosa hamu ya kula ambazo zinaweza kujitokeza zote kwa pamoja, ingawa mgonjwa anaweza kuwa na dalili moja au mbili kati ya hizo.

Dalili hizo huweza kujitokeza siku ya tano baada ya mtu kuona dalili za kwanza za ugonjwa huo na anaweza kutokwa na damu kupitia tundu za mwili kama mdomoni, puani na sehemu za siri. Baada ya kupatikana na virusi vya ebola, mgonjwa anapaswa kujitenga na wengine, mfano asisalimiane kwa mikono, kumbusu mwengine au kufanya tendo la ngono.

Sampuli za damu, mate na mkojo lazima zipelekwe maabara yenye vifaa vya kuaminika ili kufanyiwa uchunguzi wa kina kubainisha mapema virusi hivyo.

Mwaka jana, Shirika la Afya Duniani (WHO), lilizitaka Uganda, Sudan Kusini, Rwanda na Burundi zichukue tahadhari ya haraka kutokana na kusambaa kwa ugonjwa huo.

Shirika hilo lilisema hatari ni kubwa kwa Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini na tayari nchi hizo zimeambiwa kuchukuwa hatua za haraka ili kuzuia ugonjwa huo.

WHO ilitoa kauli hiyo baada ya mkutano maalumu wa dharura uliofanyika mjini Geneva kujadili hali ya ugonjwa huu nchini ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambako takwimu zilionyesha kati ya watu 10 walioambukizwa ebola sita hufariki.

Agosti 11, mwaka jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema Tanzania hakuna mgonjwa yeyote aliyehisiwa au kuthibitishwa kuwa na virusi vya ebola.



Mkurugenzi Mkuu na Mwakilishi wa Umoja wa Watengeneza Mifuko Mbadala Tanzania, Mhandisi Allen Kimambo (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu upatikanaji wa mifuko mbadala na mafunzo ya utengenezaji wa mifuko hiyo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kortini kwa kutakatisha bil. 8.1/-

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA mkazi wa Nairobi nchini Kenya, Abshir Hachi Afrah (56), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka matatu yakiwamo kukwepa kodi, kuisababishia hasara Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kutakatisha Sh. bilioni 8.107.

Mfanyabiashara huyo ambaye pia ni raia wa Somalia, alisomewa mashtaka yake na Wakili wa Serikali Wankyo Simon, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Mtega.

Simon alidai kuwa kati ya 2015 na 2018 jijini Dar es Salaam, mfanyabiashara huyo alikwepa kulipa kodi wakati wa kusambaza ya mafuta ya petroli.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na tarehe za tukio la kwanza, katika ofisi za TRA jijini Dar es Salaam, kwa kitendo chake cha ukwepaji wa kodi aliisababishia hasara mamlaka hiyo Sh. 8, 107,509,385.48 kinyume cha Sheria ya Kodi ya mwaka 2015.

Katika mashtaka ya tatu, ilidaiwa kuwa mshtakiwa alijipatia Sh. bilioni 8.107 kwa kukwepa kulipa kodi wakati akijua kwamba fedha hizo ni zao la uhalifu ambalo ni la kutakatisha fedha.

Hakimu Mtega alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi hadi ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Juni 4, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na mshtakiwa amerudishwa rumande kwa sababu mashtaka hayo hayana dhamana.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani, Philbert Sanga (katikati), akifurahia jambo na wawakilishi wa Kioo Ltd, William Bongo (kushoto) na Richard Musumle, baada ya kupokea msaada wa madawati 45 na meza 45 kutoka kwa kamapuni hiyo, kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Vianzi, wilayani humo, jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jela miaka 27 kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wanne wa jijini Dar es Salaam wamehukumiwa kwenda jela kutumikia miaka 27 baada ya kupatikana na hatia ya makosa matatu ikiwamo kuratibu genge la ujangili na kukutwa na vipande sita vya meno ya tembo vyenye thamani ya Dola za Marekani 15,000 (Sh. 32,565,000).

Kadhalika mahakama huyo imetaifisha gari yenye usajili T 540 DDS aina Funcargo, iliyotumika kusafirisha meno hayo.

Hukumu hiyo imetolewa Mei 20, mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Hakimu aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Solomon Makuru, Siasa Shabani, Musa Ligagabile na Omary Sabo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na mawakili wa serikali, Salim Msemo na Costantino Kakula.

Upande wa Jamhuri uliita mashahidi 11 na vielelezo ikiwamo meno ya tembo pamoja na gari.

Katika shtaka la kwanza washtakiwa wote kasoro mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa nne wamehukumiwa kwenda jela miaka mitano.

Shtaka la pili kujihusisha na nyara za serikali, wote wamehukumiwa kwenda jela miaka miwili.

Katika shtaka la tatu la kusafirisha nyara hizo wamehukumiwa kwenda jela miaka 20.

"Mahakama yangu bila kuacha shaka imewaona washtakiwa mna hatia inawahukumu kwenda jela kutumikia kifungo hicho na kwamba adhabu yote itakwenda sambamba," alisema Hakimu Kasonde.

Katika kesi ya msingi inadaiwa Juni 23, 2016 eneo la Kimara Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam kwa pamoja walikutwa wakisafirisha vipande sita vya meno ya tembo vikiwa na thamani ya Dola za Marekani 15,000 (Sh. milioni 32.5), mali ya serikali ya Tanzania bila kibali cha mkurugenzi wa wanyamapori.

# Mifuko mbadala ya plastiki kuuzwa 70/-

**Na Mary Geofrey**

UMOJA wa wazalishaji na wauzaji wa mifuko mbadala ya kubeba bidhaa mbalimbali nchini, umesema wamejipanga kuzalisha bidhaa za kutosha kukidhi mahitaji ambayo itauzwa kuanzia Sh. 70.

Kwa sasa mfuko mmoja wa plastiki unauzwa kuanzia Sh. 50 hadi Sh. 500.

Mwakilishi wa wazalishaji wa bidhaa hizo, Daniel Ngumbuke, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wao na waandishi wa habari kueleza namna walivyojipanga kuzalisha bidhaa hiyo na kutoa mafunzo ya utengenezaji kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema awali viwanda vilivyokuwa vinazalisha bidhaa hizo vilisuasua kwa sababu ya kukosekana kwa soko la uhakika lililokuwa limezidiwa na mifuko ya plastiki na kwamba vimeshaanza kufanya kazi.

"Tumejipanga kuzalisha bidhaa nyingi ambazo zitatosheleza kwa mahitaji yaliyopo hasa ikizingatiwa asilimia 80 ya mifuko ya plastiki iliyokuwa inatumika nchini ilikuwa inatoka nje ya nchi. Hivyo tumejipanga kutoa elimu pia kwa wazalishaji wadogo na wajasiriamali kwa sababu bidhaa hiyo inaweza kuzalishwa na mtu yoyote," alisema Ngumbuke.

Aidha, umoja huo uliiomba serikali kuendelea kuwalea na kufungua milango ili kutoa nafuu za kuwezesha kutekeleza jukumu hilo la kukidhi mahitaji ya Watanzania.

Alisema kuwa uharibifu unaotokana na mifuko ya plastiki umekuwa ukiipa gharama serikali kurekebisha miundombinu pamoja na kuliwa na wanyama kama ng'ombe na

INAENDELEA UK.8

# Askofu wa Tanzanite kuzikwa Jumatatu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MFANYABIASHARA maarufu wa madini ya Tanzanite mkoani Arusha, Thomas Mollel maarufu kwa jina Askofu aliyefariki dunia jijini Dodoma, atazikwa Jumatatu.

Mwili wake unatarajia kusafirishwa kwa ndege Jumapili kupelekwa mkoanuArusha.

Akizungumza kwa njia ya simu ya kiganjani Katibu wa Cha Cha Mapinduzi CCM Wilaya ya Meru, Shabani Mdoe, alisema baada ya kuwasili katika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), utapelekwa nyumbani kwao Mbuguni Arusha kwa ajili ya mazishi Jumatatu.

Alisema ndugu zake walifika jana Dodoma na kufanikiwa kusimamia shughuli za uchunguzi wa mwili wa ndugu yao.

Mollel alifariki Mei 20 mwaka huu majira ya usiku akiwa hotelini jijini Dodoma alikokwenda kumsindikiza Mbunge mpya wa Jimbo la Arumeru Mashariki, Dk.John Pallangyo, aliyeapishwa jana.

Kabla ya kifo chake, Mollel alikuwa mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Meru na Halmashauri Kuu ya CCM katika Wilaya hiyo na alishika nafasi ya udiwani kati ya mwaka 2010 hadi 2015 katika Kata ya Mbuguni.

Askofu alikuwa miongoni mwa wachimbaji wachache wa madini waliofanikiwa na kuendelea kuishi kijiji alichozaliwa cha Mbuguni wilayani Arumeru, kilometa chanche ulipo migodi ya madini ya Tanzanite katika eneo la Mirerani.

Askofu atakumbukwa zaidi kwa tukio la mwaka 1995, baada kupata madini ya Tanzanite aligawa fedha kwa kuzirusha akiwa ghorofani katika jengo lake la Hotel ya Pallaons ikatikati ya Jiji la Arusha.

Mbali na kuwa mchimbaji wa madini na mwanasiasa, Molle pia alikuwa mwanamichezo ambaye ulifanikiwa kuanzisha timu ya soka ya Pallson ikiwa na makazi yake kijijini Mbuguni.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo serikali utekelezaji katazo la mifuko ya plastiki

**UTEKELEZAJI** wa katazo la serikali dhidi ya matumizi ya mifuko ya plastiki, kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira ulikuwa umeibua wasiwasi na hofu kubwa katika jamii.

Makundi ambayo yalikuwa yameingiwa na hofu kubwa kwamba yangeathirika zaidi ni watumiaji na wauzaji wa mifuko hiyo; kwamba wangekutana na bughudha ikiwamo vipigo kutoka kwa watendaji na mgambo.

Serikali ilishatangaza kwamba mwisho wa matumizi ya mifuko hiyo ni Juni mosi mwaka huu, na kutangaza kanuni ambazo zinaainisha adhabu zikiwamo faini kwa watakaokiuka katazo hilo kwa kuiagiza kutoka nje, kuisafirisha, kuiuza na kuitumia.

Licha ya kuwapo hofu ya kibano hicho, pia kulikuwapo na wasiwasi kuhusiana na upatikanaji wa mifuko mbadala. Hata hivyo, serikali imekuwa ikisisitiza kwamba tayari mifumo mbadala mbalimbali itakuwapo na itapatikana kwa urahisi.

Hata hivyo, jana serikali ilitoa maelezo yenye ufafanuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa katazo hilo utakavyokuwa, huku ikiwatoa wasiwasi wananchi kuwa hakutakuwapo na matumizi ya nguvu kama walivyokuwa wakihofia.

Kimsingi, maelezo yaliyotolewa na viongozi wa serikali wenye dhamana jana yameondoa hofu na wasiwasi uliokuwapo katika jamii kuhusiana na utekelezaji wa katazo hilo.

Serikali iliwataka watendaji na watumishi wa mkoa wa Dar es Salaam, kutotumia nguvu kuwapiga virungu wananchi watakaokutwa na mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi, mwaka huu. Aidha, amepiga marufuku watendaji watakaosimamia kazi hiyo kutoingia kwenye maduka, ofisi na kwenye magari ya watu kutafuta mizigo ya mifuko ya plastiki.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), January Makamba, ndiye aliyetoa angalizo hilo jana, wakati akizungumza na watendaji wa mkoa wa Dar es Salaam, wakiwamo wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi, madiwani, wenyeviti na watendaji wa kata na mitaa, wasimamizi wa masoko, maofisa afya, mazingira na biashara kujadili utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki.

Makamba alisema kuwa katika utekelezaji wa sheria hiyo mpya inayoanza, serikali hatutegemei kuona watu wanaendelea kubeba mifuko.

ma wanapigwa virungu na mgambo kisa wamebeba mifuko na wala haitegemei kuona watu kuporwa mali zao.

Alieleza katika utekelezaji wa sheria hiyo, watendaji watakaosimamia kazi hiyo hawapaswi kuingia kwenye ofisi, maduka na kufungua magari ya watu kutafuta mizigo ya mifuko ya plastiki.

Alisema katika utekelezaji wa jambo hilo, mwananchi ambaye atakutwa amebeba au mfanyabiashara anayeuza mifuko ya plastiki ndiye atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Hatua ya serikali kutoa ufafanuzi huo ni ya kupongeza kwa kuwa sasa wananchi hawatakuwa tena na hofu ya kubughudhiwa, na kwa kuzingatia kuwa mpango huo utaenda sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu udhibiti wa matumizi ya mifuko hiyo.


Ushauri wetu ni kuwa watendaji wazingatie maelekezo hayo ili kuondoa uwezekano wa kusababisha usumbufu usio wa lazima, kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia utekelezaji wa baadhi ya operesheni husisan mgambo wanapokuwa wakisimamia usafi katika maeneo ya miji.

Ni matarajio yetu kuwa mamlaka husika kama Ofisi ya Makamu wa Makamu wa Rais (Mazingira), Tamisemi na Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (Nemc) zitafuatilia kwa ukaribu kuhakikisha hakuna mkanganyiko wala uonevu kwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



Na Salome Kitomari

## Muungwana Lazima Nilonge

# Bodi ya Utalii nchini ipanue wigo zaidi wa kujitangaza

**ZIPO** jitihada mbalimbali za kutangaza vivutio vya utalii kitaifa na kimataifa, lengo likiwa ni kuongeza idadi ya watalii na hivyo mapato yatokanayo na sekta hiyo.

Utalii ni sekta ya kwanza nchini kuchangia pato la taifa kutokana na hifadhi za taifa, mapori ya akiba, maeneo yaliyohifadhiwa, utalii wa maeneo ya historia na wa asili.

Jitihada za kutangaza utalii zimefanyika ikiwamo kushiriki kwenye maonyesho ya kidunia, ambayo huleta pamoja watu kutoka maeneo tofauti duniani ambapo Tanzania hupata nafasi nzuri katika ramani ya dunia vivutio vyake kuzidi kufahamika.

Kutokana na jitihada hizo, Tanzania ilipokea hivi karibuni watalii zaidi ya 1,000 kutoka Israeli na wengine 300 kutoka China.

Kimsingi, utangazaji upo wa namna nyingi, mathalani kupitia mashirika makubwa ya ndege, treni za miji na majiji mbalimbali, mitandao ya kijamii, tovuti, majarida makubwa na yanayosomwa na watu wengi.

Pamoja na hatua hizo, Mjadala unaona kwamba jitihada hizo zinapaswa pia kufanywa kwenye soko la ndani kwa maana ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

ATCL inapaswa kuwa na majarida yenye kuelezea utalii Tanzania, ili abiria anapopanda ndege hizi, iwe kwa safari ya ndani au nje ayasome na hivyo kuvutika kutumia fedha zake kwenye utalii.

Hivi karibuni, nilipanda ndege ya ATCL kwenda na kurudi jijini Dodoma. Miongoni mwa abiria walikuwa ni raia wa kigeni ambao wamekuja nchini kwa shughuli mbalimbali za uwekezaji, lakini pia kuonana na viongozi wakuu jijini humo.

Ndani ya ndege hiyo kulikuwa na majarida lakini sikuona jarida lolote linaloelezea vivutio vya utali vilivyopo nchini.

Badala yake kulikuwa na majarida ya bidhaa na vitu vingine ambavyo ni muhimu, lakini ingependeza zaidi kama yangekuwapo pia ya kutangaza vivutio vya utalii.

Vilevile, nilitumia usafiri wa Shirika la Ndege la Uturuki (Turkish) katika moja ya safari zangu ambapo kulikuwa na jarida la Skylife, ambalo zaidi ya kurasa nane ndani yake zilikuwa zinatangaza utalii wa Kenya.

Katika jarida hilo kuna maelezo juu ya uhamaji wa wanyama kwenda Maasai Mara wakishawishi watalii kuitembelea hifadhi hiyo.

Kwamba watembelee ili waone uhamaji wa makundi makubwa ya nyumbu, lakini pia wanyama wakubwa watano wanaopatikana hapo.

Katika habari hiyo yenye kichwa 'Masai Mara: The Home of safari, kuna picha mbalimbali za makundi ya nyumbu yakikatiza mto Mara na ushiriki wa jamii ya Masai kwenye utalii wa asili, huku kukiwa na picha ya mtoto wa Kizungu akifundishwa kuwinda na kijana wa Kimasai.

Jarida hilo huandikwa kwa lugha mbili za Kiingereza na Kituruki, lengo likiwa kuwafikia watu wengi zaidi wanaozungumza lugha hizo.

Pia nilitembelea Jiji la Geneva, Switzerland. Huko nako Kenya inajitangaza vyema na zaidi ikibainisha kwamba kwamba ukitembelea nchi hiyo utauona na kuupanda Mlima Kilimanjaro kirahisi.

Katika moja ya treni inayofanya safari zake za kila siku kwenye jiji la Geneva ilikuwa na mabango ya kulitangaza Shirika la Ndege la Kenya, pamoja na vivutio vya utalii vilivyopo nchini humo, ukiwamo muonekano wa Mlima Kilimanjaro na theluji yake. Aidha, wameweka mabango ya hoteli na maeneo ya mapumziko kwa watalii, yakisema kwamba wataona wanyama na baada ya hapo watakuwa na eneo zuri la porini kwa ajili ya mapumziko yao.

Haya yote yanafanyika wakati Geneva imepokea wageni zaidi ya 500 kutoka mataifa mbalimbali duniani, wanaohudhuria mkutano wa wadau wa Umoja wa Mataifa wa kupunguza athari za maafa (United Nation Disaster Risk Reduction- UNDRR).

Treni yenye matangazo hayo hufanya safari zake kati ya eneo liitwalo Nations ambako kuna ofisi zote za Umoja wa Mataifa, kuelekea katikati ya jiji la Geneva.

Hii ni mbinu ya kutangaza vivutio na kuteka soko la Ulaya, kwani ni rahisi kwa mtalii kuelewa atakachokipata akiitembelea Kenya.

Kwamba ataona vivutio vyote vinavyotangazwa kwa maana ya uhamaji wa makundi makubwa ya wanyama na Mlima Kilimanjaro, hivyo kutumia muda mwingi na fedha zaidi nchini humo.

Mjadala unaona kuwa kazi nzuri imefanywa na Bodi ya Utalii Tanzania, lakini bado jitihada zaidi zinahitajika kujitangaza.

Hiyo ni pamoja na kupata nafasi kwenye majarida makubwa ya mashirika ya ndege kama Turkish, lenye zaidi ya ndege 500 zinazokwenda maeneo yote ya dunia.

# Tamwa yatoa tamko vitendo vya ubakaji

**Na Enock Charles**

MKURUGENZI wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Rose Reuben, amevitaka vyombo vya dola kuchukua hatua zinazostahili kwenye matukio ya ubakaji yalioibuka mkoani Kigoma ambayo ni maarufu kwa jina la "Teleza".

Akizungumza na Nipashe jana, mkurugenzi huyo alidai matukio hayo ya ubakaji yanaweza kusababisha waathiriwa wa tatizo hilo ambao ni wanawake kuingia katika uhusiano wa kimapenzi na wanaume wanaofanya ukatili huo kwa lengo la kupata ulinzi.

"Vyombo vya dola vifuatilie tatizo hili kwa sababu inashangaza sana kuona vitendo hivi vinaendelea wakati tuna polisi na vyombo vingine vya usalama," alisema Rose.

Akizungumza bungeni juzi, Mbunge wa Kigoma Mjini, (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, alihoji sababu za kile alichokiita kufumbia macho vitendo hivyo viovu licha ya kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeshapata taarifa kutoka kwa viongozi na wananchi.

Zitto alisema utafiti uliofanywa na taasisi zisizokuwa za kiserikali, umebaini kuwapo kwa vitendo vya unyanyasaji, huku serikali ikiwa haijachukua hatua zozote za haraka na za kisheria.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari wiki tatu zilizopita, asasi sita za kiraia nchini ikiwamo Taasisi ya Utafiti ya Twaweza, zilizofanya utafiti wa suala hilo ziliitaka serikali ichukue hatua haraka dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyojulikana kama teleza, ambavyo vinahusisha kubaka na kujeruhi wanawake.

Vitendo hivyo kwa mujibu wa taarifa ya taasisi hizo vinatajwa kukithiri katika eneo la Mwanga Kusini mkoani Kigoma, hadi sasa wanawake 45 wamebainika kutendewa ukatili ikiwamo kujeruhiwa kwa mapanga au visu.

# IFAD yaombwa kuendeleza kilimo TZ

**Na Peter Haule,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Gilbert Houngbo na kuiomba Taasisi hiyo kusaidia kuendeleza zaidi sekta ya kilimo kupitia mpango wake mpya wa awamu ya 11 wa kuendeleza kilimo nchini.

Dk. Mpango aliyataja baadhi ya maeneo ya kipaumbele kuwa ni uzalishaji wa mbegu bora, kusaidia kilimo cha umwagiliaji, kutafuta masoko ya uhakika ya mazao ya wakulima, upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na kuanzisha taasisi za utafiti wa kilimo za kikanda.

Aidha, Dk. Mpango alimwomba kiongozi huyo kusaidia pia mbinu za kupunguza upotevu wa mazao wakati na baada ya mavuno ili kuchochea na kuongeza tija katika sekta ya kilimo ambayo alisema inaajiri zaidi ya asilimia 66 ya Watanzania.

"Takiribani asilimia 66 ya Watanzania wanategemea kilimo na ndio mwajiri mkuu hivyo kwa kuwa IFAD ina programu mpya, tumeamua kushauriana ili wajue vipaumbele vya serikali na fedha tutakazo zipata tuzielekeze katika maeneo hayo," alieleza Dk. Mpango.

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA**
**AT MWANZA**
**RM.CIVIL CASE NO. 29 OF 2019**
**ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF**
**VERSUS**
**ASMA K. JABIL………………………………DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
1. ASMA K. JABIL
OF MWANZA

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA**
**AT MWANZA**
**RM.CIVIL CASE NO. 24 OF 2019**
**ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF**
**VERSUS**
**EDWIN G. NYAMTABA………………………..DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the **SEAL** of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
EDWIN G. NYAMTABA
OF MWANZA

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA**
**AT MWANZA**
**RM.CIVIL CASE NO. 29 OF 2019**
**ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF**
**VERSUS**
**KASSIM H. SINGASINGA……………………..DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
KASSIM H. SINGASINGA
OF MWANZA

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA**
**AT MWANZA**
**RM.CIVIL CASE NO. 24 OF 2019**
**ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MALIYAHEWA D. SINGU…………………………DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
1. MALIYAHEWA D. SINGU
OF MWANZA

# Mpina amshukia Tizeba bungeni

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameshukia bungeni Waziri wa zamani wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Tizeba, kwa kuingilia utendaji wa maofisa wa wizara yake.

Vilevile, waziri huyo ameliomba Bunge kuipa muda serikali kuangalia kama kuna haja ya kufuta tozo ya Dola za Marekani 0.4 kwa kila kilo ya samaki wanaovuliwa bahari kuu.

Mpina aliyasema hayo bungeni jana jioni alipokuwa anahitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema serikali ya awamu ya tano hakuna namna inavyoweza kumwonea mtu kwa kuwa sheria zote ambazo inazitekeleza zimetungwa na Bunge.

Alisema wakati mwingine hata wabunge hugeukana anapokamatwa mtu waliye na uhusiano naye wa karibu.

"Amezungumza hapa Mheshimiwa Tizeba, Tizeba alikuwa Waziri wa (Kilimo), Mifugo na Uvuvi, lakini hata hili la kuzungumza kuwa vijana wanawaonea watu wake siyo kweli," alisema.

Mpina aliongeza: "Mheshimiwa Tizeba amekuwa akiwapigia simu vijana wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi 'kuwa-harass' na kuwaambia akiwa waziri hataki watu wake wakamatwe kwa uvuvi haramu."

Waziri Mpina alilieleza Bunge kuwa Dk. Tizeba pia amekuwa akiingilia utendaji wa watumishi wa wizara hiyo hata sasa akiwa mbunge kwamba hataki mtu wake akamatwe.

"Sasa ukifika hapa (bungeni) unabadilika kwa sababu hawa vijana hawako ndani ya Bunge, hili unawashutumu kwa kiwango hicho, siyo vizuri. Vijana wetu wanafanya kazi vizuri sana lakini kama wakifanya vibaya, tuletee tutawashughulikia tu," alisema.

Kuhusu hoja ya baadhi ya wabunge kutaka serikali ifute tozo ya Dola 0.4 kwa kila kilo ya samaki wanaovuliwa bahari kuu, Mpina alisema kuna haja serikali ipate muda wa kuliangalia kwa kina suala hilo kabla ya kufikia uamuzi huo.

Mpina aliwataka wabunge kuitendea haki nchi kwa sababu jambo hilo limeanzia ndani ya Bunge.

"Watu walikuja na meli zenye ukubwa wa hadi tani 300, wanalipa leseni ya Dola za Marekani 65,000 (Sh. milioni 150) pekee yake. Mbona hamjajiuliza tena samaki akivuliwa hapa anauzwa shilingi ngapi hadi waseme kuwa tuiondoe hiyo Dola 0.4?" Mpina alihoji.

Waziri huyo alisema Bunge ndiyo liliiambia serikali kuwa nchi imechoka kudhulumiwa na kuonewa na meli za uvuvi zinazotoka nje ya nchi.

Alisema baada ya kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano, ilitekeleza kwa kubadili kanuni mwaka 2016 kwa kuweka mrabaha wa Dola za Marekani 0.4.

"Waziri aliyekuwapo, Mheshimiwa Tizeba, alitoa 'holiday' ya miezi sita wasilipe Dola 0.4, alipotoa likizo ya Dola 0.4, Kamati ya Bunge ikabaini dosari na Tanzania imepoteza Sh. bilioni tano kwa 'holiday' ile.

Mpina aliendelea kuhitimisha hoja akisema: "Waziri aliyekuwapo, aliweka kanuni na jana (juzi) aligeuka kuwa mlalamikaji ya kwamba mimi 'nime- frastuate' (nimevuruga) kwa 0.4.

Wakati wa mjadala huo juzi, Dk. Tizeba ambaye pia

Mbunge wa Buchosa (CCM), alisema uvuvi umekuwa kizunguzungu na kwamba yeye alifanya marekebisho makubwa ya kanuni.

Hata hivyo, Dk. Tizeba alisema baadhi yametekelezwa, lakini marekebisho katika Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu ambayo yana mwaka mmoja, bado haijaingiza fedha.

"Tumetunga sheria na kanuni ili ituongezee mapato ama ipoteze mapato? Naiomba serikali jambo hili lifanyiwe tafakari," alisema.




Mkurugenzi wa Mawasiliano Airtel Tanzania, Beatrice Singano na Mkurugenzi wa Masoko Isaack Nchunda, wakionyesha bango baada ya kuzindua huduma mpya inayojulikana kama 'Tamba Mitandao Yote', jijini Dar es Salaam jana, yenye lengo la kuwapa wateja wake suluhisho na uhuru wa kuchagua huduma ya mawasiliano ambayo ni nafuu zaidi wakati wowote hata kama mteja hajajiunga na bando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JK aibua hoja utawala bora, umaskini

INATOKA UK. 2

kiafrika ni vyema zikiendana na sera zote zilizopo kwenye nchi husika.

Alisema kizazi cha kati kinachopata nafasi ya kushika uongozi, baadhi yao wamekuwa wakiongoza katika maslahi yao binafsi.

"Kutokana na hali hiyo, kuna wakati lilibainika pengo la uongozi katika baadhi ya nchi, tofauti na walivyokuwa wakiongoza kina Jomo Kenyatta na Mwalimu Nyerere," alisema.

Tamasha hilo la siku tatu kuanzia Mei 22 hadi 24 ni la wazi kwa watu wote, na linatajwa kuendelea kuwavutia wasomi wa nchi mbalimbali hasa za Afrika.

Wazungumzaji wakuu ni Prof. Patrick Lumumba kutoka Kenya, Ali Mufuruki atazungumzia kuhusu soko huria na dola, huku Profesa Georges Ntalaja, raia wa Kongo anayeishi Marekani atazungumzia kuhusu utawala bora na siasa. Profesa Paul Zeleza kutoka Malawi, Dk Suzan Kavuma Uganda atazungumzia kuhusu hali ya Uganda na kuendeleza viwanda.

Tamasha hilo linaendeshwa chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,lengo likiwa ni kuhuisha mawazo ya Mwalimu Nyerere kwa kuwezesha yatumike katika kuleta chachu ya maendeleo nchini na Afrika kwa ujumla.

# Mifuko mbadala ya plastiki kuuzwa 70/-

INATOKA UK. 5

mbuzi ambao hufariki.

Pia alilishauri Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta) kuweka kipaumbele cha mafunzo ya uzalishaji wa mifuko mbadala pamoja na teknolojia ya kutengenezea ili kuleta matokeo chanya na makubwa nchini.

Kwa upande wake Mhandisi Allen Kimambo, alisema licha ya kuwa utoaji huduma hiyo utaanza kwa changamoto, wanatarajia ushirikiano kutoka serikalini katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Aliwataka Watanzania kuendelea kuhamasika kuzalisha mifuko mbadala na kuunga mkono juhudi za kutokomeza mifuko ya plastiki ambayo madhara yake ni makubwa kiafya, kiuchumi na kimazingira. Naye Mwanasheria kutoka Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (Nemc), Vincent Haule, alisema wapo kwenye hatua za mwisho za kutoa viwango vya mifuko mbadala vinavyotakiwa kutumika.

Alisema wanashirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuandaa ubora wa bidhaa ambazo zitatakiwa kutumika nchini na watatoa maelekezo hivi karibuni.

Kunzia Juni Mosi, mwaka huu mifuko ya plastiki haitatakiwa kutumika nchini, baada ya serikali kutoa katazo hilo kwa mujibu wa sheria na adhabu ya atakayekutwa na bidhaa hiyo ni kutozwa faini ya Sh. 30,000.

# Wastaafu wa PSSSF sasa wasotea pensheni miezi 4

INATOKA UK. 3

2011, na alishahakiki taarifa zake na alikuwa akipata pensheni ya kila mwezi, lakini kwa sasa hapati na kwamba ndiyo fedha aliyokuwa anaitegemea kwa ajili ya kuendeshea maisha yake.

Mwingine alistaafu mwaka 2017 na kwa miezi minne sasa hajalipwa pensheni ya mwezi, kwa sababu ya kuelezwa kuwa majina yao hayajaingizwa kwenye mfumo.

Meneja wa PSSSF mkoa wa Ilala, James Mlowe, alipozungumza na wastaafu hao mwezi uliopita, alithibitisha kuwapo kwa tatizo hilo kutokana na mfumo mpya baada ya mifuko kuunganishwa, na kwamba katika kuingiza majina ya wastaafu wapo waliosahaulika licha ya kufanya uhakiki.

"Tunafanya tuwezalo kuwa kabla ya Mei 25, mwaka huu, wawe wamelipwa fedha zao zote za nyuma, hili ni tatizo la kimfumo lilijitokeza ila linashughulikiwa baada ya uhakiki wa wastaafu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, ambao hawajahakikiwa walitolewa kwenye daftari, wapo waliohakikiwa, lakini mfumo haukuwatambua kutokana na uchanga wa mfumo husika," alisema.

Alisema PSSSF ina wastaafu 124,000, na kwamba kitakachofanyika ni kuandaa malipo kwa ajili ya wachache ambao majina yao yalirukwa wakati wa kuingiza taarifa kwenye mfumo.

# Ugonjwa wa fistula bado tishio nchini

**Na Yasmine Protace**

TAKWIMU zinaonyesha Tanzania inakadiriwa kila mwaka wanawake wanaoripotiwa kwenda hospitali kwa matibabu ya ugonjwa wa fistula ni takribani wagonjwa wa fistula 1,200 hadi 3,700.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Programu ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, Dk. Felista Bwana kutoka Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), wakati akizungumzia Siku ya Maadhimisho ya Kutokomeza Fistula Duniani ambapo kila mwaka ufanyika leo.

Alisema kulingana na takwimu za magonjwa wanaokwenda kutibiwa kwenye hospitali zinazotoa matababu ya fistula, Tanzania inakadiriwa kuwa na wanawake takribani 1,200 hadi 3,700 ambao kila mwaka huripotiwa kuugua ugonjwa huo.

Alisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa ripoti zinatokana na Hospitali ya CCBRT na Shirika la AMREF.

Alisema takwimu za dunia zinaonyesha wanawake na wasichana zaidi ya milioni mbili inakadiriwa wanaishi na tatizo la fistula hasa nchi za kusini mwa Jangwa la Saraha, Asia na Uarabuni.

Alisema ugonjwa huo unatibika na matibabu yake hutolewa bure kwa wahusika.

"Inakadiriwa kuwa takribani wanawake na wasichana 100,000 hupata tatizo jipya la fistula kila mwaka, pamoja na juhudi zimefanyika lakini bado upo uhitaji mkubwa wa kuwasaidia waathirika kwa sababu tatizo linazuilika na walio wengi wametibiwa kwa njia ya upasuaji," alisema.

Pia, alisema tangu mwaka 2003 UNFPA limeendelea kuongoza na kuratibu kampeni za kutokomeza ugonjwa huo kwa kushirikiana na wadau wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, alisema ugonjwa huo hujitokeza kwa wingi Afrika hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia na kwamba mataifa ya magharibi wameshautokomeza.

Alisema kwa mwaka huu maadhimisho hayo yamebebwa na kauli mbiu isemayo, 'Fistula ni Ukiukwaji wa Haki za Binadamu inatakiwa kutokomezwa'.

Alisema Hospitali ya CCBRT kama wadau wakuu wa kutokomeza ugonjwa huo Tanzania, imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwenye kukinga na kutibu fistula ya uzazi.



Malori yakipakua mahindi mabichi katika soko la Temeke Stereo, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Watakiwa kuchukua tahadhari za moto

**Na Romana Mallya**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limewataka wamiliki na wakuu wa shule za kutwa na bweni ambazo hazijapatiwa mafunzo ya kinga na tahadhari ya majanga ya moto kuwasiliana na makamanda wa mikoa ili kupatiwa elimu hiyo.

Wakati jeshi hilo likieleza hayo, yako matukio kadhaa ya moto yaliyotokea kwenye shule za bweni na kusababisha hasara kwa shule husika na wanafunzi kupoteza maisha na mali zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na jeshi hilo, ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto ni pamoja na kutoa ushauri wa namna ya uwekaji wa vifaa vya kinga na tahadhari.

"Ukaguzi huu unafanyika kwa mujibu wa sheria namba 14 ya mwaka 2007 ikisomwa pamoja na Kanuni ya Vyeti ya Usalama wa Moto ya mwaka 2008 na marekebisho ya mwaka 2014 pamoja na Kanuni ya Tahadhari dhidi ya moto kwenye majengo ya mwaka 2015," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatakiwa kutoa elimu katika sehemu mbalimbali kama vile viwanda, hoteli, maduka, shule za msingi na sekondari, migodi na vituo vya mafuta. "Watumishi wa taasisi husika wanapaswa kulipia gharama ya mafunzo Sh. 20,000 kwa kila mshiriki kama ilivyoainishwa katika kanuni za jeshi hili," alisema. Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa mafunzo hayo hutolewa bure kwa wanafunzi wa ngazi zote.

# Ahimiza ushirikiano kukabili majanga

**Na Salome Kitomari**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Dorothy Mwaluko, amesema kuna umuhimu wa ushirikiano wa kikanda na kimataifa kupata misaada ya kiufundi na kifedha katika kukabili majanga ya asili na yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa mujibu wa taarifa yake aliyoiwasilisha kwenye mkutano wa wadau ulioitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Kupunguza Majanga (UNISDR) hivi karibuni, alisema Tanzania itaendelea kupambana na maafa mbalimbali kwa kuhakikisha usalama wa watu wake.

Majanga hayo ni ukame kupindukia, njaa, mafuriko, vimbunga, matetemeko ya ardhi na mengineyo ambayo huwa na matokeo hasi kwa maisha ya watu, mali, miundombinu na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Alisema kwa miaka miwili iliyopita, serikali imepiga hatua mbalimbali za kutekeleza mkataba wa Sendai wa kupunguza majanga wa mwaka 2015-2030 katika sekta mbalimbali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mwaka 2017 serikali ilitengeneza kanuni za kusimamia majanga ikiwa ni mkakati wa kuimarisha uratibu wa majanga na kukabiliana nayo," alisema.

Mwaliko alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuweka kipaumbele, bajeti kwa kadri inavyopatikana, kupunguza majanga na ustahimilivu ikiwa ni pamoja na kuimarisha uchumi.

Alizitaja jitihada mbalimbali zilizofanyika kuwa ni pamoja na kuimarisha sekta ya usafiri ikiwamo kuongeza usafiri wa majini, ardhi na anga.

Alizitaja jitihada zingine zilizofanyika ni upatikanaji wa huduma za maji safi na salama hususan maeneo ya vijijini, lengo likiwa ni kupunguza majanga kwa watu wa kipato cha chini.

Alisema kwenye upande wa sekta ya afya, serikali imeweka kipaumbele maeneo ya vijijini ambako kuna idadi kubwa ya wakazi, ikiwamo kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, pamoja na kuhakikisha wakati wa majanga wananchi wanapata huduma zote muhimu.

Katibu Mkuu huyo alisema hatua zingine zilizochukuliwa ni kuzuia uchomaji wa misitu ovyo kwa kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya wadau kulinda misitu na mashamba.

# Ataka tamko matokeo mabaya kidato cha nne

MBUNGE wa Bumbwini (CUF), Muhammed Amour Muhammed, ameitaka serikali kutoa tamko kuhusu matokeo ya mtihani wa kidato cha nne ambayo yamekuwa mabaya kwa kipindi kirefu.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema hali hiyo kwa muda mrefu haijapatiwa ufumbuzi wowote.

"Nini tamko la serikali kuhusiana na hali hiyo?" Je, ni juhudi zipi za makusudi ambazo serikali inakusudia kuchukua ili kupandisha hali ya ufaulu wa wanafunzi hao?"Alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema ufaulu wa wanafunzi katika matokeo hayo umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema katika mwaka 2018 watahiniwa waliofaulu ni asilimia 78.36 ikilinganishwa na asilimia 77.09 ya mwaka 2017, asilimia 70.35 ya mwaka 2016 na asilimia 67.91 ya mwaka 2015.

"Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza ufaulu katika ngazi mbalimbali za elimu, ikiwamo kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga na kukarabati miundombinu katika shule," alisema.

Alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, zaidi ya Sh. bilioni 93.8 zimetumika katika uboreshaji wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari 588 yakiwamo madarasa 1,190, mabweni 222 na vyoo 2,141, mabwalo 76 na nyumba 99.

Aidha, alisema serikali imeendelea kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwamo, vifaa vya maabara na katika shule na vifaa vya kielimu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Vile vile, katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Aprili 2019, serikali imeajiri jumla ya walimu 17,884 na pia serikali imeendelea kuimarisha Idara ya Uthibiti Ubora wa shule," alisema.

Ole Nasha alisema serikali imenunua na kusambaza magari 45 ya uthibiti ubora wa shule na pikipiki 2,897 kwa ajili ya maofisa elimu kata.

"Katika mwaka 2019/20 serikali inatarajia kujenga ofisi 100 za wathibiti ubora wa shule na kuongeza idadi ya watumishi. Hivyo, serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea kuimarisha ubora wa elimu nchini," alisema.



Mbunge wa Viti Maalum, Amina Mollel (kulia), akichukuliwa alama za vidole na Konstable wa Uhamiaji, Joha Senga, kwa ajili ya kukamilisha hatua za kupata pasipoti kwa njia ya kielektroniki, katika Ofisi za Bunge jijini Dodoma juzi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Viwango vya fidia uharibifu wanyamapori vyapitiwa upya

SERIKALI imesema inapitia upya viwango vya kifuta machozi kwa watu ambao mali zao zimekuwa zikiharibiwa na wanyamapori waharibifu ikiwamo tembo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge Viti Maalum (CCM), Leah Komany, ambaye alitaka kujua ni lini serikali itaongeza vifuta machozi hivyo.

"Serikali imekuwa ikichukua muda mrefu kulipa vifuta jasho, lakini pia vifuta jasho vinavyotolewa haviakisi uhalisia, serikali ina mpango gani wa kubadili kanuni zake ili kuongeza gharama?"Alihoji.

Akijibu, Kanyasu alikiri kuwa kumekuwapo na malalamiko ya muda mrefu ya kiwango kidogo cha kifuta machozi na jasho, lakini kwa sasa wizara inapitia upya viwango hivyo.

"Mara itakapokamilika itatangazwa na kuwajulisha waathiri ingawa haiwezi kulipa maisha ya mtu na mazao yaliyoharibika lakini itakuwa imeongezwa kulingana na hali ya sasa," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Busega (CCM), Dk. Raphael Chegeni, alitaka kujua mkakati wa serikali wa kudhibiti ongezeko la tembo na wanyama waharibifu ambao wamekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wanaoishi maeneo ya kando kando ya hifadhi na ziwa.


Kanyasu alisema kanuni za wanyamapori wakali na waharibifu za mwaka 2011 zimeainisha aina ya wanyamapori ambao wanapaswa kushughulikiwa kama wanyamapori wakali na waharibifu.

Alisema kwa mujibu wa kanuni hizo, jedwali la tatu limeorodhesha wanyamapori hao ambao ni tembo, kiboko, mamba, nyati, chui, samba na fisi.

Hata hivyo, alisema serikali imeweka mikakati katika kunusuru maisha na mali za wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

"Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya doria za udhibiti wanyama hao, kutumia mbinu na teknolojia mbalimbali mfano kupanda pilipili na kutundika mizinga ya nyuki pembezoni mwa mashamba, kufunga vitambaa vyenye vilainisho vya magari(oil), kuzunguka mashamba na kutumia ndege zisizokuwa na rubani kwa ajili ya kudhibiti tembo," alisema.

Alitaja mkakati wa tatu ni kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi ili waepuke kulima kwenye shoroba za wanyamapori.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Marekebisho sheria wanyama yanukia

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema hivi karibuni watendaji wa serikali wamekuwa wakiiona kama ni sehemu ya uhalifu bila kujua ni viumbe hai wenye mahitaji yao ya msingi.

Kufuatia hali hiyo, wizara inakamilisha marekebisho ya kanuni ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya mwaka 2008 na ifikapo Julai Mosi, mwaka huu, watendaji ambao wamekuwa wanakamata wanyama ovyo na kutoa visingizio kwamba wanatekeleza sheria watashughulikiwa.

Mpina alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Dk. Immaculate Semesi.

Mbunge huyo alisema kuwa kumekuwa na ukatili wa wanyama hususan kwenye migogoro, usafirishaji ambapo kumekuwa na idadi kubwa ya wanyama wanasafirishwa umbali mrefu wakiwa wamebanana.

"Serikali inajipangaje katika kusimamia hili ili dhuluma na ukatili kwa wanyama unakuwa umeisha," alihoji.

Akijibu, Mpina alisema wanyama hao wana mahitaji yao ya msingi ya malisho, chanjo na tiba na kwamba wanapokamatwa sio wahalifu.

"Baada ya kuona sasa kila ofisa wa serikali ni mkamataji mifugo tukaamua kuboresha sasa kanuni za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya mwaka 2008, na Sheria ya Mifugo ya mwaka 2003, marekebisho haya yatakuwa tayari Julai Mosi, mwaka huu,"alisema.

Waziri Mpina alisema lengo ni kushughulika na watendaji wa serikali ambao wamekuwa wakinyanyasa mifugo na imekuwa ikifa ikiwa imeshikiliwa kwa sababu zisizojulikana.

"Kama mifugo ikifa imeshikiliwa inamaana rasilimali ya taifa imekufa, sasa Julai mosi tutaanza kushughulika na watendaji hawa wa serikali wanaokamata mifugo ovyo kwa kisingizio kuwa wanatekeleza sheria bila kujua mifugo ina sheria zao zinazowalinda,"alisema.

Mpina alisema watendaji hao watashughulikiwa wao kama wao na sio serikali tena.

Awali, Naibu Waziri wizara hiyo, Abdallah Ulega, alisema serikali imeanza kufanyia kazi teknolojia ya utambuzi wa wanyama ambapo watavalishwa hereni badala ya kuwapiga chapa.

Ulega akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, ambaye alisema kuwa utaratibu wa kuwatambua wanyama kwa kuwapiga chapa kwa kuwachoma ni wa kikatili.

"Kwanini isitafutwe njia mbadala nyingine,"alihoji huku Spika Job Ndugai akiongezea kudai kuwa kumekuwa na ukatili mkubwa kwa wanyama ikiwamo kuku kubebwa miguu juu kichwa chini.

Akijib, Ulega alisema upigaji chapa ni utaratibu wa kisheria na kwamba ipo sheria ya utambuzi wa wanyama ambayo inataka mnyama atambuliwe ili kwenda sambamba na sheria za kimataifa. Alikiri kuwa kweli njia inayotumika sasa kuwaweka chapa wanyama kwa kuwachoma haifai na ndio maana wameanza kufanyika kazi teknolojia ya kuwaweka herini na wataanza na ng'ombe wa maziwa.



# Mahakama Afrika yajitambulisha Djibouti

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

RAIS wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR) yenye makao yake makuu jijini Arusha, Jaji Sylvain Ore', ameongoza ujumbe wa mahakama hiyo kwa ziara ya kikazi nchini Djibouti.

Katika ziara hiyo, mahakama hiyo inatarajiwa kufanya mazungumzo na wadau kwa lengo la kuitangaza. Mahakama hiyo iko chini ya Umoja wa Afrika (AU).

Ujumbe huo ulioanza ziara nchini humo juzi hadi Mei 24, unatarajiwa kukutana na Waziri Mkuu wa Djibouti, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Sheria na Spika wa Bunge.

Jaji Ore' alisema wakati wa ziara hiyo wataendesha semina inayolenga kukuza uelewa wa wadau hao juu ya uwapo wa mahakama hiyo na jinsi inavyoendesha shughuli zake ikiwamo kupokea mashauri.

Kwa mujibu wa Jaji Ore', uelewa wa wadau hao kuhusu uwapo wa AfCHPR pia utaleta hamasa kwa nchi nyingi zaidi za AU kuridhia itifaki iliyoanzisha mahakama hiyo na kutoa tamko rasmi la kutambua na kukubali mamlaka ya mahakama hiyo kupokea kesi za watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

"Ili mahakama kufanikisha malengo yake na pia kuimarisha mfumo wa haki za binadamu barani Afrika, nchi nyingi za Afrika hazina budi kuridhia itifaki iliyounda Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa mujibu wa kifungu cha 34(6)", alisisitiza.

Tangu mwaka 2010, mahakama hiyo imeendesha programu mbalimbali zinazolenga kutoa elimu ya uwapo wake na shughuli zake katika baadhi ya nchi za Afrika zikiwamo Chad, Ethiopia, Afrika Kusini, Ghana, Malawi, Kenya, Uganda, Zambia, Morroco na Tunisia.

Nchi zingine ni Ivory Coast, Cape Verde, Jamhuri ya Kiarabu ya Sahrawi, Misri na Guinea Bissau.

AfCHPR ilianzishwa mwaka 2006 na ilianza shughuli zake rasmi mwaka 2008.

## Wafanyabiashara madini wahakikishiwa usalama

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu, amewahakikishia wafanyabiashara wa madini usalama na kuwapo kwa usiri wa kutosha katika biashara hiyo, ili wapate fedha na kulipa kodi halali kwa serikali.

Kitundu alisema hayo jana mjini hapa wakati akizindua soko la madini la Wilaya ya Babati lililoanzishwa rasmi na kuwekwa katika jengo la Halmashauri ya Mji wa Babati, kwa ajili ya kuwahudumia wafanyabiashara hao.

"Niwahakikishie kutakuwa na usiri wa kutosha na usalama utakuwa wa uhakika kwa wauzaji wa madini watakaofika soko hili. Cha msingi tunaomba ushirikiano wa watu wote na muwe wazalendo na wachapakazi ili mkipata kipato chenu na serikali hakikisheni inapata sehemu yake kwa ajili ya maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema anaamini kuwa baada ya kuzinduliwa kwa soko hilo, wachimbaji wengi watajitokeza kwenda kutafuta leseni ili waanze kuchimba kihalali na masoko hayo yatapunguza utoroshaji wa madini na kuongeza ajira.

Mkuu huyo wa wilaya aliongeza kuwa kuanzishwa kwa soko la madini kutakuwa mkombozi kwa halmashauri kwa sababu zitapata ushuru hasa zile ambazo madini yanapatikana, hivyo zitaondokana na kulalamika kuwa madini yanazalishwa kwao na zenyewe haziambulii kitu.

Naye Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Manyara, Mhandisi Joseph Kumburu, alisema soko hilo litakuwa linatoa huduma siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kwa wiki. Alisema leseni 79 ndizo zinamilikiwa na Halmashauri ya Babati. Ofisa Madini Mkaazi Mkoa wa Kimadini Mirerani, Daud Ntalima, aliwaambia wadau wa madini kuwa serikali ilianzisha soko la madini ili wachimbaji walipe kodi, kuwa na taarifa za uzalishaji na kupata masoko ya madini.

"Serikali inawathamini sana wachimbaji wa madini, hivyo na nyie muithamini serikali kwa kulipa kodi ili kuletewa huduma za kijamii zilizo bora katika maeneo yenu na kuanzishwa kwa masoko, kutawasaidia kupata fursa nyingi za kiuchumi," alisema Ntalima.

Mwenyekiti wa wachimbaji Mkoa wa Manyara, Jastin Nyari, alisema kwa sasa wana masoko ya ndani na alitumia fursa hiyo kuiomba serikali iwapatie masoko ya nje pia huku akisisitiza kuwa hakuna mtu atakayetorosha madini wakati kuna soko hilo.

Mwenyekiti wa Masoko ya Kimataifa kutoka Chama cha Wafanyabiashara wa Madini (Tamida), Abe Latif Suleman, alisema kuanzishwa kwa masoko ya madini, kutaepusha mlolongo wa kodi, huku akisema madini ni ya pili kwa kuingiza kipato baada ya sekta ya utalii.



Mafundi wa Shirika la Umeme Nchini (Tanesco), Mkoa wa Arusha, wakibadilisha nguzo ya zamani na kuweka mpya pamoja na transfoma katika Mtaa wa Jacaranda, jijini humo jana, kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## EAC yajitosa kudhibiti magonjwa ya mlipuko

**Na Zanura Mollel,**
LONGIDO

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC), inatarajia kufanya majaribio ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko eneo la mpakani Namanga, Tanzania na Kajado nchini Kenya ifikapo kati ya Juni 11 na 14, mwaka huu.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Michael Katende, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Afya wa jumuiya hiyo, alisema jana alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari, katika ukumbi wa kituo kimoja cha forodha (OSBP) upande wa Kenya.

"Kazi hii ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko maeneo ya mpakani ni makubaliano ya mawaziri wa afya wa jumuiya hii mwaka 2015," alisema.

Alisema kazi hiyo inafanyika chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Jamii nchini Ujerumani (GIZ) na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa kushirikiana na EAC.

Dk. Katende alisema kumekuwa na magonjwa ya mlipuko maeneo ya mipakani, kutokana na mwingiliano wa watu na wakati mwingine magonjwa hayo husambazwa na wanyama na binadamu na kusababisha athari katika utalii, biashara na kilimo.

Alisema kwa sasa wanaangalia utayari wa nchi hizo mbili katika kukabiliana na magonjwa hayo na kuweka njia mbadala ya kudhibiti pindi yanapotokea kwa kuwa husababisha kuporomoka kwa uchumi wa nchi na hata maendeleo ya wananchi.

Katende aliyataja magonjwa yanayoonekana kuwa tishio na kupoteza maisha ya watu wengi kwa haraka katika Kanda ya Afrika Mashariki kuwa ni ebola, homa ya bonde la ufa, kipindupindu, kupooza, tauni na kichaa cha mbwa.

Alisema wanatarajia kukutana na zaidi ya watu 250 kutoka pande zote za nchi hizo kwa ajili ya kazi hiyo na pia kutakuwapo na wengine kutoka ndani ya EAC na kila nchi inatarajia kuwa na watu maalumu watakaoshughulikia magonjwa hayo maeneo ya mipakani.



Meneja wa Tigo Kanda ya Ziwa Kusini, Gwamaka Mwakilembe (kushoto), akifafanua jambo kwa mmoja wa mawakala wakuu wa Tigo Pesa wilayani Bariadi Mkoa wa Simiyu, Ng'esha Marenya, wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa mnara ulioboresha huduma ya mtandao wa 4G wilayani **humo jana. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wataka ukaguzi 'Day Care'

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, wametaka maofisa wa idara ya elimu wa halmashauri hiyo kupita katika kata 32 za majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo, kufanya ukaguzi wa dharura wa vituo vyote vya kutwa ambavyo vinatoa huduma ya kulea watoto wadogo maarufu kama 'Day Care'.

Lengo la madiwani hao, pamoja na mambo mengine ni kutaka kujiridhisha kama vituo hivyo vinakidhi matakwa ya kisheria ya uanzishwaji wake na huduma inayotolewa.

Diwani wa Old Moshi Mashariki, Andrew Ringo, alisema yako malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba kuna baadhi ya vituo vilivyoanzishwa mitaani havikidhi viwango vya kutoa huduma, hivyo kuwa moja ya visababishi vya kujitokeza kwa mmomonyoko wa maadili na malezi kwa watoto.

"Katika kata ya Old Moshi Mashariki tumeshachukua hatua wenyewe kuanza ukaguzi wa vituo vya kulea watoto mchana na tumepita vituo takribani vinane na pia kuvijengea uwezo wa namna ya uendeshaji," alisema.

Ringo alivitaja vituo hivyo kuwa ni Kisamo Montesori, Kikarara Montesori, Kitonyohu Montesori, Bethania Montesori, Visdom Nursery & Kindergarten, Mahoma Montesori, Montesori Usharika wa Kidia na Emnanuel Pentecost Day Care.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Exaud Mamuya, akizungumzia suala hilo, alisema kuna vituo kadhaa wana shaka navyo kama vinakidhi viwango na kujitathmini upya kama vinastahili kuendelea kutoa huduma kabla ya kufungwa.

"Kwa ujumla viko vituo ambavyo tayari nimeambiwa havikidhi matakwa ya kisheria na viwango vya utoaji huduma," alisema Mamuya.

Mamuya ambaye ni Diwani wa Marangu Mashariki, ametaka kazi hiyo ifanyike katika maeneo yote ya Moshi ili kujua kama uanzishaji wa vituo hivyo ulifuata taratibu na vinazingatia sheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Castori Msigala, alisema suala hilo litashughulikiwa na idara husika na taarifa yake itatolewa baada ya zoezi hilo kukamilika.

Ofisa mmoja wa idara ya ustawi wa jamii katika halmashauri hiyo alisema vituo vingi vinavyofunguliwa havikidhi viwango vya utoaji huduma na vina udhaifu mkubwa kama vile watoto kukosa waangalizi wa kutosha.

Moja ya majukumu ya idara hiyo ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sheria, sera, miongozo, kanuni na viwango vya ubora katika utoaji wa huduma mbalimbali za ustawi wa jamii, kufanya tathmini, ufuatiliaji na uratibu wa huduma za ustawi wa jamii. Kazi nyingine ni pamoja na kusimamia programu ya malezi, makuzi na maendeleo changamshi ya awali ndani ya kaya na katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ili kuwawezesha kukua vyema kimwili, kiakili, kijamii na kihisia.

# Wakulima kukatwa kodi kwa kuuza mahindi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu wakulima au kikundi katika Wilaya ya Moshi kinachotaka kuuza mahindi katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwenye ghala lake lililoko Arusha kuwa watakatwa kodi ya zuio ya asilimia mbili.

Kwa mujibu wa notisi iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigala, mahindi yanayopaswa kuuzwa ni yale yaliyovunwa katika msimu wa mwaka 2017/18.

Katika notisi hiyo iliyotolewa na Msigala, serikali kupitia NFRA, hivi sasa inanunua mahindi hayo katika Ofisi ya Kanda ya Mikoa ya Kaskazini iliyoko mkoani Arusha.

"Bei elekezi iliyopitishwa ghalani ni Sh. 490 kwa kilo moja. Aidha, mkulima au kikundi kitakatwa kodi ya zuio asilimia mbili na mahindi yatafanyiwa ukaguzi wa ubora kabla ya kuidhinishwa kupokewa," alisema Msigala.

Aidha, mkurugenzi huyo alisisitiza kuwa malipo ya mahindi hayo yatakayopelekwa kuuzwa ghalani, yatafanyika baada ya saa 48.

Wakati halmashauri hiyo ikitangaza kuwapo kwa suala hilo, katika maeneo ya vijiji vilivyoko ukanda wa milimani hasa Old Moshi, bei ya mahindi kwa gunia moja la kilo 100 ni Sh. 75,000.

Alipoulizwa Diwani wa Old Moshi Mashariki, Andrew Ringo, kuhusu uuzaji wa mahindi katika eneo hilo, alisema ni kweli gunia moja la mahindi limefikia bei hiyo sokoni. Masoko ya mazao kama Kwa Sadala, Wilaya ya Hai na Sanya Juu katika Wilaya ya Siha, bei ya mahindi kwa gunia moja imefikia Sh. 80,000.

# Wataka mila zifutwe kupinga ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAJUMBE 30 wa kamati za mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika Wilaya ya Rombo, wamesema kama jamii inataka kufanikiwa kudhibiti ukatili unaondelea katika ngazi ya kaya ni lazima mila ya kutumia jani chonganishi kuzima haki likataliwe.

Wazo la kutaka jamii ya Wachaga kuweka kando matumizi ya jani la kimila aina ya 'Isale' ambalo hutumika kuombana msamaha baada ya mtu kutenda kosa na kisha kumalizana kienyeji bila kufuatwa taratibu za kisheria, lilitolewa jana na mwanamke mashuhuri kutoka Kata ya Nanjara, Wilaya ya Rombo, Mwanaidi Mkumbo.

Mkumbo aliyasema hayo jana, wakati wa uhitimishaji wa mafunzo ya siku tatu ya kuzijengea uwezo kamati hizo maarufu kama Mtakuwwa.

Katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF), mwanamke huyo alisema kwa sasa ajenda yao kuu wanapokutana na kinamama kwenye vikundi ni kuwashauri kuachana na kuliabudu jani hilo chonganishi katika jamii ya Wachaga.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Rombo, Jonathan Mkama, alisema mbali na kujengewa hoja ajenda hiyo ya kushauri kupuuzwa kwa matumizi ya jani hilo, bado iko haja kwa watumishi, wafanyabiashara na watu wanaokosa muda wa kukaa na familia, kutenga siku moja kila wiki kuogesha watoto wao ili kubaini kama wana tatizo.

"Ni vyema angalau mara moja kwa wiki walao kama wanao ni wadogo uwe unajitahidi kuwaosha, ukimwogesha mtoto kama mzazi unaweza kugundua matatizo aliyo nayo," alisema.

"Utafutaji wa fedha umetutenga mbali sana na familia zetu. Watoto wamekuwa wa housigeli na hiyo imefanya hata kutojua kwamba watoto wetu wanapata ukatili wa namna gani. Ukiwa karibu na watoto wako na kuongea nao mara kwa mara wanaweza wakakuambia matatizo waliyo nayo." Aliongeza.

Aidha, Ofisa Elimu Kata, Thadeus Shayo, alishauri kuwa katika suala la ujauzito kwa wanafunzi, sheria ing'ate kote kote na itumike kukamata mwanafunzi mwenyewe, mtu aliyempa ujauzito na mzazi wa msichana ili wote washirikishwe na ijulikane ni nani ambaye anatakiwa kuwajibika.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Ikwiini, Farida Janowalah, alisema: "Sisi maofisa maendeleo ya jamii kipindi cha nyuma tulipokuwa hatuna mafungu ya kufanyia kazi za utekelezaji wa Mtakuwwa, tulikuwa tunaweza kufanya haya alisema kutumia bajeti ndogo ambayo inapatikana katika halmashauri na kutumia mashirika ya kiraia ambayo yanaisaidia halmashauri katika kutekeleza mpango wa Mtakuwwa."

# ama




Ukurasa 17

**Taharuki mlipuko wa Ukimwi kwa watoto**


Ukurasa 19

Miaka 44 zananati kijijini 'simulizi' wajawazito wakihamia mbadala


Ukurasa 14

**Unakumbuka simanzi ya Mv Bukoba?**



## DENGUE DAR

# Masaki, Tandale zimo katika maeneo 19 maambukizi tishio

Ukurasa 14

## Unakumbuka simanzi ya Mv Bukoba?

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI ilikuwa kumbukumbu ya tukio la kuzama meli ya MV Bukoba, mwaka 1996. Ni janga lenye vifo vilivyoishitua nchi.

Baada ya muda mfupi, iliundwa Tume chini ya Jaji Robert Kisanga, iliyochunguza chanzo cha ajali hiyo ya meli iliyopakia abiria kati ya 750 na 800 pamoja na wafanyakazi 37.

Kati ya hao, 114 waliokolewa wakiwa hai; wakati 391 waliopolewa wakiwa wamefariki na kuzikwa katika makaburi ya Igoma, nje kidogo ya Jiji la Mwanza. Miili mingine ilichukuliwa na jamaa kuzikwa kwao. Jumla ya miili 332 haikupatikana.

Kila mwaka, ifikapo Mei 21, viongozi wa serikali huongozana na viongozi wa madhehebu ya dini na waganga,kwenda eneo la ajali kufanya kumbukumbu.

Serikali ilimshitaki aliyekuwa nahodha wa MV Bukoba, Jumanne Rume-Mwiru, (sasa marehemu), Mkaguzi wa Mamlaka ya Bandari Gilbert Mokiwa; aliyekuwa Meneja wa Bandari ya Bukoba, Alphonce Sambo na aliyekuwa Meneja wa Bandari ya Kemondo, Prosper Lugumila.

Katika kesi ya mwaka 1998 katika Mahakama, watuhumiwa walishinda na kuachiwa huru.



Meli ya MV Bukoba, ilivyozama. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

DENGUE DAR

# Masaki, Tandale zimo katika maeneo 19 maambukizi tishio

- Mikocheni, Sinza 'hakufai'; Ilala kinara
- Mganga Mkuu aanika operesheni ilivyo




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mary Geofrey**

HIVI sasa katika maeneo mbalimbali nchini, watu wana ufahamu wa namna fulani kuhusu ugonjwa wa dengue. Hii in maana kama si kusikia, basi wameshuhudia, kuuguza au kuugua.

Kitaalamu inaelezwa kuwa, ni ugonjwa wa kitropiki unaosababishwa na virusi maarufu kama dengue.

Pia, inajulikana kama 'homa ya kuvunja mifupa' kwa sababu inamfanya mgonjwa kuwa na maumivu makali, hadi kuhisi 'mifupa yao inavunjika.'

Tangu mtu aambukizwe, dalili zake huanza wastani wa kati ya siku tatu hadi 14, baada ya kuambukizwa. Baadhi ya dalili ni homa kali, kuumwa kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungo.

> "Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja mpaka sasa na niwatahadharishe wanaoendelea kutoa taarifa za upotoshaji.

Kwa baadhi watu na mara nyingi si wengi, homa ya dengue inaweza kubadilika kwa kuhatarisha maisha. Dalili kubwa inatajwa ni kuvuja damu, kutoka mishipa ya damu.

Kwa kawaida matibabu yake yanachukua kati ya siku tatu hadi saba mgonjwa kupona. Hakuna dawa ya chanjo inayomudu kuwakinga dhidi ya virusi vya dengue.

Wakati serikali ikiendelea na mkakati wa kudhibiti mazalia ya mbu wanaoeneza homa ya dengue na kusambaza vifaa tiba vya kupima homa hiyo katika hospitali mbalimbali nchini, watu wamebuni mbinu mbadala ya kujikinga na mbu hao.

Wakazi wa jiji la Dar es Salaam, wamekuwa wakitumia mafuta ya nazi na kuamini kuwa mbu hao hawawezi kutua kwenye mwili wa binadamu. Ugonjwa huo ambao umeshamiri katika jiji la Dar es Salaam, pia mikoa ya Tanga, Pwani na Kilimanjaro iliyoanza kupata mgonjwa mmoja mmoja, ulianza kubainika Januari mwaka huu. Tayari takribani watu 2,000 wamebainika kuugua.

Baadhi ya wananchi wa jiji la Dar es Salaam, wamebuni kinga hiyo na kudai inazuia mbu wenye virusi vya homa ya dengue kutua miguuni, hivyo kuepuka kung'atwa na kupata maambukizi hayo.

Hata hivyo, Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Mohamed Kambi, anakanusha uhakika wa utaalamu huo mbadala, kudhibiti mbu waenezao homa ya dengue.

Anasema taarifa hizo ni za upotoshaji, hivyo wananchi wanapaswa kufuata taratibu za kujikinga na homa hiyo, ambazo zimetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja mpaka sasa na niwatahadharishe wanaoendelea kutoa taarifa za upotoshaji kuhusu tiba ya ugonjwa huu kupitia mitandao ya kijamii," anasema Profesa. Kambi.

**HATUA MUHIMU**

Profesa Kambi anawaasa wananchi kuendelea kuchukua hatua za kujikinga kuumwa na mbu, ikiwa ni pamoja na kutumia dawa za kufukuza mbu.

Anasema mbinu nyingine ni kuvaa nguo ndefu za kujikinga dhidi ya kuumwa na mbu na kutumia vyandarua vyenye viuatilifu, pia kuweka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba wanazoishi.

"Watu wanasema mafuta ya nazi yanazuia mbu wenye virusi vya dengue, lakini bado hatujadhibitisha kuhusu hilo. Hivyo, ni muhimu wananchi wakafuata taratibu zilizotolewa na Wizara ya Afya," anasisistiza Profesa Kambi.

Anasema, wanapaswa kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo kwa kuzuia kunga'atwa na mbu kwa kutumia chandarua chenye dawa.

Pia, anataja mbinu nyingine ni wananchi kujipaka mafuta ya kufukuza mbu mikononi na miguuni, wakiwa wamevaa nguo ndefu zinazofunika mwili kama mikono, miguu na mgongo.

Dk. Kambi anasema, Manispaa zote za jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine, zinapaswa kutekeleza mpango wa upulizaji viuatilifu katika madimbwi yanayotuamisha maji katika kudhibiti ugonjwa huo.

**INAVYOKABILIWA**

Profesa Kambi anapongeza hatua zinazochukuliwa na Mkoa wa Dar es Salaam katika kuudhibiti ugonjwa huo, inayojumuisha kunyunyizia dawa vya kuua wadudu kwa ajili ya kuangamiza mazalia ya mbu, linaloendelea sambamba na kutoa elimu watu kujikinga.

Anawataka wananchi waongeze kasi kutumia kamati za kitaalamu na sekta zote kudhibiti ugonjwa, pia kuwachukulia wanaokiuka

AFYA

# Masaki, Tandale zimo katika maeneo 19 maambukizi tishio

taratibu na sheria za usafi wa mazingira, zinazosababisha mazalia ya mbu au kutochukua tahadhari.

Profesa Kambi anawataka viongozi wa mikoa kuanzia za juu hadi chini kama vile tarafa, kata, vijiji, mitaa na vitongoji, kuchukua hatua kupambana na ugonjwa, ulioanza kusababisha athari katika ukanda wa Pwani.

“Tunasisitiza kuwa ugonjwa huu unazuilika. Tushirikiane kudhibiti mbu, kwa sababu kufanya hivyo pamoja na kudhibiti ugonjwa huu, tutadhibiti pia magonjwa mengine yanayoenezwa na mbu,” anasema Profesa Kambi.

Anarejea somo la kuangamiza mazalia ya mbu wa dengue, ni kufukia madimbwi ya maji yaliyotuama au kunyunyuzia dawa ya kuua viluwiluwi vya mbu kwenye madimbwi hayo na kuondoa vitu vyote vinavyoweka mazalia ya mbu.

Mganga Mkuu wa Serikali, anayataja baadhi yake kuwa ni vifuu vya nazi, makopo, magurudumu ya magari yaliyotupwa ovyo na vichaka jirani na makazi ya watu.

Anasema, kuna haja ya kuhakikisha maua yanayopandwa kwenye makopo au ndoo hayaruhusu maji kutuama, huku yawe yanafunika mashimo ya majitaka kwa mfuniko imara na kusafisha paa la nyumba zinazoruhusu maji kutuama.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile.



Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa. Mohamed Kambi.

### HALI IKOJE?

Takwimu zilizotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hadi wiki iliyopita, zinasema kila siku kuna watu 75 kila siku kuwa na virusi vya homa ya ndengue hali inayopelekea idadi ya wagonjwa kuendelea kuongezeka na kufika 1,901.

Kati ya wagonjwa hao, 1,809 ni wakazi wa jiji la Dar es Salaam, 89 kutoka Tanga mmoja kutoka Singida, mmoja Kilimanjaro na mmoja kutoka mkoani Pwani.

“Katika kipindi cha siku tisa ambazo wizara ilikuwa ikikusanya muenendo wa hali ya ugonjwa huu nchini, kuna ongezeko la wagonjwa 674 sawa wastani wa wagonjwa 75 kwa kila siku, ikiwa ni tofauti ya wastani wa wagonjwa 32 waliopatikana kila siku kwa mwezi uliopita,” anasema Profesa Kambi.

Kwa mujibu wa Profesa Kambi, ongezeko hilo linatokana na uelewa, kuhusu ugonjwa huo kwa wananchi.

Serikali nayo imeendeleza huduma za uchunguzi zinazoendelea kupanuka kwenye vituo vya afya katika Mkoa wa Dar es Salaam na Tanga.

Aidha, anasema idadi ya vituo vinavyopima ugonjwa huo imeongezeka hadi kufikia 19, tofauti na vituo saba vilivyokuwapo awali, ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma.

“Ugonjwa huu unapimwa kwenye vituo vyetu vya serikali na tunaendelea kuimarisha upatikanaji wa vipimo vya ugonjwa huu bure. Niwatake watoa huduma za afya wote na wananchi, watambue kuwa si kila homa ni dengue,’ anasema Profesa Kambi na kuongeza:“Chunguza au chunguzwa maradhi mengine na wataalamu kwenye vituo vyetu vya huduma ya kwanza, kabla ya kupima.”

> Dalili hizi huanza kujitokeza kati siku ya tatu hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya dengue. Hivyo ni muhimu wananchi kuchukua tahadhari.



Mbu aenezae dengue.

### KUNAKOPATIKANA HUDUMA

Anataja vituo vya serikali kunakopatikana huduma hizo jijini Dar es Salaam, ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Maabara Kuu Muhimbili, Hospitali za rufani za Manispaa Amana, Temeke na Mwananyamala.

Pia, kuna Hospitali Kuu ya Jeshi la Lugalo, Hospitali za Sinza, Mnazi Mmoja na Mbagala, pia zahanati za Vijibweni, Kigamboni na FFU Ukonga.

Mbali na Dar es Salaam, Profesa Kambi, anataja kwingine kwenye huduma hizo Hospitali za Rufani za Bombo mjini Tanga, Morogoro na Tumbi, Kibaha.

Zingine anazitaja ni Hospitali ya Utete Rufiji, Mkuranga, Mafia, na Manyara. Profesa Kambi anafafanua: “Natambua vipo pia vituo binafsi vinavyotoa huduma za upimaji. Katika mikoa mingine, ufuatiliaji unaendelea na hatujapata wagonjwa wenye dalili.”

### WIZARA INAVYOJIPANGA

Katika kukabiliana na changamoto ya matibabu, Profesa Kambi anasema serikali imeagiza vipimo vingine vya kupima wagonjwa 30,000, vinavyotarajia kuingia nchini hivi karibuni na vitasambazwa kwenye vituo vya umma mkoani Dar es Salaam na kwingineko.

“Niwatahadharishe wanaoendelea kutoa taarifa za upotoshaji kuhusu tiba ya ugonjwa huu, kupitia mitandao ya kijamii,” anatahadharisha.

Profesa Kambi anasema, wizara kwa kushirikiana na mikoa na halmashauri, imechukua hatua, ikiwamo kuandaa mpango wa dharura kukabiliana na ugonjwa huo, inayojumuisha uandaaji mwongozo wa matibabu ya ugonjwa, kuimarisha ufuatiliaji na utoaji elimu.

### DAR VITANI

Mganga Mkuu Profesa Kambi anasema, wizara imetuma timu za wataalamu kuungana na timu za Mkoa wa Dar es Salaam, kuudhibiti ugonjwa huo.

Maganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile, anataja maeneo yenye wagonjwa wengi katika jiji hilo na idadi yake katika mabano ni: Ilala (253); Sinza (223); Vingunguti (86); Kariakoo (79); Mbezi (78); Kimara (65); Masaki (56); Msasani (50); Wazo (49); Kinondoni (45); Mikocheni (40).

Maeneo mengine ni Tabata (41) Gerezani (40), Mbezi Beach (37), Tandale (38), Kijitonyama (34), Ukonga (26), Mwenge (28) na Tegeta (270.

“Hivi ndio vituo ambavyo zimetoa wagonjwa zaidi ya 25 lakini zipo kata nyingine nyingi ambazo zina wagonjwa wa homa ya Dengue katika wilaya zote za jiji hili,” anasema Dk. Ndugile.

Anasema mkoa huo unendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kujikinga na maambukizi ya homa hiyo inayosababishwa na mbu aina ya ‘Aides Mweusi’ mwenye madoa meupe ya kung’aa.

Dk. Ndugile anasema, dalili za ugonjwa huo ni homa ya ghafla, maumivu ya kichwa hususani machoni, maumivu ya viungo na uchovu.

“Dalili hizi huanza kujitokeza kati siku ya tatu hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya gengue. Hivyo ni muhimu wananchi kuchukua tahadhari.

AFYA

# MIMBA ZINAZOTOLEWA ZINAVYOITIKISA SENGEREMA

• Yashika namba mbili nyuma ya malaria • Kila anayedhamiria akimbilia dawa asili • Mabingwa hospitalini: Ni mtihani mkubwa • Binti Mchungaji asimulia naye alivyonasa

**Na Veronica Mrema**

AKIWA na matarajio ya kufika mbali kimaisha, Naomi Pastory (25), mkazi wa Busilasogwa, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza, ghafla ndoto zake ziliyeyuka kama mshumaa, pale alipopata ujauzito.

Naomi anasimulia jinsi alivyonasa kwenye penzi zito na kijana mmoja mtanashati (hakupenda jina lake liandikwe gazetini), akidokeza mkasa ulivyo: "Niliamini atakuwa mume wangu. Nikiwa na miaka 18 tulianza kujamiiana kwa siri. Nilikuwa darasa la saba,"

Anasema miezi mitatu ilipita tangu waanze uhusiano huo, hakuona siku zake na akapatwa na hofu kubwa. Anasmulia: "Mpenzi wangu alikwenda Dar es Salaam kushughulikia mchakato wa kujiunga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam."

Anaongeza: "Sikuwa na mawasiliano naye, niliogopa kuwashirikisha wazazi wangu, ni watu wa dini. Baba yangu ni Mchungaji. Mimi ni mtoto wa sita kuzaliwa. Niliogopa kuwaeleza dada zangu, sikutaka taarifa ziwafikie wazazi wakati ule.

"Miezi ilizidi kwenda, niliogopa jamii itanielewaje itakapojulikana nina ujauzito. Wazazi wengi waliwasihi watoto wao kuiga mfano kwangu," anasimulia na kuongeza, na kwamba aliamua kumshirikisha rafiki yake ambaye walishauriana na mambo mengi.

"Alinitaka nisiwe na wasiwasi, atanifichia siri yangu. Alinishauri tuitoe, alinipeleka kwa mtu nikapatiwa dawa, majani na mizizi ya miti.

"Nilirudi nikazificha nyumbani, kila nilipotaka kuvitumia, nilihisi sauti ya mama yangu 'ikipita' kwenye ufahamu wangu, niliwahi kumsikia akisema 'kutoa mimba ni hatari, mtu anaweza kufa.

"Sentensi ile ilijirudia mara nyingi kwenye ufahamu wangu. Hofu ilizidi kuniandama. Mwisho nikamueleza wazi mama. Hakuamini, akamueleza baba. Walisikitika mno, waliniuliza kwanini nilificha, niliwaeleza nilihofia yule kijana angenikimbia kwa hofu ya kukamatwa.

"Hivyo, hata yeye asingekuwa makini na masomo chuoni. Niliamini atarejea tujenge familia yetu, jamii ilinilaumu, nilinyooshewa kidole kila nilikopita, maisha yangu yalibadilika," anasema.

Naomi anasema, hayo yalitokea kipindi alikuwa anakaribia kuhitimu darasa la saba. Anasena, kilichomsaidia kutogundulika mapema ni umbile lake. Tumbo lake halikuwa kubwa mno na akafaikiwa kuhitimu masomo salama.

Hata hivyo, matokeo yake hayakuwa mazuri, hakuendelea na sekondari. Alilea mimba yake, akajifungua mtoto wa kiume.


Mshauri wa Afya ya Akili, Hospitalini Sengerema, Modesta Masala.


Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya Sengerema, Daktari. St. Marie Jose Voeten.

> **Alinitaka nisiwe na wasiwasi, atanifichia siri yangu. Alinishauri tuitoe, alinipeleka kwa mtu nikapatiwa dawa, majani na mizizi ya miti.**


Dawa za asili zinazotumika kutoa mimba. **PICHA ZOTE: VERONICA MREMA**

Anasema, hatimaye kijana yule alirejea kijijini. Siku moja akiwa ameambatana na wazazi wake, walienda kumuona mtoto. Naomi anasimulia ilivyokuwa:

"Walifurahi mtoto amefanana na baba yake. Aliahidi kumtunza. Waliondoka, wakarejea tena kutoa mahari, lakini tangu alipoondoka hadi sasa mtoto ana umri wa miaka saba, hakurejea tena. Nilipata taarifa ameoa mwanamke mwingine," anasimulia.

"Wasiwasi wangu mkubwa niliyo nao, kwa kuwa alitoa mahari, kwa mila zetu wakati wowote anaruhusiwa kuja kumchukua mwanawe. Sipo tayari!" anang'aka.

"Kinachonisikitisha zaidi, alinizalisha, akanitelekeza. Nimelea mwenyewe, hajanisaidia chochote. Hapa Sengerema wasichana wengi wanatoa mimba kwa dawa za kienyeji. Hatuna elimu sahihi ya afya ya uzazi, tunaelimishana wenyewe 'vibarazani.'

"Sasa hivi katika mahusiano, wasichana wanaona bora kupata Ukimwi kuliko mimba. Wanaume si waaminifu kabisa," anaeleza Naomi.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, akiwakemea wanaume

### MKASA WODINI

Nipashe ilihamia katika Wodi ya Kimamama katika Hospitali ya Wilaya Sengerema. Hapo katika kitanda kilichoko jirani na mlango wa kutoka wodini, amelazwa kijana, Miriam John (19).

Huyo ana maumivu makali mwilini na anazungumza kwa sauti ya chini, kwamba amelazwa hapo kupatiwa huduma ya kusafisha kizazi.

"Ni ujauzito wangu wa pili. Ule wa kwanza nao uliharibika," anasema Miriam, ambaye hata hivyo hakuwa tayari kuweka wazi sababu iliyochangia hali hiyo.

"Daktari hajaniambia sababu. Binafsi sijawahi ama kujaribu au kutoa mimba. Ilitoka nikiwa nyumbani. Nimefikishwa na jamaa zangu hapa hospitalini," anasema.

Mshauri wa Afya ya Akili, hospitalini hapo, Modesta Masala, anafafanua jambo hilo akisema, kuna kawaida ya wasichana wengi wilayani humo kutoa mimba kwa njia zisizo salama, kaktika usiri mkubwa.

"Hakuna aliye tayari kukiri. Mara nyingi tunawapokea wasichana kati ya umri miaka chini ya 20 hadi 26 kwa tatizo la kuharibika mimba. Tunapowahoji wengi, tunabaini wapo kwenye migogoro na wenza wao.

"Tunadhani pengine ni sababu mojawapo inayowasukuma kuharibu mimba. Binafsi nimewahi kukutana na msichana mmoja akiwa katika harakati za kutoa mimba. Alihofia misimamo ya wazazi, itakuwaje pindi watakapojua ni mjamzito?" anasema Modesta.

Anaendelea: "Nilimshauri asitoe. Alijifungua mtoto akampatia jina langu. Sasa ana mimba ya pili, wengi hufikishwa kwetu wakiwa na hali mbaya.

"Tunakuta wamejaribu kutoa, imeshindikana au imetoka sasa wanahitaji kusafishwa. Japo hawaweki wazi, jukumu letu ni kuokoa maisha, tunafanya kila tunachoweza kuwasaidia."

Modesta anasema mara kadhaa wameshawakamata wajawazito, wakiwa na mitishamba wodini wakati wakisubiri kujifungua. Anasimulia:

"Kuna za unga (zimesagwa tayari), nyingine ni mizizi, nyingine katika mfumo wa majimaji (akimuonyesha mwandishi wa makala mfano mmojawapo). Wanadai zinasaidia kuongeza uchungu, wajifungue mapema. Tunadhani ndizo zinazotumika pia kutoa mimba."

### MBINU ZINAZOTUMIKA

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sengerema (DMO), Peter Mao, anakiri kuwapo changamoto hiyo, akiupa ufafanuzi: "Siwezi kusema kwa kiasi gani. Wengi hawaweki wazi. Tunafahamu wapo wanatumia dawa za asili hudai kupatiwa na waganga wa kienyeji, wengine dawa za hospitali.

"Nimewahi kupata kesi (mkasa) moja ya msichana kutumia kijiti, sijui ni cha aina gani, alijichokonoa, mimba ikatoka."

Katika hilo mkazi wa Sengerema, Fausta Kimambo, ana ufafanuzi: "Nimepata kushuhudia baadhi ya ndugu zangu wakitoa mimba. Wanatumia mti wa muhogo, wanauchonga unakuwa na ncha, wanaingiza sehemu za siri na kuchokonoa mpaka mimba inatoka.

"Wengine hukoroga majivu mengi, chai ya rangi yenye majani mengi au spoku za baiskeli. Wapo wanaonunua dawa (anazitaja). Maduka ya dawa muhimu zinauzwa kuanzia 60,000 wanameza nyingi, mimba inaharibika."

### MTIHANI SENGEREMA

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa Afya Wilaya ya Sengerema, Maria Mgoa, anasema takwimu zinaonyesha zaidi ya mimba 1000 ziliharibika mwaka 2018 wilayani humo na anapngeza: "Lakini haijulikani sababu. Si rahisi kujua, wengi hawaelezi iwapo wametoa mimba au la."

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya Sengerema, Daktari. St. Marie Jose Voeten, anasema kila mwaka wanapokea wajawazito kati ya 9,000 na 10,000 wanaohudumiwa katika kliniki ya uzazi hospitalini hapo.

Anasema, katika hilo mikasa ya kuharibika mimba inashika nafasi ya pili, kati aina 10 ya wagonjwa waliopokewa na kuhudumiwa hospitalini hapo, mwaka jana.

"Takwimu zinaeleza tulipokea wanawake 850, walioharibikiwa mimba (abortion), malaria iliongoza kwa idadi ya wagonjwa 860," anabainisha.

Anaongeza: "Matumizi ya dawa za asili yapo kwa kiasi kikubwa, huwa wanazitumia katika kipindi cha 'mashimba-shimba' (ufanyaji kazi/ vibarua).

"Japo hatujui moja kwa moja mama amepata 'abortion' (utoaji mimba) kwa sababu ya dawa hizo, tunao ushahidi wa mjamzito mmoja pekee ambaye alikiri kutoa mimba kwa dawa za asili, 2018.

"Elimu ya afya ya uzazi ipo chini mno, hawaelewi athari za matumizi ya dawa hizo. Wengi huchelewa kuja hospitalini, hufika wakati tayari chupa imeshapasuka au wakati mwingine mfuko wa uzazi hupasuka, hasa ikiwa mtoto ana umbo kubwa.

"Wakati mwingine kondo la nyuma hutangulia kutoka kabla ya mtoto. Hivyo hufia tumboni. Ni hatari kubwa, wengi huletwa wakiwa na 'complications' matatizo. Kwa mfano, tunakuta mimba imetoka, lakini bado kuna kiungo kimebaki ndani," anaeleza.

> **Takwimu zinaeleza tulipokea wanawake 850, walioharibikiwa mimba (abortion), malaria iliongoza kwa idadi ya wagonjwa 860.**

Dk. Marie anataja athari mojawapo ya kutumia dawa za asili za uzazi: "Wapo wanaotokwa damu nyingi, kuna wanaopata kifafa cha mimba, maambukizi kwenye kizazi, hizi ni sababu zinazochangia vifo vya uzazi, Sengerema."

### HATARI ILIKOJIKITA

"Wilaya ya Sengerema inachangia vifo vingi vya uzazi mkoani Mwanza, mwaka 2017 vilitokea vifo 33, 2018 vifo 27 na kipindi cha Januari hadi April, 2019 vimetokea vifo saba," anasemaDk. Marie

Anataja sababu, kwamba wengi huchelewa kuanza kliniki, au hufika katika vituo vya kutoa huduma za kujifungua na takwimu zinaonyesha asilimia 39 pekee, ndiyo wahudhuriaji kliniki.

"Mtoto anapofia tumboni, hali hiyo huweza kusababisha hitilafu kwenye mfumo wa damu wa mama. Kitaalamu tunaita DIC au hupata tatizo jingine ambalo linafanana na hilo. Mama anapopata tatizo hilo, mara nyingi damu ikianza kutoka huwa haikomi, huwa haigandi kabisa," anabainisha.

INAENDELEA UK.20

## Taharuki mlipuko wa Ukimwi kwa watoto

**SINDH,** Pakistan

NI hali ya aina yake, kijiji kimoja nchini hapa kimekumbwa na mlipuko wa virusi vya HIV vinavyosababisha ugonjwa wa Ukimwi.

Hiyo ilianza na kuibuka dalili zilizojitokeza tangu miezi mitatu iliyopita, kijijini Ratto Dero, Kusini mwa nchi katika mazingira yanayotafsiriwa yenye utata.

Hadi sasa hatua zimeshaanza kuchukuliwa na daktari mmoja amekamatwa kuhusishwa na mlipuko huo ambayo waathirika wakuu ni watoto.

Inaelezwa kuwa, wazazi walijaa katika hospitali kulalamika watoto wao wanapatwa na homa za kila mara, hali inayotawaliwa na kuwapo mfululizo wa matukio hayo, kila baada ya muda.

Ili kubaini undani wa tatizo, serikali iliagiza watoto hao wafanyiwe uchunguzi wa kina kiafya na matokeo ya uchunguzi yalithibitisha kuwa wameambukizwa virusi vya HIV pasipo kujulikana chanzo kilivyo.

"Kufikia Aprili 24, watoto 15 waligunduliwa kuwa na virusi vya HIV, japo wazazi wao hawakuwa na virusi hivyo," daktari mmoja anasema.

Kutokana matokeo hayo, zaidi ya watu 607 wengi wao ni watoto kiwango cha asilimia 75, wamekutwa na virusi vya HIV baada ya fununu ya mlipuko wa ugonjwa huo, uliyozifanya familia kwenda katika kambi maalum iliyoazishwa na hospitali ya serikali ya mji huo, katika Mkoa wa Sindh.


Watoto wakipatiwa huduma ya kuangaliwa afya, mkoani Sindh. **PICHA: BBC**

Mshangao unaotawala ni kwamba, huo si mlipuko wa kwanza kutokea mahali hapo, bali imekuwa mara kadhaa katika miaka tofauti, ikiwamo kijijini hapo, mwaka 2016 watu 1,521 walikutwa na virusi hivyo.

Takwimu zilizopatikana wakati huo, kwa sehemu kubwa walioambukizwa ni wanaume na ilihusishwa na biashara ya ngono, hasa ya jinsia moja katika mkusanyiko ya kibiashara.

Wakati huo, msako mkali ulifanywa dhidi ya makundi hayo na ukahaba ulikemewa, lakini haukutoweka.

Katika maeneo ya vijijini nchini Pakistan, watu wengi hutafuta huduma za afya kutoka kwa wahudumu wasio rasmi na wanaodaiwa hawajahitimu, kwa sababu inasadikiwa hospitalini huduma ni ya gharama kubwa.

Dk. Fatima Mir, anafanya kazi katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Aga Khan, anaamini, mlipuko wa kwanza mwaka 2015 hadi 2016, ulichangiwa na udhaifu katika sekta ya afya.

"Kuna njia tatu tu ambayo mtoto anaweza kuambukizwa virusi," anaelezea na kuongeza:"Huenda ikawa kupitia maziwa ya mama anayenyonyesha akiwa na virusi hivyo, kupitia utoaji damu, au kupitia vifaa vya matibabu kama vile sindano."

Anasema, mikasa mingi ya kuambukizwa watoto inaashiria uwezekano mkubwa wagonjwa kadhaa walitibiwa katika kliniki za vijijini, kutumia sindano moja

Mtuhumiwa Dk. Muzaffar Ghangro, alikamatwa kwa kushukiwa anaeneza maambukizi ya Ukimwi kwa kutumia sindano moja, kuhudumia wagonjwa kadhaa katika kliniki yake, madai ambayo amekanusha

Inaelezwa katika mkoa husika kuna jumla ya kliniki 500 ambazo hazitimiza masharti yaliyowekwa na zimefungwa kote mkoani humo. Pia, serikali mkoani Sindh, ambako kuna athari ya maambukizi, wameanzisha uchunguzi kubaini chanzo cha mlipuko huo.

AFYA

## NUSU KARNE HAWAIJUI ZAHANATI

# Aliyejifungua na mzaliwa njiani, kila mmoja afunguka mkasa wake ulivyo

• Wachekelea TASAF kuwaletea zahanati




Hospitali ya Misheni, Ilembula, ilioyoko wilayani Wanging'ombe, imekuwa suluhisho la vilio vya tiba katika maeneo mbalimbali ya mkoani Njombe, lakini inabaki kuwa umbali mrefu kutoka kijijini Mafinga. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Elizabeth Zaya, a**liyekuwa Wanging'ombe

KULIKUWAPO kilio cha muda mrefu kinachowatesa wakazi wa kijiji cha Mafinga, Kata ya Kipengele katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging`ombe, mkoani Njombe. Hapo inazungumziwa ukosefu wa kituo cha afya cha kuwahudumia.

Watu hao walilazimika kutumia gharama kubwa ya fedha kwenda mbali kufuata huduma na wakati mwingine, katika kuhanagika huko, wamepata matatizo kabla ya kuifikia huduma.

Katika waliotaabika, wapo baadhi ya wanawake wajawazito waliowahi kupoteza maisha na waiojifungulia njiani, katika hekaheka kuwahi huduma hiyo ya afya.

Japokuwa waliandaliwa mapema na wataalamu wa afya katika vituo vya karibu vilivyowapatia huduma hiyo kuhusu kuwahi huduma kabla ya kufikia hatua ya mwisho kujifungua, wanajikuta kushindwa kuwahi huduma.

Sababu kuu katika hilo ni kubarikiwa katika maandalizi ya gharama ya kifedha kujikimu katika kipindi cha kusubiri kujifungua.

Wao wanaosema kwamba, walishawahi kuomba msaada kupelekewa kituo cha afya kupata huduma, lakini hawajafanikiwa.

> **Mimi ni mtoto wa pili. Mama yangu Josina Chaula, aliniambia alinizalia njiani baada ya kushindwa kufika hospitali kutokana na umbali.**

Baada ya kilio hicho cha muda mrefu, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(Tasaf), iliguswa na kilio hicho na kuamua kuwajengea kituo hicho cha afya, ili walau kupunguza adha kwa wakazi walio taabuni.

Tasaf kupitia msamiati wake 'Kinga ni Bora Kuliko Tiba' ilishawishika kufikisha huduma hiyo ya afya na kuweka historia mpya, tangu kijiji kianzishwe zaidi ya miaka 40 tangu kuanzishwa.

Wananchi kijijini hapo wanazungumzia namna walivyoishi kwa kuhangaika kufuata huduma ya afya mbali na gharama kubwa, wakikumbwa na mikasa ya kupoteza wapendwa wao.



Zahanati mpya iliyojengwa kijijini Mafinga, Wilaya ya Wanging'ombe, kwa msaada wa Tasaf. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

### WALIOFIKWA WASIMULIA

Rafikinjema Mgaya anasema wanalazimika kusafiri umbali mrefu kupata tiba kwenye Kijiji cha Ilembula ambako hivi ni mji mkubwa, wakitokea kijijini kwao Mafinga.

Mkazi huyo mwenye umri wa miaka 56, pia kiongozi mdau mnufaika wa Tasaf, anataja mbadala wa kupata matibabu kutoka hospitali hiyo ya Mishenni Ilembula na nyingine binafsi, ni katika vijiji vya Ikonda na Kibena.

Huyo ni mmoja wa viongozi kwenye kijiji cha Mafinga, aliyekuwa miongoni mwa wananchi waliofika kushuhudia kukamilika ujenzi wa Kituo cha Afya, mradi unaosimamiwa na Tasaf.

"Niliwahi kuzalia njiani baada ya kuzidiwa na uchungu, wakati nikipelekwa hospitali kujifungua. Mwanangu ambaye nilijifungulia njiani, yuko kidato cha nne sasa hivi," anasimulia Rafikinjema.

Anasema, ni mkasa wa wanawake wengi wa kijiji hicho waliwahi kujihungua njiani na baadhi walishapoteza maisha.

"Sababu kubwa ni kukosa fedha kwa ajili ya gharama za kusubiri muda wa kujifungua hospitalini." anasema.

Rafikinjema, anasema gharama za kusubiri kujifungua hospitali inayoaminika ambayo inamilikiwa na Misheni, inafikia Sh.80,000 na waliojifungua njiani wanatozwa faini ana hospitali Sh. 20,000, ndipo wanaopatiwa huduma.

Anasema faini, hiyo ni adhabu kwa wanaojifungua nje ya hospitali, lengo ni kudhibiti uzembe na matatizo yanayoweza kutokea wakati wa kujifungua.

Maama huyo anaeleza matarajio kwamba, kituo cha afya kilichojengwa na Tasaf, kitasaidia vijiji jirani vya Miyango na Milamba, ambavyo pamoja na Mafinga viko kwenye Kata ya Kipengele.

Rahabu Chaula (28), ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji,anayesimulia alivyozaliwa njiani kutokana na mama yake kushindwa kufika hospitali, baada ya kuzidiwa na uchungu njiani.

"Mimi ni mtoto wa pili. Mama yangu Josina Chaula, aliniambia alinizalia njiani baada ya kushindwa kufika hospitali kutokana na umbali," anasema Chaula.

Anayaeleza mapokeo hayo, kwamba ni kijiji chao kimepata mkombozi na kwamba mradi wa hospitali hiyo ni chaguo la wananchi na waliojitolea nguvu kufanya kazi, kama vile ufyatuaji na ubebaji matofali.

"Hiki ni kituo cha serikali, tofauti na vingine ambavyo vya binafsi," anasema Rahabu na kuongeza kuwa, hospitali hiyo ni msaada wa kuwaondolea gharama zilizowafika kinamama.

### MRATIBU TASAF

Mratibu wa Tasaf katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Joyce Mdemwa, anasema mradi huo ulibuniwa na wananchi wenyewe baada ya kutaabika kwa miaka 43 kufuata matibabu kwenye maeneo ya mbali.

INAENDELEA UK.20

AFYA

KIMANZICHANA MAGHARIBI

# Miaka 44 zananati kijijini 'simulizi' wajawazito wakihamia mbadala

**Na Yasmine Protace,**
Mkuranga

KANUNI ya afya inaweka bayana kwamba, mama anapojigundua ana ujauzito, tayari anawajibika kuhudhuria kliniki, ili aweze kupata elimu na maelekezo ya kiafya, yatakayomsaidia kupata mtoto katika hali salama.

Pia, manufaa ya elimu hiyo kliniki, inamsaidia kupata elimu ya malezi ambayo itamsaidia ili mtoto aweze kukua vizuri, katika afya bora na kimsingi ni haki yake kifya na kisheria, ambako ananufaishwa na huduma ya chanjo.

Kanuni na miongozo ya afya, inashauri mtoto mdogo ahudhurie kliniki kwa kipindi kisichopungua umri wa miaka mitano kumhakikishia ulinzi wa kiafya.

Hivi karibuni Nipashe ilifanikiwa 'kutinga'katika kijiji cha Kimanzichana Magharibi, wilayani Mkuranga, ambako wanakijiji hao wako katika kero tangu zama za miaka 44 sasa.

**DIWANI KIMANZICHANA**

Diwani, Ally Ndipitipi, anasema kumekuwapo azma ya kujengwa zahanati, kiwanja kilichotolewa na mmoja wa wanakijiji tangu zama za mbunge Adam Malima, aliyejitolea matofali na mbunge wa sasa Abdallah Ulega, naye akafanya hivyo.

Ndipitipi anasema, alijitolea matofali kwa kushirikiana na wananchi, lakini ujenzi wa zahanati bado umesuasua hadi sasa na kwamba, kukosekana zahanati katika kijiji hicho, wanakijiji wanahangaika kufuata huduma katika vijiji vingine.

"Mkuranga ina kata 25, inakuwaje kijiji kinapatiwa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuongeza katika ujenzi wa zahanati," anahoji Diwani Ndipitipi na kuongeza: "Fedha hizo ni ndogo, zitaishia katika kupauwa, lakini nyumba ya Mganga Mkuu na vyoo, haviwezi kupatikana,"

Kilio cha Diwani huyo ni kwamba, Halmashauri ya Mkuranga, iwaonee jicho la huruma na kuwasaidia kiwango kingine cha fedha, ili waweze kumalizia jengo hilo.

**MWENYEKITI HALMASHAURI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga Juma Abeid, anasema wilaya inatambua afya ya kila mwananchi na hata sera ya nchi, inaelekeza kuwapo na vituo vya afya au zahanati.

Anasema katika mwaka ujao wa fedha, zahanati ya Kimanzichana imetengewa Sh. milioni 20, kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wake.

**VIONGOZI WA KIJIJI**

Said Abdallah, ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji, anayeomba mashirika yajitokeze kuwawezesha kuchangia, ili zahanati yao ikamilike

Pia, anaishukuru Halmashauri ya Wilaya Mkuranga kutoa fedha hizo, lakini analalamika fedha walizopewa Sh. milioni 10, ni kidogo na kinaishia kupauwa jengo la zahanati pekee.

"Tumepata pesa, lakini kinachosikitisha baadhi ya wanakijiji kugoma kuchangia na kudai nchi imepata uhuru michango sio kazi hao," anasema Abdallah.

Kiongozi huyo anasema, halmashauri iwaongezee pesa ujenzi ukamilike na kuwapunguzia kero wanakijiji, kwenda maeneo ya mbali kutafuta huduma hiyo.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Kimanzichana Magharibi, Ally Abdallah, anakiri wakazi wake kuhangaika katika kufauta matibabu.

**WASEMAVYO WAKAZI**

Subira Kizaza, ni mkazi wa kijijini Kimanzichana Magharibi, analia kwamba ni hali inayowalazimu kwenda vijiji vya mbali kupata huduma hiyo.

Anasema, mwanamke anayekumbwa na ujauzito, hawezi kumudu gharama za kwenda katika vituo vya afya vya binafsi (vya misheni) kujifungua, kutokana na gharama kubwa.

"Kijiji hakina kituo cha afya, wajawazito hatuna uwezo wa kwenda katika vituo vya Misheni kujifungua na hali hiyo inachangia kujifungua majumbani au kutumia wakunga wa jadi," anasema.

Subira anasema, wajawazito na watoto hawahudhurii kliniki kutokana na umbali uliopo, kwani kwenda kliniki wanapaswa kutumia usafiri wa bodaboda kwa gharama ya Sh. 20,000, kwenda na kurudi.

Anafafanua kwamba kinachowafanya washindwe kuhudhuria huduma za vituo vya afya ni gharama kubwa za mahudhurio ya kliniki, akiitaja kila mwezi Sh. 6,000.

Pia, anasema katika hilo, mtu anapofikia hatua ya kujifungua, kwa kawaida gharama yake ni Sh. 30,000 na upasuaji Sh. 300,000.

Subira analalamika kwamba, kutokana na vipato vidogo, wanashindwa kuhudhuria kliniki na hata kuwapeleka watoto kwa ratiba iliyopo ya kila mwezi, kwamba imekuwa mtihani kwao, wanaishia mbadala wa kubaki nyumbani.

Mama huyo anayejitambulisha kuwa mjane na ana watoto wanne, anasema changamoto inayomkabili ni pale anapoumwa, watoto wanakosa msaada kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ( Tasaf), kutokana na hali aliyo nayo.

Hadija Juma anasema kijiji chake kina zahanati, lakini ujenzi wake haujulikani siku ya kukamilika, hivyo wanaomba wadau wa kiserikali kuwaelekeza jicho la huruma, kuchangia ujenzi kituo cha afya kijijini.

Ndicho kilio alicho nacho, Zainabu Juma, akilalama ujenzi wa zahanati umeanza miaka mingi na wanaendelea kuwa kizani, kuhusu kukamilika kwake.

Mkazi, Asha Hemed, anataja hangamoto nyingine mbali uzazi na malezi, ni matukio ya watu kugongwa na nyoka kijijini kwao, hasa katika mashamba yaliyotelekezwa, waathirika wakubwa wakiwa watoto.

"Mtoto akigongwa nyoka matibabu yake ni Sh.10,000 hadi 12,000 katika hospital binafsi. Kutokana na uwezo kuwa mdogo, tunalazimika kuwapeleka wapate tiba mbadala," anasema.

**OFISA LISHE**

Vumilia Dandago, anasema manufaa ya mjamzito kuudhuria kliniki, ni kumuwezesha kupata elimu itakayomsaidia kujifungua salama.

Anasema mjamzito anapohudhuria kliniki, ananufaika na elimu lishe na jinsi ya kumtunza mwanawe, hali inayomsaidia asipate upungufu wa damu, ikiwamo kunusurika na kifafa cha mimba.

Vumilia anasema, watoto wana haki ya kuudhuria kliniki kupata chanjo ambazo ni kinga na mkombozi katika maisha yao na watoto walio na sifa ya kuudhuria kliniki, wana nafasi ya kubwa ya kibali salama kiafya.



Jengo la zahanati Kimanzichana Magharibi, ambalo halijakamilika kwa miaka mingi. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

> "Mtoto akigongwa nyoka matibabu yake ni Sh.10,000 hadi 12,000 katika hospital binafsi. Kutokana na uwezo kuwa mdogo, tunalazimika kuwapeleka wapate tiba mbadala.

AFYA

# MIMBA ZINAZOTOLEWA OVYO ZINAVYOITIKISA SENGEREMA

INATOKA UK.17




Dk. Marie anasema, katika kukabili changamoto hiyo, Wilaya ya Sengerema, sasa imeanzisha mafunzo maalum kuwaelimisha wakunga na waganga wa jadi athari za utoaji mimba kienyeji.

"Tunafuatilia vifo na kuvijadili kwa kina, ili kuchukua hatua zaidi, tumenunua dawa na vifaa tiba vya kutosha. Tunaelimisha kupitia Radio Sengerema na wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHW), kwenye kaya na mfumo wa rufaa umeimarishwa," anasema Maria.

### SHERIA ILIKOSIMAMIA

Julius Titus, Mshauri wa Kisheria katika shirika lisilo la kiserikali nchini la Pathfinder, anasema hakuna sheria nchini inayoruhusu utoaji mimba.

"Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, vinavyoanzia kifungu cha 150 hadi 152 vinazungumzia adhabu ya mwanamke aliyetoa mimba, aliyemtoa na aliyesaidia kufanikisha utoaji mimba.

"Inatamka, anayetoa (mara nyingi ni daktari) atafungwa miaka 14 jela. Mwanamke anayetolewa, atafungwa miaka saba, aliyesaidia kufanikisha utoaji atafungwa miaka mitatu jela," anafafanua kuwa ni vigezo vinavyowafanya wanawake kutafuta huduma hiyo kwa siri.

### WAZIRI UMMY

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema utoaji mimba usio salama ni changamoto inayochangia asilimia 18 ya vifo vitokanavyo na uzazi.

"Sheria zetu zinakataza kutoa mimba, isipokuwa zinaruhusu ikiwa labda kuna sababu za kiafya, hasa ikiwa ujauzito unaweza kuleta athari kwa afya ya mama au mtoto aliye tumboni.

> **"Ni kosa la jinai kutoa mimba kulingana na sheria zetu, hatujabadilisha sheria, mimi siwezi kuhamasisha ifanyiwe marekebisho.**

"Pale mimba imetoka au ametoa, anachosaidiwa ni kusafishwa kizazi. Sasa kwanini watu wanatoa mimba mimi naona kwa sababu hawataki kuzaa," anasema waziri.

"Ni kosa la jinai kutoa mimba kulingana na sheria zetu, hatujabadilisha sheria, mimi siwezi kuhamasisha ifanyiwe marekebisho.

"Kikubwa kwetu (Wizara) ni kuhakikisha tunahamasisha jamii kutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, mtu aamue mwenyewe azae lini na nani, wapi badala ya kutoa mimba.

"Kama 'abortion' imetokea, tuna mwongozo wa huduma baada ya mimba kuharibika wa mwaka 2015 (comprehesive post abortion care), unatumika katika vituo vya kutoa huduma za afya.

"Mama anapatiwa huduma anazostahili, hatuulizi sababu ya mimba kutoka, hatuulizi kwanini amechoropoa, hiyo ni 'non of our business' ( si wajibu wetu), akifikishwa hospitalini tunamchukulia kama mgonjwa.

"Siwezi kuwa 'champion' (kinara wa kuruhusu utoaji mimba, japo najua zipo nchi zimeruhusu. Kama mtu amebakwa, hatuna namna tena, tutakachozingatia sisi ni kuelimisha njia za kisasa za uzazi wa mpango," anasisitiza.

### WATAFITI WATAMKA

Ripoti iliyochapishwwa mnamo Machi 31, 2016 katika mtandao wa Chuo Kikuu cha Guttmacher, Marekani, inakadiriwa kila mwaka wanawake milioni moja nchini wanapata mimba zisizotarajiwa, asilimia 39 zinatolewa.

Ni zao la utafiti uliofanywa na Chama cha Madaktari Bingwa wa Uzazi na Magonjwa ya Wanawake Tanzania (AGOTA), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na wenzao wa Guttmacher.

Pia, inataja utoaji mimba usio salama ni ya pili kuchangia vifo vya kinamama na wasichana.

### TAKWIMU ZA WHO

Shirika la Afya Duniani (WHO), linakadiria kila mwaka kuna mimba zipatazo milioni 25 hutolewa katika njia zisizo salama, kulingana na ripoti yake ya 2010/2014.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe: veronicaromwald@gmail.com na simu: Simu; (+255) 0758 218 013***

## Aliyejifungua na mzaliwa njiani, kila mmoja afunguka mkasa

INATOKA UK.17

Anasema kipato cha wananchi katika kijiji hicho ni kidogo, hivyo kutokana na umbali wananchi wengi hawakuwa na uwezo wa kumudu gharama za kufuata matibabu kwenye maeneo hayo.

Mdemwa anasema hospitali hiyo inatarajiwa kukabidhiwa kwa wananchi na huduma kuanza kutolewa mwezi ujao.

Anasema hospitali hiyo iliyojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 65.2 ushiriki wa wananchi ulikuwa ni nguvu zao na pia wameongeza jengo lingine mbali na yaliyofadhiliwa na Tasaf.

Mkakati wa Serikali hivi karibuni Serikali ilitangaza kujenga Hospitali za Wilaya 67, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuimarisha sekta ya Afya nchini.

### JAFFO

Akizungumza redioni hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo (pichani), anasema serikali itatumia Sh. bilioni 105 kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali nchini.

"Tangu tupate uhuru tulikuwa na hospitali za wilaya 77, lakini sasa Serikali ya Awamu ya Tano inaenda kuweka historia kwa mageuzi makubwa yanayofanyika katika sekta hii ya afya na tumejipanga kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata huduma bora za afya," anasisitiza Jafo.

Anafafanua kuwa serikali imeweka historia kwa tangu lipate uhuru, kulikuwapo vituo vya afya vinavyofanya upasuaji 115 nchi nzima, lakini katika mwaka wa fedha 2017/2018, serikali imejenga vituo vya afya vyenye uwezo wa kufanya upasuaji 208 vinavyoenda sambamba na ujenzi wa hospitali za wilaya, zinazoanza kujengwa mwaka huu.

Anasema, bohari Kuu ya Dawa (MSD) imeshapatiwa fedha za kusambaza vifaa tiba katika vituo vya afya ili vianze kufanya kazi.

### HISTORIA YA AFYA

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, kabla ya Uhuru, huduma za afya nchini zilitolewa zaidi kwenye maeneo ya shughuli za kiuchumi, kama vile miji na mashamba makubwa.

Lakini baada ya uhuru, serikali iliweka msukumo zaidi kupanua huduma za afya, ili kuwafikia wananchi wa vijijini.

Katika hilo, serikali iliweka mfumo wa rufaa wa huduma za afya, ambazo mwendelezo wake ulijenga ngazi za zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa, maalum, kanda na taifa, ambazo zilianzishwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ulioidhinishwa mwaka 2007 na kuanza kutumika mwaka 2008.

Katika hilo, inalenga kila kijiji au kitongoji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya, wilaya inatakiwa kuwa na hospitali.

Vivyo hivyo, hospitali za rufani zinatajwa kuwa ni za ngazi ya mkoa, kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). Aidha, serikali inahamasisha kuwezesha hospitali za mashirika ya kidini kushirikiana nayo kutoa huduma kwa wananchi, kupitia makubaliano maalumu.

Mojawapo ni baadhi ya hospitali binafsi kuingia mkataba na serikali, kutoa huduma kwa niaba ya hospitali za serikali, katika maeneo yenye pengo la huduma hiyo. Kwa ujumla, kipaumbele kikuu kinachosimamia sera na miongozo mbalimbali ya tiba ni " kinga ni bora kuliko tiba.'

## Wakulima wadogo waitwa vikundini

**Na Cynthia Mwilolezi,** MBEYA

TAASISI ya kuendeleza mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT) kwa kushirikiana na wadau wa taasisi za fedha nchini, zimewahimiza wakulima hasa wadogo kujiunga katika vikundi ili waweze kupata mikopo na pembejeo, kwa ajili ya kulima kilimo chenye tija.

Akizungumza wakati wa kongamano la wadau wa zao la alizeti, lililofanyika mkoani hapa, Meneja wa zao hilo wa

AMDT, Martin Mgallah, alisema njia pekee ya kumkomboa mkulima wa alizeti nchini ni kumwezesha kuwa na uwezo wa kupata mikopo kutoka katika taasisi za kifedha.

"Sisi tunatambua wakulima wengi nchini hasa wadogo wanapata vikwazo kupata mikopo, katika taasisi za kifedha ila wakijiunga katika vikundi watapata mikopo na pembejeo na kulima kilimo chenye tija na hasa alizeti," alisema Mgalla.

Mgalla alisema taasisi imekusudia kumwinua mkulima wa alizeti nchini na itaendelea kushirikiana na wadau wake kuhakikisha wakulima wanakuwa katika vikundi, ili viweze kuwa na sifa ya kukopesheka.

Alisema AMDT imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali katika mikoa 15 nchini, na zaidi ya wakulima 150,000 wamekwisha fikiwa kupitia mradi huo.

Mmoja wa wakulima wa alizeti na msindikaji wa mafuta ya alizeti, Anita Mwakyoma, alisema kumekuwapo na changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, hali ambayo imekuwa kikwazo katika kuwasaidia wakulima wadogo wa zao hilo.

"Ni ukweli usiopingika wengi wetu licha ya kuvutiwa na kilimo cha alizeti, kutokana na hamasa na elimu ambayo tumekuwa tukiipata kutoka kwa wadau wetu wa kilimo, lakini tunashindwa kufanya kilimo chenye tija, kutokana na uwezo wetu kuwa mdogo," alisema Anita.

Alisema pamoja na ugumu wa upatikanaji wa mikopo, bado wakulima wengi wameshindwa kumudu bei za mbegu bora za alizeti zinazopatikana sokoni na hivyo kulazimika kutumia mbegu zisizokuwa na ubora, ambazo zimekuwa hazitoi mbegu za kutosha hali ambayo inayomfanya mkulima asinufaike na kilimo.

Naye mkulima wa alizeti katika Mkoa wa Songwe, Sophia Mwanandenga, aliziomba mamlaka zinazohusika na kilimo, hususani upande wa pembejeo kuangalia namna zitakavyomsaidia mkulima kupata mbegu bora kwa bei nafuu.

Akijibu hoja ya upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo, Mwakilishi wa Benki ya Posta (TPB), Tawi la Mbeya, Leonard Katamba, alisema kwa muda mrefu mkulima mdogo amekuwa hakopesheki, kutokana na kushindwa kufikia vigezo vilivyowekwa na baadhi ya taasisi za fedha.

"Kwa kutambua mchango wa mkulima katika ukuaji wa uchumi nchini, TPB tumeanzisha mpango maalumu wa kuwahamasisha wakulima kujiunga na vikundi, hatua ambayo itakuwa ni msaada kwa mkulima kuweza kupata mikopo pindi atakapokuwa anahitaji," alisema Katamba.

# Maonyesho kilimo yatumika kuwapa mbinu wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanzisha maonyesho ya kilimo ya mazao mbalimbali kwa kutumia mashamba darasa ili kutoa elimu kwa wakulima na kuwapatia mbinu za kuzalisha mazao mengi kibiashara.

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuwainua wakulima kiuchumi na kuwakinga wananchi na baa la njaa. Alisema uamuzi wa kuanzisha maonyesho hayo waliufanya baada ya kubaini wakulima wengi hawafuati kanuni bora kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha.

Alisema hali hiyo inawafanya wakulima washindwe kuzalisha mazao mengi, hivyo kusababisha waendelee kuwa maskini huku wakinyemelewa na baa la njaa.

"Tumefanya utafiti na kubaini wakulima wengi wanalima bila kufuata kanuni za kilimo, suala hili linasababishwa na wakulima kutokuwa na elimu, mbinu, ujuzi na teknolojia za kilimo bora, ndio sababu tumeanzisha maonyesho ya kilimo kwa kutumia mashamba darasa ili tuwafundishe kwa vitendo," alisema Dk. Bucheyeki.

Baadhi ya maofisa kilimo walioshiriki kuandaa maonyesho hayo walisema ipo changamoto ya wakulima wengi kutoshirikiana na wataalamu wa kilimo hali ambayo inawafanya washindwe kutatua matatizo ya kilimo kwenye maeneo yao.

Regina Kimario alisema ili kuwasaidia wakulima wengi kupata elimu ya kilimo bora, wameamua kuweka maonyesho hayo mahali pa wazi kando kando ya barabara kuu ya Tanzania na Zambia jijini Mbeya, ili kutoa fursa kwa wakulima wengi kufika na kupata teknolojia na mbinu za kilimo bora.

"Kuna changamoto ya wakulima wengi kutoshirikiana na wataalamu wa kilimo kwenye shughuli zao, hili pia ni tatizo linalowafanya wakulima kushindwa kutatua matatizo yao, hivyo maonyesho haya tumeyaweka mahali hapa pa wazi ili kila mtu afike na kujifunza mbinu bora za kilimo," alisema Kimario.

Baadhi ya wananchi ambao walifika kwenye maonyesho hayo walikishukuru Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole kwa ubunifu huo wakisema kuwa utasaidia sana wakulima kupata elimu ya bure hasa kwa kuzingatia kuwa hakuna gharama wala kiingilio kwenye maonyesho hayo.



Mfanyabiashara wa ndizi (kulia), akijadiliana jambo na mpagazi, wakati akisubiri wateja kando ya Barabara ya Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. Mkungu mmoja wa ndizi uliuzwa kwa bei ya 20,000/- hadi 40,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Diwani amkingia kifua mtendaji tuhuma za matumizi ya mil. 10/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO ulioibuka kati ya wenyeviti wa mitaa ya Kata ya Iyela na wenyeviti wa mitaa ya Nero na Mapambano kuhusu matumizi ya shilingi milioni 10 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya shule, umechukua sura mpya baada ya Diwani wa Kata hiyo, Charles Mkera kudai wenyeviti wana maslahi binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu mgogoro huo, Mkera alisema sio kweli kwamba fedha za ujenzi wa vyoo hivyo zimetafunwa kama wanavyodai wenyeviti wa mitaa na kwamba fedha hizo zinaendelea kufanya kazi iliyokusudiwa.

Alisema Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyela baada ya kupokea fedha hizo, ilipokea pia maelekezo kutoka katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji hilo juu ya matumizi ya fedha na kwamba maelekezo hayo ndiyo yanayozingatiwa.

Mkera alisema miongoni mwa maelekezo waliyopewa ni pamoja na kununua vifaa vinavyotakiwa kwenye mradi huo badala ya kupeleka fedha.


"Tatizo lililopo ni kwamba wenyeviti wanataka wapewe fedha hizo ili wanaponunua mchanga wawe wanapata 10,000 suala ambalo halikubaliki maana serikali ya sasa ni tofauti kabisa na ilivyokuwa miaka ya nyuma," alisema Mkera.

Alisisitiza kuwa walitekeleza maelekezo ya Mkurugenzi wa Jiji kwa kupeleka fedha kwa wazabuni wanaowapelekea vifaa, huku akidai kuwa baadhi ya vifaa vilishanunuliwa na vimehifadhiwa kwenye ofisi za shule hizo.

Alisema wenyeviti wa mitaa ndio wanaotakiwa kusimamia ujenzi wa vyoo hivyo na sio kazi ya ofisa mtendaji wa kata wala diwani na kwamba wao kazi yao ni kufuatilia utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, baadhi ya wajumbe wa Kamati za Shule hizo za Nero na Mapambano waliomba Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya kuwasaidia kumlazimisha Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Anna Spalika, ili ahudhurie kikao na kuwasomea mapato na matumizi.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya wazazi wa Shule ya Msingi Nero, Amos Mwakalinga, alisema wao wasiwasi wao ni kwamba fedha za mradi huo zimeliwa na viongozi wa kata hasa ofisa mtendaji na diwani.

Alisema awali walikuwa wanashindwa kuwatuhumu kwa sababu walikuwa bado hawajawaita kwenye kikao cha aina yoyote kwa ajili ya ufafanuzi, lakini baada ya kuitisha vikao vitatu ambavyo watumishi hao wamevikacha ndipo walipoanza kuwa na wasiwasi.





# Vijiji 7,000 sasa vina umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Umeme Vijijini (REA), umefikisha nishati hiyo katika vijiji, 7,000 kati ya 12,268 vilivyoko nchini huku ukitakiwa kuhakikisha makandarasi wana kamilisha miradi kwa wakati.

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Innocent Luoga, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha kujadili mpango kazi na bajeti ya REA kabla ya kuwasilishwa bungeni makadirio ya Wizara ya Nishati ya mwaka 2019/20.

Katika kikao hicho, Luoga ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. Hamis Mwinyimvua, alisema kikao hicho kimewakutanisha wadau wa maendeleo wanaochangia miradi ya nishati nchini na kwamba ifikapo mwaka 2021 vijiji vyote vitakuwa vimefikiwa na huduma hiyo.

Aliwataja washirika wa maendeleo ambao wamekuwa wakisaidia masuala ya nishati ni Norway, Sweden, Uingereza, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID), Ujerumani, Benki ya Dunia na Ufaransa.

"Ili miradi ya umeme ikamilike kama ilivyopangwa na kutimiza azma ya serikali ya kufikisha umeme katika vijiji vyote 12,268 ifikapo 2021, ni vyema REA wakawasimamia kwa karibu makandarasi hao ili utekelezaji wake uende kwa wakati," alisema.

Alisema REA inatakiwa kuhakikisha inawasimamia ipasavyo makandarasi 29 waliopewa kazi ya kupeleka umeme vijiji ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati.

"Azma ya serikali ni kufikisha Tanzania katika uchumi wa kati kupitia viwanda na nishati ya umeme ni nguzo muhimu katika kufikia azma hiyo," alisema.

Kamshina Luoga alisema pia lengo la kuwafikishia wananchi umeme katika vijiji vyote ni kuhakikisha nishati hiyo inachangia pato la taifa kwa asilimia 10 kutoka asilimia saba ya sasa na kupunguza umaskini hadi kufikia asilimia 16 kutoka asilimia 28.7 za sasa ifikapo 2022.

"Tunalenga kuongeza upatikanaji umeme wa uhakika na kwa bei nafuu kwa kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka megawati 1,600 hadi megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025," alisema.

Alitoa wito kwa wadau wa maendeleo kuwekeza katika miradi mbalimbali ya nishati na kuwahakikishia matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa, usambazaji sawa wa miradi kwa lengo la kuwanufaisha wanawake, watoto, wanaume na watu wenye ulemavu.

Naye Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, kipaumbele chao ni kuona mabadiliko ya maisha ya Watanzania kwa kuunganishwa na umeme.

Aidha, alisema wametekeleza miradi ya majaribio katika eneo la vijijini kwa kuwapa mikopo nafuu ili kubadilisha hali zao za kiuchumi kuwa bora.

"Miradi hii ya majaribio inaenda vizuri kwa wananchi walikopewa kujihusisha katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwa na mashine za kukoboa na kusagia, saluni, bekari za kuokea mikate," alisema.

Alisema kampeni maalum kwa watu waliounganishwa na umeme ili kuanzisha biashara ndogo imekuwa baraka kwa wengi na mwaka jana zaidi ya watu 240 walipata ajira za kudumu.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (mwenye suti), akiangalia maziwa ya kampuni ya Asas Dairies Milk, yaliyotolewa bure kwa wabunge kwenye viwanja vya Bunge Dodoma jana. Kushoto ni Mwakilishi wa kampuni hiyo, Mkoa wa Dodoma, Lupyana Chengula. **PICHA PETER MKWAVILA**

# TPSF yabainisha vikwazo sekta binafsi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Salum Shamte, amesema sheria ya kodi, viwango vya juu vya kodi na nguvu kubwa inayotumika katika zoezi la kukusanya kodi imeathiri ujasiri wa sekta binafsi na kusababisha biashara nyingi kufungwa.

Shamte aliyasema hayo jijini hapa juzi, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa majadiliano ya sekta binafsi Kanda ya Kati ikiwa sehemu ya maadhimisho ya kutimiza miaka 20 ya taasisi hiyo.

Alisema biashara zipatazo 16,000 zimefungwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

"Tanzania katika suala la mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara imeendelea kushuka kutoka nafasi ya 137 duniani mwaka 2016 hadi nafasi ya 144 mwaka 2017 kama inavyoonyeshwa katika ripoti ya Benki ya Dunia ya urahisi wa kufanya biashara ya mwaka 2018.

"Tunamshukuru Rais (John Magufuli) pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango (Dk. Philip Mpango) kwa kulitambua hili na kulikemea vikali. Tumewasilisha mapendekezo yetu serikalini ya namna ya kuboresha kodi tukitambua kuwa sekta binafsi lazima tulipe kodi kuchangia maendeleo ya taifa letu," alisema.

Aidha, alisema pia matukio ya kuwanyanyasa, kuwatisha na hata kuwaweka ndani wawekezaji na wafanyabiashara kwa amri za wakuu wa mikoa na wilaya yalikithiri na kuanza kuvuruga uhusiano kati ya sekta binafsi na ya umma.

"Mheshimiwa Rais amelikemea hili nalo na tunashukuru pia kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Utawala Bora wamelikemea na kusisitiza kuwa sheria hiyo muhimu isitumike kwa kutisha na kuwaweka ndani watu holela hata kama hakuna dalili za uvunjaji wa amani," alisema.

Alisema wameelezwa kuwa wanayo haki ya kumshtaki kiongozi yeyote atakayetumia madaraka hayo nje ya sheria na kwamba mwanasheria mkuu hatamtetea.

Vile vile, alisema changamoto nyingine katika suala la uwekezaji ni upatikanaji wa mitaji ambayo imekuwa tatizo ambalo limeathiri hasa wazawa na vijana.

Alifafanua kuwa vyanzo vya mitaji vya ndani vimeshindwa kukidhi mahitaji ya mitaji kwa wawekezaji wa ndani.

"Matokeo yake ni kwamba mataifa kadhaa ya nje yameona hali hii ni fursa kwao na hivyo wameanzisha mifuko, ili kuwawezesha wananchi wao kuwekeza nje ya nchi zao," alisema.

Aliongeza kuwa changamoto nyingine ni kukithiri kwa wingi wa taasisi za udhibiti na gharama zao zinazopandishwa kiholela na matumizi mabaya ya sheria, ambazo zimetumika hata kufunga biashara.

Hata hivyo, alisema ni muhimu kutenganisha majukumu ya serikali ya kusimamia, kuratibu na kuisaidia sekta binafsi ishamiri kuliko kuwa mstari wa mbele kushindana nayo hasa kwenye miradi kama ya ujenzi, viwanda na huduma.

## Pinda awapa somo wafugaji nyuki

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewashauri wafugaji nyuki na wafanyabiashara wa asali kuunda ushirika wenye nguvu ili kuwezeshwa mbinu za ufugaji bora na masoko.

Ushauri huo aliutoa juzi alipozungumza kwenye kufunga maonyesho ya ufugaji nyuki duniani yaliyoadhimishwa kitaifa katika Viwanja vya Nyerere Square, jijini hapa.

"Wengi wana ujuzi wa asili kwenye ufugaji nyuki lakini wanatakiwa kuwezeshwa mbinu bora za kisasa za ufugaji nyuki ili kufikia kiwango bora cha masoko ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema ushirika huo utawasaidia kujuana na kusaidiana katika kutatua changamoto ya masoko na namna ya kuhifadhi katika ubora unaotakiwa.

Aidha, Waziri Mkuu mstaafu Pinda alisema asali ni chakula kwa baadhi ya makabila na wakati mwingine imekuwa ikitumika kama dawa kwa watu mbalimbali.

"Kuna kabila moja la Wahadzabe liko huko mkoani Singida wamekuwa wakiishi kwa kutumia asali kama chakula chao kikuu na afya zao zipo vizuri," alisema.


Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, alisema maadhimisho hayo yameshirikisha washiriki 17 kutoka mikoa mbalimbali nchini pamoja na taasisi nane.

Dk. Mwakalukwa alisema maonyesho hayo kitaifa yalianza Mei 18, mwaka huu, kwenye viwanja vya Kumbukumbu vya Mwalimu Nyerere na kufikia kilele jana.

Naye Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala, alisema maonyesho hayo ya nyuki duniani yanafanyika kwa mara ya kwanza baada ya Umoja wa Mataifa (UN) kutangaza rasmi Desemba 20, 2017.

Dk. Kigwangala alisema baraza hilo lilitangaza maadhimisho ya nyuki duniani kwa sababu ya umuhimu wa mdudu nyuki kusaidia katika ikolojia ya duniani kuchavusha mimea.

Alibainisha kuwa wizara itahakikisha inawasaidia wafugaji nyuki kujenga viwanda vya kuchakata asali kila wilaya kwa mikoa 10 kupitia vikundi katika bajeti yake ya 2019/2020.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, katika mkutano wa utekelezaji wa mpango kazi wa wizara hiyo, uliofanyika Ikulu Ndogo Kibweni Zanzibar jana. Kushoto Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi na (wa pili kulia) ni Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee na waziri wa wizara hiyo, Dk. Sira Ubwa. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wawakilishi walilia sera ajira kubana wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka serikali kutayarisha sera ya ajira ambayo itakuwa mwongozo na kuwabana wawekezaji wa kigeni na kuwalazimisha kuajiri wafanyakazi wazalendo nchini.

Mwakilishi wa Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, aliyasema hayo wakati akichangia bajeti ya makadirio mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2019-2020.

Juma alisema hakuna sera ya ajira ambayo inawaelekeza wawekezaji wa nje kuajiri wafanyakazi wazalendo katika sekta mbalimbali ikiwamo hoteli za kitalii. Alisema hoteli nyingi za kitalii zimeajiri wafanyakazi wa kigeni kwa visingizio mbalimbali ikiwamo hakuna wafanyakazi wazalendo wenye sifa.

"Tunapiga kelele sana katika suala la ajira kwa wafanyakazi wetu wazalendo katika sekta za hoteli za kitalii...njia pekee ya kudhibiti na kukabiliana na tatizo hilo ni kutunga sera itakayowabana wawekezaji hao kuajiri wafanyakazi wazalendo," alisema.

Naye Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema wapo wawekezaji wengi wa nje ambao hawatoi kipaumbele cha ajira kwa wafanyakazi wazalendo.

Alisema njia pekee ya kuwabana ni kuweka sheria madhubuti na kuhakikisha wafanyakazi wazalendo wanapata ajira.

Alieleza zipo baadhi ya nchi ambazo mwekezaji anapokwenda kuwekeza anapewa masharti ikiwamo kuhakikisha asilimia fulani ya ajira zinakwenda kwa wazalendo.

"Sasa wakati umefika tuhakikishe kwamba tunatunga sera zitakazowabana wawekezaji wanaokuja kutoa ajira kwa wafanyakazi wazalendo ili wafaidike na sekta ya uwekezaji," alisema.

Mwakilishi wa Chaani, Nadir Abdulatif Yussuf, aliwapongeza wawekezaji wazalendo aliwamo Mwenyekiti wa makampuni ya Azam, Said Salim Bakhresa, kwa kutoa nafasi nyingi za ajira kwa wafanyakazi wazalendo katika kampuni zake.

Alisema Bakhresa ameajiri sehemu kubwa ya wafanyakazi kutoka Zanzibar, hivyo wazalendo kufaidika na uwekezaji wake.

# SMZ yapewa 5 kuimarisha redio jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, Mwantatu Mbaraka Khamis, ameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha redio jamii ambazo zimesaidia kuelimisha wananchi na kufikisha ujumbe wenye malengo maalumu.

Mbaraka alisema hayo wakati akisoma maoni ya kamati hiyo katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema redio jamii zinafanya kazi nzuri ya kufikisha taarifa zenye ujumbe wa kuelimisha jamii katika maeneo ya elimu, sekta ya afya na maendeleo.

Alieleza redio jamii zilizopo katika kisiwa cha Pemba zimefanya kazi kubwa katika kutoa ujumbe wa amani na utulivu na kuwataka wananchi kufanya kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Aliitaja redio jamii ya Micheweni ni mfano wa kuigwa kwa kutoa elimu inayohusu masuala ya wanawake na watoto pamoja na umuhimu wa lishe kwa afya ya watoto.

"Mheshimiwa Spika, redio jamii ziliopo nchini zimetusaidia kwa kiasi kikubwa kufikisha ujumbe wa masuala mbalimbali yanayoihusu jamii pamoja na kuimarisha amani na utulivu," alisema. Aliiomba serikali kuwawezesha wafanyakazi wa redio jamii kwa kuwapatia mafunzo ikiwamo ya kozi fupi ili kuendesha redio hizo. Zipo jumla ya redio jamii nne zinatoa taarifa kwa wananchi vijijini ikiwamo ya Tumbatu, Makunduchi kwa Unguja na Pemba na redio jamii Micheweni, Mkoani.

Kuhusu Kamisheni ya Utalii, Mbaraka aliitaka kuongeza wigo wa masoko ambayo yatawawezesha kupata watalii wengi.

Alisema utafiti umefanywa na kubaini kwamba bado yapo masoko mengi zaidi ya watalii ambayo hayajafikiwa vizuri ikiwamo katika nchi za iliyokuwa Jamhuri ya Urusi.

"Kamisheni ya utalii ifanye kazi ya kupenya na kutafuta masoko mapya ya utalii ikiwamo katika bara la Asia lenye idadi kubwa ya wananchi," alisema.

Kamati imeipongeza kamisheni ya utalii kwa kuvuka malengo ya kupokea watalii 500,000 hata kabla ya wakati uliopangwa kwa mwaka 2020.

# Elimu mjumuisho yachochea ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya walimu 40 wamepata masomo ya stashahada ya elimu ya mjumuisho, hivyo kufundisha wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu kwa ufanisi.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu, Zaina Abdalla Salum, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuwapatia elimu wanafunzi wenye mahitaji maalumu walemavu.

Akijibu hoja, Said alisema walimu 1,800 wamepata mafunzo ya kazi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuleta ufanisi katika kazi za kufundisha.

Alisema mafunzo waliyoyapata walimu yatawawezesha wanafunzi kupiga hatua kubwa ya maendeleo na ufaulu baada ya kupata watendaji wenye uwezo na mbinu za kisasa.

Aliitaja mikakati iliyoanza kuchukuliwa ni pamoja na matayarisho ya kamusi ya lugha ya alama ambayo itawawezesha watu wenye mahitaji maalumu kupata huduma hizo bila ya matatizo.

Alisema maandalizi ya kamusi hiyo yamekamilika ambayo itakuwa mwongozo kwa wanafunzi wenye mahitaji ya alama na hivyo kuweza kufahamika vizuri wakati wanaposomesha.

"Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Wizara imejipanga vizuri kwa ajili ya kuimarisha huduma za elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu," alisema.

Aidha, Said alisema tayari jumla ya shule 50 za Unguja na Pemba zimejengwa miundombinu rafiki ambayo itawawezesha kuzifikia shule hizo kwa urahisi na kupata mahitaji yao.

Alisema malalamiko yaliokuwapo awali sasa yameanza kupatiwa ufumbuzi wake ikiwamo kukamilika kwa kusajili wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa ajili ya kuwafahamu.

"Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu tumepiga hatua kubwa katika kuimarisha elimu ya mjumuisho na kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji mbali mbali kufaidika na sekta ya elimu," alisema.

# Dar yajipanga kwa elimu marufuku mifuko ya plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Dar es Salaam umesema umejiandaa kutoa elimu kwa umma kuhusu marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki.

Hivi karibuni, serikali ilipiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira, huku mwisho wa matumizi hayo ni Juni mosi, mwaka huu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amesema mkoa unatumia City Radio kuwaelimisha wananchi juu ya katazo hilo.

Kadhalika, Kunenge amesema kuwa Mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda, ataandaa mkutano maalumu katika harakati za kutoa elimu juu ya katazo hilo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza litatumia kanda zake saba kuhakikisha utekelezaji wa katazo hili unakwenda vizuri kwa kushirikiana na mikoa kuandaa maeneo ya kuhifadhi masalia ya mifuko baada ya katazo. Pia amewaalika wadau wenye kutaka ufafanuzi juu ya katazo hili kuwasiliana na makao makuu ya baraza.

Wakati mkoa ukielezea mkakati wake wa elimu kwa umma, serikali imesema kuwa utekelezaji wa marufuku ya matumizi ya plastiki niwakutoza faini kwa wabebaji wa bidhaa katika mifuko iliyozuiwa na siyo kuzua vurugu kwa kupekuwa mabegi au majumba ya watu.

Akizungumza na watendaji wa serikali wa Mkoa wa Dar es Salaam juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, aliwaambia watendaji hao jijini Dar es Salaam kwamba serikali haitarajii vurugu au matumizi ya nguvu kipita kiasi katika utekelezaji wa marufuku hiyo.

Makamba alisema utekelezaji wa marufuku hiyo uwe wa kisheria na kistaarabu na siyo kuwabughudhi wananchi kwa sababu walengwa ni watu waliobeba mifuko hiyo hadharani na kwa matumizi yao.

Waziri aliwasihi watendaji hao kwa kusema: "Hatutarajii matumizi ya nguvu iliyopitiliza katika kuwazuia wananchi kutumia mifuko ya plastiki. Kanuni za Sheria ya Mazingira zinataka watu wapigwe faini. Kwanza, ukikutwa na mfuko mmoja faini ni shilingi 30,000 au kifungo siku saba jela au vyote kwa pamoja. Hatutarajii watendaji kupekuwa mabegi au nyumba za watu wakisaka mifuko ya plastiki.

Utekelezaji wa kanuni wa aina hii utaleta vurugu na kuifanya dhamira njema ya serikali ionekane ni dhamira mbaya machoni mwa wananchi."

Waziri Makamba aliwaomba Watanzania wawe na mtizamo chanya wa marufuku hii na kusema kwamba ilipita miaka 30 baada ya Uhuru kabla ya mifuko ya plastiki kuanza kutumika nchini na maisha yalikwenda vizuri tu. Aliwataka wafikirie madhara yanayotoka na matumizi ya mifuko na fursa zinazoibuka kutokana na katazo hili.

Alisema Watanzania wengi watapata riziki kwa mifuko mbadala kuanzia ajira viwandani hadi wauzaji wa rejareja. Amesema zaidi ya nchi 60 tayari zimepiga marufuku matumizi ya mifuko ya aina hii na maisha yanakwenda.



Mkuu wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu, akizungumza wakati akizindua soko la madini ya vito na dhahabu wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Walanguzi pamba ya wakulima waonywa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKULIMA wa zao la pamba wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wame tahadharishwa kuacha kuuza pamba yao kwa walanguzi kwa bei ya Sh. 500, tofauti na bei elekezi ya Serikali ya Sh. 1,200 kwa kilo moja.

Imeelezwa kuwa wakati Bodi ya Pamba ikiendelea na ukamilishaji wa upitishaji wa kampuni ambayo itakuwa ikinunua pamba kwa wakulima kupitia vyama vya msingi vya ushirika (Amcos), baadhi ya wafanyabiashara wameanza kutembea kwenye kaya za wakulima na kulangua pamba kwa Sh. 500 kwa kilo. Mkaguzi wa pamba wilayani Kishapu, Thomas Tiluhongelwa, ambaye pia ni mwakilisha wa Bodi ya Pamba, alisema amesikitishwa na kitendo cha wakulima kulanguliwa pamba yao, hali ambayo itawafanya kuendelea kuwa maskini.

"Natoa onyo kwa wafanyabiashara wanaolangua pamba kwa wakulima kinyume cha taratibu za Serikali...inaelekeza wanunuzi ni kampuni kupitia Amcos kwa bei ya 1,200, hivyo tutakayemkamata tutaitaifisha pamba yake kama tulivyofanya juzi, tulitaifisha tani moja ya pamba na kesi ipo Polisi," alisema Tiluhongelwa.

"Nawaomba wakulima na wao waache kuuza pamba yao kwa kulanguliwa kwa bei ndogo ya Sh. 500 kwa kilo moja, bali wawe na subira kwa kuwa msimu umeshafunguliwa na wasubiri kuiuza kwa bei ya Serikali ya Sh. 1,200, ili wapate pesa nyingi na kuinuka kiuchumi," aliongeza.

Meneja wa Bodi ya Pamba Kanda ya Ziwa, Jones Bwahama, alisema iwapo kwenye usajili wa kampuni ambayo zitaruhusiwa kununua pamba kwa mujibu wa sheria, na ndio maana licha ya msimu kufunguliwa Mei 2, pamba haijaanza kununuliwa.

Baadhi ya wakulima wa Pamba wilayani Kishapu, walisema wamekuwa wakiuza pamba kwa walanguzi kutokana na kukabiliwa na ukata wa fedha, na kutoa wito kwa Bodi ya Pamba iruhusu kampuni kuanza ununuaji wa pamba hiyo ili kuwanusuru dhidi ya umaskini.

# Abiria basi la Express wanusurika

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ABIRIA 24 waliokuwa wakisafiri kwa basi la Arusha Express linalofanya safari zake kutoka Bukoba-Arusha wamenusurika kifo, baada ya basi hilo kuwaka moto na kuteketea kabisa dakika chake kutoka kituo kikuu cha mabasi mjini Bukoba.

Wakizungumzia tukio hilo, mmoja wa wafanyakazi wa kampuni ya Arusha Express, Ally Nkusa, alisema moto ulitokea kwenye injini na kuwa walijaribu kuuzima ikashindikana, na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walipofika gari lilikuwa limeshateketea.

Mmoja wa abiria, Humulie Kaimani, alisema alikaa kiti cha nyuma ya dereva na ghafla alisikia harufu, lakini hakujua sababu na muda mfupi abiria aliyekuwa amekaa naye kiti kimoja ndiye aliona moto na kumwita dereva ili asimamishe gari.

"Dereva alisimamisha gari haraka, abiria tukaanza kukimbia, sisi tuliokuwa viti vya mbele tukapitia mlangoni lakini wengine wakapitia madirishani," alisema.

Shuhuda, Vicent Michael ambaye ni mlinzi katika kituo cha mafuta cha Smart Oil, alisema akiwa kazini alifuatwa na watu waliokuwa na pikipiki wakimtaka awasaidie mtungi wa kuzimia moto. "Walinibeba katika pikipiki nikiwa na mtungi wa kuzimia moto wa kazini kwangu, nilipofika nikakuta wamekwishatoa abiria wote na mizigo, nikaanza kuzima moto kuanzia mlango wa dereva nikafanikiwa, nilipohamia mlango wa abiria mtungi wangu ukaishiwa poda," alisema Michael.

"Haiwezekani dereva anaondoa gari stand bila kukagua mtungi wake, hili ni kosa kubwa, lakini gari kubwa kama hili inabidi liwe na ndoo ya mchanga kama ungekuwapo moto ungezimwa," alisema.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji mkoa wa Kagera, Khamis Dawa, alisema walipopata taarifa waliwahi eneo la tukio kuzima moto huo, lakini walikuta basi hilo limeshateketea, ingawa taarifa za awali za dereva zimedai kuwa alisikia mlipuko kwenye injini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha kuwapo kwa ajali hiyo na kusema hakuna kifo wala majeruhi, na abiria wote walitafutiwa basi lingine na kuendelea na safari.

HABARI KIMATAIFA

## Tshisekedi ateua Waziri Mkuu

**KINSHASA,** Congo

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amemteua Sylvestre Ilunga Ilukamba kuwa Waziri Mkuu.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu na kutangazwa na televisheni ya taifa Jumatatu ilieleza kuwa Ilukamba anachukuwa nafasi ya Bruno Tshibala aliyetumikia nafasi ya Waziri Mkuu tangu Aprili 7 mwaka 2007, chini ya utawala wa Rais mstaafu Joseph Kabila.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Ilukamba kabla ya uteuzi huu alikuwa Mkuu wa Kampuni ya Reli ya Taifa nchini Congo inayojulikana kama SNCC. Pia aliwahi kuwa Waziri wa Fedha wakati wa utawala wa Mobutu Sese Seko.

Wakati huo huo, maelfu ya watu Jumatatu wamemlaki kwa shangwe na vigelegele Moise Katumbi, mpinzani mkuu wa Rais mstaafu Joseph Kabila, alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege mjini Lubumbashi, akirejea nyumbani kutoka uhamishoni.

Katumbi mwenye umri wa miaka 54, mwanasiasa pia mfanyabiashara alikuwa gavana wa Jimbo la Katanga kwa muda mrefu.

Katumbi alikataliwa kushiriki kwenye uchaguzi wa Desemba mwaka 2018, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu akiwa nje ya nchi.

Alikuwa anatuhumiwa kumiliki ardhi kinyume cha sheria, shutuma ambazo alizikana. Lakini hukumu hiyo ilifutiliwa mbali na vyombo vya sheria vya DRC. **VOA**

## ...mwili wa baba yake kurejeshwa Congo

**KINSHASA,** Congo

FAMILIA ya aliyekuwa kiongozi wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Étienne Tshisekedi wa Mulumba, imesema mwili wa kiongozi huyo, utarejeshwa nyumbani Mei 30, mwaka huu, kuzikwa Juni mosi.

Étienne Tshisekedi ni baba wa rais wa sasa wa Congo, Felix Tshisekedi, ambapo ni muda wa miaka miwili imepita tangu alipofariki dunia akiwa mjini Brussels nchini Ubelgiji mwezi Februari mwaka 2017.

Baada ya kifo chake kulizuka utata ni wapi atazikwa kiongozi huyo, ambapo uongozi wa chama chake cha UDPS, ulitaka azikwe kwenye makao makuu ya chama hicho, katikati ya Jiji kuu la Kinsasha, lakini serikali wakati huo ikiongozwa na Rais Joseph Kabila ilikataa.

Hadi anafariki, Étienne Tshisekedi alikuwa kiongozi wa muda mrefu wa upinzani, akiongoza chama cha UDPS lakini aliwahi kuhudumu kama Waziri Mkuu wakati wa utawala wa rais wa zamani wa nchi hiyo, Mobutu Seseko kuanzia mwaka 1991 hadi 1993 na baadaye mwaka 1997.

Étienne Tshisekedi aliwahi kuwania nafasi ya urais mara kadhaa nchini humo. **RFI**

# Sudan Kusini kufunga balozi kisa umaskini

**JUBA,** Afrika Kusini

SERIKALI ya Sudan Kusini imesema inapanga kufunga balozi zake 39 nje ya nchi kwa sababu ya hali ngumu ya kiuchumi.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Mawien Makol, alisema Juba inapata shida kuendesha balozi hizo kwa sasa.

Aidha, ameongeza kuwa sababu ya kufunga balozi hizo ni kutumia fedha zitakazohifadhiwa ili kuendesha zile zinazosalia na kwamba uamuzi huo unaanza kutekelezwa haraka iwezekavyo.

**Rais Salva Kiir wiki iliyopita kuwafuta kazi mabalozi 40 ambao alisema walikuwa hawaendi kazini kwa muda mrefu.**

Hatua hii imekuja, baada ya Rais Salva Kiir wiki iliyopita kuwafuta kazi mabalozi 40 ambao alisema walikuwa hawaendi kazini kwa muda mrefu.

Sudan Kusini ilipata uhuru mwaka 2011 na kutuma mabalozi katika mataifa mbalimbali lakini changamoto kubwa imekuwa ni kuanza kwa vita mwaka 2013.

Kumalizika kwa mzozo wa Sudan Kusini kati ya Rais Salva Kiir na Riek Machar, pande zote mbili zilitia saini mkataba wa amani, unataka kuundwa kwa serikali ya mpito, suala ambalo halijafanyika hadi sasa. **RFI**



Wafuasi wa mgombea urais Indonesia, Prabow Subianto, wakiwa wamembeba kijana aliyejeruhiwa kwenye mapigano na Jeshi la Polisi, imeelezwa kuwa watu sita wamefariki kwenye vurugu hizo. **PICHA REUTERS**

# Sita wafariki, 200 wajeruhiwa vurugu

**JAKARTA,** Indonesia

RAIS wa Indonesia, Joko Widodo, amesema hawezi kuvumilia kuona mtu yeyote anavuruga mchakato wa kidemokrasia wa nchi hiyo.

Ametoa kauli hiyo baada ya kutokea kwa mapambano kati ya polisi na wafuasi wa jenerali mstaafu wa jeshi, Prabowo Subianto, ambaye alishindwa katika uchaguzi hivi karibuni.

Katika mapambano hayo, watu wasiopungua sita wameuawa na wengine zaidi ya 200 wamejeruhiwa katika vurugu hizo zilizotokea jana.

"Hatutatoa fursa yoyote ghasia kufanyika, hasa wale ambao wataleta uharibu wa nchi ya Indonesia, jeshi na polisi watachukua hatua madhubuti kwa kufuata sheria," alisema Rais Widodo.

Alisema waandamanaji walikaidi kutawanyika wakati polisi walipokuwa wanajaribu kuwashawishi kuondoka huku wakiwaambia ni mwezi wa Ramadhani na wajiepushe na kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani katika mwezi mtukufu.

Inadaiwa kuwa waandamanaji hao walichoma nyumba za polisi na magari, hali iliyowalazimu Jeshi la Polisi kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya waandamanaji.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Dedi Prasetyo, alieleza kuwa maandamano hayo yalibadilika kuwa vurugu Jumanne usiku na ziliendelea hadi Jumatano, idadi kubwa ya watu wameshakamatwa.

Widodo alisema hali ya amani nchini Indonesia iko shwari na kuwataka wananchi wa Indonesia kuungana baada ya uchaguzi.

Tume ya Uchaguzi ya Indonesia (KPU) Jumanne ilithibitisha kuwa Joko Widodo, ambaye anajulikana pia kama Jokowi, alichaguliwa tena kwa kura kwa kupata kura asilimia 55.50, na kumshinda Jenerali mstaafu wa Jeshi, Prabowo.

Prabowo, ambaye na anaungwa mkono na wanasiasa wasomi na Waislam wenye msimamo mkali, alipata kura asilimia 44.50.

Prabowo alitoa tamko kupitia picha ya video Jumanne, akihimiza wafuasi wake kumuunga mkono kwa njia ya amani.

"Hatua zetu lazima zifuate katiba, demokrasia, amani bila ya vurugu! Wale wote waliokuwa na imani na mimi na marafiki zangu hapa... hatupiganii maslahi binafsi, lakini kwa ajili ya uhuru wa watu wetu, kwa ajili ya demokrasia, kwa ajili ya Indonesia huru, ili tuwe huru kutokana na uvamizi wa nchi yetu katika muundo wowote," alisema Prabowo.

Prabowo alikataa kuyakubali matokeo na kujitagaza yeye ndiye mshindi.

Katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari Jumanne asubuhi, alisema kuwa timu ya kampeni yake imepanga kupinga matokeo ya uchaguzi katika Mahakama ya Katiba.

Anadai kulikuwa na wizi mkubwa wa kura lakini hakutoa ushahidi wowote wa kuthibitisha hilo.

Msemaji wa Polisi mjini Jakarta, Argo Yuwono, alieleza kuwa askari wasiopungua 50,000 walikuwa wamepelekwa katika eneo hilo ikitarajiwa kutokea fujo zilizokuwa zimeandaliwa. **VOA**

# Familia ya Azory Gwanda yafunguka

**Na Magreth Magosso,**
KIGOMA

BABA mzazi wa aliyekuwa mwandishi wa habari gazeti la Mwananchi, Azory Gwanda, Obeid Gwanda (96) amezungumza kwa mara ya kwanza kuhusu kupotea kwa mtoto wake.

Mzee Gwanda aliyasema hayo jana katika kijiji cha Msimba, Kata ya Mngonya wilayani Kigoma.

Alisema anataka kufahamu kama kijana wake yuko hai au amekufa kwa lengo la kuhitimisha msiba kwa taratibu ya imani yake ya Kikristo.

"Ni mtoto aliyekuwa ananibeba pale ninapokwama. Nina miaka 96 sina uwezo wa kufanya kazi za vibarua vya kulima ili nipate chakula bora, kama atapatikana nitashukuru, kama amekufa nihitimishe kwa imani yangu ya Kikristu," alisisitiza Mzee Gwanda.

Naye mama wa mwandishi huyo Eva Mpulumba, alisema hivi sasa wanaishi kwa dhiki kwa mahitaji ya msingi hasa chakula na mavazi na watoto waliobakia kijijini hapo wana mazingira magumu kiuchumi hali inayowapa ujasiri wa kumwomba Rais John Magufuli aingilie kati kwa kuhimiza taarifa sahihi na tamko rasmi juu ya hatima ya kijana wao hata kama itabainika amekufa.

Wadogo zake, John Gwanda na Sofia Gwanda, kwa nyakati tofauti walisema ni zaidi ya mwaka mmoja na nusu tangu walipopata taarifa kupitia vyombo vya habari juu ya kutoweka kwa kaka yao.

Gazeti hili limewahoji baadhi ya majirani juu ya mienendo ya mwandishi huyo namna alivyoishi na familia yake na jamii kiujumla na Mzee Mikael Kasunzu alisisitiza kuwa awali kijana huyo alikuwa msaada tosha kwa jamii yake kimawazo na hata kifedha kwa wazee waliohitaji msaada kwake.

Wakati huo huo, Prisca Daniel, ambaye ni ndugu wa mwandishi huyo, alisema hivi sasa familia imekuwa ikisaidiwa na majirani pale wanapokwama kifedha sambamba na chakula na kuomba serikali iingilie kati juu ya hatima ya ndugu yake ili watulie na waridhike na matokeo sahihi ya kupotea kwake.

Gazeti hili limeshuhudia uhalisia wa mazingira ya makazi ya wazazi wa mwandishi huyo yanahitaji msaada wa kijamii na serikali katika kumudu gharama za maisha wakati huohuo rais wetu msikivu mpenda haki kwa wanyonge aingilie kati suala la kutoweka kwa mwandishi huyo aliyekuwa akiripoti matukio ya mauaji ya watoto huko mkoani Pwani.

Azory alitoweka tangu Novemba 21, mwaka juzi na kwa mujibu wa mke wake, Anna, watu wasiojulikana wapatao wanne wakiwa na gari aina ya Toyota Land Cruiser walimchukua.


IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
AT MWANZA
RM.CIVIL CASE NO. 28 OF 2019
ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF
VERSUS
MARY NZUMI MASANJA……………………….DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION

TAKE NOTICE THAT the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
MARY NZUMI MASANJA
OF MWANZA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
AT MWANZA
RM.CIVIL CASE NO. 24 OF 2019
ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF
VERSUS
SAADA B. KILYA………………………DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION

TAKE NOTICE THAT the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
SAADA B. KILYA
OF MWANZA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
AT MWANZA
RM.CIVIL CASE NO. 28 OF 2019
ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF
VERSUS
SIMON M. IKOHI…………………………...DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION

TAKE NOTICE THAT the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
SIMON M. IKOHI
OF MWANZA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
AT MWANZA
RM.CIVIL CASE NO. 28 OF 2019
ACCESS BANK (T) LTD……………..PLAINTIFF
VERSUS
ZAKARIA CHARLES CHEREHANI…………DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION

TAKE NOTICE THAT the above case has been fixed for hearing/mention on the 27 Day of May 2019 at 8:30 a.m. in the afternoon.

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this Day of 20 May 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

TO BE SERVE UPON:
ZAKARIA CHARLES CHEREHANI
OF MWANZA


# NEC yateua madiwani 7 viti maalum

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imefanya uteuzi wa madiwani wanawake wa viti maalum saba katika halmashauri za manispaa za Sumbawanga na Tunduma, Tandahimba, Korogwe na Rombo.

Akizungumza ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mbarouk Mbarouk, alisema uteuzi huo ulifanyika baada ya tume kupokea taarifa kutoka kwa waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa kuhusu kuwapo kwa nafasi za madiwani wanawake wa viti maalum katika halmashauri hizo kutokana na sababu mbalimbali.

Alizitaja sababu hizo kuwa ni pamoja na waliokuwa madiwani katika halmashauri hizo kufariki dunia, kujiuzulu na kuvuliwa uanachama na hivyo nafasi zao kuwa wazi.

Jaji Mbarouk Mbarouk, aliwataja madiwani walioteuliwa na vyama wanavyotoka kuwa ni Regina Willbard Lyakurwa na Beatrice Revocatus Silayo, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Regina Abiudi Liffi, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ni Agness Atanazi Chilulumo, Halmashauri ya Manispaa ya Tunduma wote wanatoka Chadema.

Wengine ni Shahara Alfani na Mey Dadi, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kutoka CUF na Mwajuma Waziri Kitumpa, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, kutoka CCM.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

### MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836


***NIPASHE***
***NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**au piga simu: 0767 223311**


### KUPOTEA KWA CHETI



**Yasin J. Shabani** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0372/0090**

Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Kirua. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu nae.

**Polisi Taarifa:**
**META/RB/271/019**

115244102

### CHETI KIMEPOTEA



**ANUSIATHA B.MAHENGE** amepotelewa na Cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya Secondari **NDEMBELA,** Alichomaliza mwaka 2014 na chenye index namba S0434-0008.

**Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**
**Taarifa ya polisi;**
**MOR/RB/4339/2019.**

115244102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo **DODOMA MJINI**
Usimamizi wa mirathi 36/2019

Ombi la **TAUSI KAWAMBA RAMADHANI** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu **MUSSA HAMISI SINUNDO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 12/6/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huy upo Mahakamani waweza kukaguliwa

115243502

### NOTISI/MNADA


**TEGEMEZA AND COURT BROKER**

Kwa niaba ya **ENTERPRISE FINANCE LTD** kutakuwa na mnada wa hadhara tarehe 30/5/2019 eneo la Tabata Kimanga. Mali itakayouzwa ni gari aina ya Raum T 683 BGZ. Mnada utaanza saa 5:00 asubuhi.

**Kwa mawasiliano:**
**0762 443118.**
**Watu wote mnakaribishwa.**

115243402

### CHETI KIMEPOTEA



**TAJI TWAIBU LUSINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha KIDATO CHA NNE chenye no S0199/0033 kilichotolewa na **NECTA TANZANIA** mwaka 2013., **CHETI CHA UDEREVA** kilichotolewa na chuo **TOP ONE IN** pamoja na **CHETI CHA KUZALIWA**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:**NT/RB/370/2019**

115241802


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUHAIL SANAULLA SANGEY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO T953DES ENGINE NO 6120689 CHASSES S NO XLER4X20004411017 YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**AR/RB/ 5307/2019.**

215242002

### KUPOTEA KWA CHETI



Aggrey John Mwaikugile anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index nambaS.0140-0002 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Mzumbe.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: URP/RB/2600/2019**

115241802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;108/2019

Ombi la **ADJUTA VICTORY MAHOWE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **EXPEDITHA THEODORY MKALI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/05/2019.

115241602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;112/2019

Ombi la WILLIAM ABBAS MILANZI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu DAGMARY DANFORD DYAULI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

115241702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Nguyen Van Son** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T582 DNL** aina ya **TOYOTA PREMIO,** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/SEL/RB/20310/2019**

115242302


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***
***Tupigie 0767 223 311***


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DESCHAMPS ATOA SOMO KWA POGBA, GRIEZMANN

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps ana furaha kuwapa maoni yake, Antoine Griezmann na Paul Pogba kuhusu majaliwa yao ya baadaye, lakini amewaonya kuhakikisha wanakuwa na uhakika na chaguzi wanazotaka kufanya kuhusu uhamisho wao.

Mshambuliaji wa Atletico Madrid, Griezmann, alithibitisha wiki iliyopita kwamba ana mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la Wana Metropolitano mwishoni mwa msimu huu, licha mwaka jana tu kukubali kusaini mkataba wa miaka mitano.

Kwa upande wake Pogba, amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na mpango wa kuhamia kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid baada ya kuwa na msimu mbaya pale Manchester United.

Deschamps ambaye amewaita wachezaji wote wawili kwenye mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Bolivia na ile ya kufuzu Euro 2020 dhidi ya Uturuki na Andorra mwezi ujao, amesema wachezaji hao wanatakiwa kufanya maamuzi ambayo hawatayajutia hapo baadaye.

"Wachezaji wanafanya uchaguzi wao, siko hapa kwa ajili ya kuwashauri," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nipo hapa kuwapa maoni yangu, lakini ni juu yao kuamua. Inategemea na kile walichokiamua kwenye maisha yao ya soka pamoja na familia zao.

"Wengi wao wananiuliza kuhusu maoni yangu. Wanaweza kuyatumia au kuyaacha kwa sababu haya ni maisha yao wenyewe."

# Juventus yafikia pazuri kumsajili Milinkovic-Savic



**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imefikia makubaliano ya awali na kiungo wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic, wakati wakiweka mipango yao sawa kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo kutoka Lazio kipindi hiki cha majira ya joto.

Milinkovic-Savic hakuwa kwenye kiwango bora mwanzoni mwa msimu huu akiwa na Lazio, lakini kiwango chake kiliimarika baadaye kuelekea mwishoni mwa msimu na alitajwa kuwa kiungo bora wa msimu kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Yeye pia alikuwa mhimili mkuu wa ushindi wa Lazio kwenye fainali ya Coppa Italia, ambapo alifunga bao la ufunguzi kwenye fainali dhidi ya Atalanta wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Italia, Gianluca Di Marzio, Juventus imemfanya kiungo huyo wa Serbia kama ndiye usajili wao muhimu zaidi na mazungumzo ya awali yameanza kwa ajili ya kujua bei yake ili aondoke hapo Lazio.

Taarifa zinaeleza kwamba, Juventus tayari imefikia makubaliano ya awali na Milinkovic-Savic, lakini majadiliano kati ya klabu hizo mbili bado hayajafanyika na inaaminika kwamba, Juventus bado italazimika kusubiri kwa muda mrefu kabla ya kukamilisha usajili wake.

Juventus awali ilijaribu kumsajili kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 thamani yake ilitajwa kuwa ni euro milioni 100 na Rais wa Lazio, Claudio Lotito.

Habari kuhusu Milinkovic-Savic bado haijawa wazi zaidi, kwani mchezaji huyo hivi karibuni alinukuliwa akisema kwamba anataka kupata mafanikio na Lazio.

Akizungumza na Calciomercato baada ya ushindi wa Coppa Italia alisema: "Bado nimeshitushwa na fainali, tuna matumaini ya kushinda zaidi. Nataka kuleta mataji zaidi hapa kwa Biancocelesti."

# Cech arudi Chelsea kama mkurugenzi

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa zamani wa Chelsea, Petr Cech, atarudi katika Klabu yake hiyo ya zamani kipindi cha majira ya joto kama mkurugenzi mpya wa michezo, Sky Sports imeripoti.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 37, atastaafu kucheza soka mwishoni mwa msimu huu na anajipanga kurudi katika klabu hiyo ambayo ametumia misimu 11 kama mchezaji kabla ya kuhamia Arsenal mwaka 2015.

Bado haijajulikana majukumu ya mwanzo ya Cech pale Stamford Bridge kwani ndio itakuwa ni mara yake ya kwanza kupewa majukumu hayo.

Nafasi hiyo imekuwa wazi tangu kuondoka kwa Michael Emenalo aliyejiuzulu mwaka 2017 na anatarajiwa kufanya majukumu yake kwa kuchukua nafasi ya Emenalo.

Sky Sports ilitangaza habari hizo kwenye tovuti yake na kuthibitisha kwamba, Cech atakuwa mkurugenzi wa michezo wa hapo kuanzia msimu ujao baada ya kutimiza majukumu yake ya kucheza pale Arsenal.

Blues hao wamedokeza kwamba, wanampango wa kuwarudisha nyota wao wote wa 'kizazi cha dhahabu' wakiwamo John Terry na Frank Lampard katika miaka michache ijayo.

Rodgers amedai kwamba anajua kuwa wachezaji wake, hasa Maguire watatakiwa na klabu mbalimbali kubwa, lakini akadai kwamba atalishughulikia jambo hilo kwa ukweli mkubwa.



HABARI MICHEZO

## Dybala, Aguero waitwa Argentina, Icardi atoswa

**BUENOS AIRES,** Argentina

PAULO Dybala na Sergio Aguero wamejumuishwa kwenye kikosi cha Argentina kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America 2019, lakini Mauro Icardi ameachwa baada ya kuwa na miezi michache migumu pale Inter Milan.

Icardi ameshindwa kuonyesha kiwango cha kuvutia katika ngazi ya klabu, pamoja na sintofahamu yake kuhusu mkataba wake na klabu hiyo na hivyo kumuacha kwenye kikosi na kumpokonya unahodha.

Alifunga kwa mara ya pili mwaka 2019 wakati Inter ikiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Napoli Jumapili, lakini mabao yote hayo aliyafunga kwa penalti na hakuwa na kipindi cha kuvutia.

Nyota wa Manchester City, Aguero ameitwa katika kikosi hicho kwa mara ya kwanza tangu kufanya vibaya kwa Argentina kwenye Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi, wakati alipofunga mabao mawili katika michezo minne. Aguero amefurahia msimu mwingine bora katika ngazi ya klabu na ana uhakika wa kufanya vizuri kwenye Copa, ambapo ataungana na mchezaji mwenzake wa pale Man City, Nicolas Otamendi.

Dybala pia ameingia katika kikosi hicho licha ya kuwa na msimu mgumu pale Juventus, huku ikionekana kufunikwa na ujio wa Cristiano Ronaldo.

Lionel Messi anatarajiwa kuwa nahodha wa kikosi hicho huku kuitwa kwa Matias Suarez mwenye umri wa miaka 31, kumewashangaza wengi, ambapo mshambuliaji huyo wa River Plate ameichezea Argentina mechi mbili tu mwaka huu. Pia kuna mshituko kwenye safu ya ulinzi, huku Milton Casco akichaguliwa mbele ya Gabriel Mercado.

Wakali wa Manchester United, Sergio Romero na Marcos Rojo pia wametemwa katika kikosi hicho.

Argentina itacheza na Colombia, Paraguay na Qatar kwenye hatua ya makundi ya michuano hiyo itakayofanyika nchini Brazil.

**Kikosi kamili cha Argentina:**

Franco Armani (River Plate), Agustin Marchesin (Club America), Esteban Andrada (Boca Juniors); Juan Foyth (Tottenham), Nicolas Tagliafico (Ajax), Renzo Saravia (Racing Club), German Pezzella (Fiorentina), Ramiro Funes Mori (Villarreal), Milton Casco (River Plate), Nicolas Otamendi (Manchester City); Roberto Pereyra (Watford), Leandro Paredes (Paris Saint-Germain), Marcos Acuna (Sporting CP), Angel Di Maria (Paris Saint-Germain), Guido Rodriguez (Club America), Rodrigo De Paul (Udinese), Exequiel Palacio (River Plate), Giovani Lo Celso (Real Betis); Sergio Aguero (Manchester City), Lionel Messi (Barcelona), Matias Suarez (River Plate), Paulo Dybala (Juventus) na Lautaro Martinez (Inter).





## FIRMINO FITI KUICHEZEA LIVERPOOL FAINALI UEFA

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Roberto Firmino, alifanya mazoezi na wachezaji wenzane Jumanne wakati aliporudi kwenye kikosi kutoka chumba cha majeruhi kuelekea fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Tottenham.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alikosa mechi tatu za mwisho ukiwamo ule wa pili wa ushindi wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona kutokana na maumivu ya nyonga.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alikuwa sehemu ya kikosi hicho wakati kikifanya mazoezi pale Marbella Jumanne na alionekana kuwa fiti kuelekea kwenye mchezo huo utakaopigwa Juni Mosi jijini Madrid mwaka huu.

Liverpool ilisema kwamba mazoezi yatafanyika kwa umakini mkubwa na Firmino atakuwa sehemu ya kikosi hicho kwenye mazoezi.

Firmino amekuwa mchezaji muhimu kwa Liverpool msimu huu akifunga mabao 16 katika mechi 47 alizoichezea kwenye mashindano yote.

## *Giroud aongezewa mwaka darajani*

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea, imethibitisha kwamba, mshambuliaji wake, Olivier Giroud amesaini mwaka mmoja kwa ajili ya kuongeza mkataba wake ambao sasa unamuweka hapo hadi msimu wa 2019/20.

Alijiunga na klabu hiyo kutoka Arsenal Januari mwaka 2018 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 15 kwa mkataba wa miezi 18, na Giroud mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa ilibainishwa kwamba hangeweza kuendelea na klabu hiyo kutokana na kiwango chake kuwa duni, tofauti na matarajio.

Na kama ilivyobainisha taarifa ya klabu hiyo, kuwa wamefikia makubaliano kwa pande zote mbili kwa kusema: "MKataba wa Olivier Giroud na Chelsea umeongezwa hadi msimu wa 2019/20."

Mchezaji mwenyewe alionesha furaha kubwa kwa kupata nafasi hiyo na kuelezea: "Nina furaha kubwa kusaini mkataba mpya. Kwa hakika nilitaka kubakia hapa kwa mwaka mmoja zaidi nilihisi kuwa ni sehemu ya timu, tangu mwanzo nilitumaini kuwa hapa na kutwaa mataji zaidi."

Na wakati tunazungumza, mkurugenzi wa muda wa klabu hiyo, Marina Granovskaia aliongeza: "Tuna furaha kwamba Olivier ataendelea kuwa mchezaji wa Chelsea msimu ujao.

"Tangu alipojiunga na sisi miezi 18 iliyopita, alikuwa na muda mzuri na sisi na tulisubiri nafasi hii kutoka kwake na tunatambua mchango wake kwa timu.

"Amekuwa mfungaji bora kwenye Ligi ya Europa kwa kufunga mabao 10 msimu huu na bado ana nafasi nzuri zaidi ya kuendelea kufanya makubwa na klabu hii."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# LACAZETTE AACHWA UFARANSA AKIJISIFU AMETISHA KIWANGO

Nimecheza soka bora katika wasifu wangu kisoka msimu huu na kwa Arsenal...

**LONDON,** England

STRAIKA wa Arsenal, Alexandre Lacazette, anashawishika kuwa kwenye kiwango bora zaidi katika maisha yake kisoka baada ya msimu mzuri akiwa na 'Gunners' hao.

**Nyota huyo wa zamani wa Lyon, amefunga mabao 19 na kutengeneza mengine 11 kwenye mashindano yote akiwa na Arsenal msimu huu, kwa ushirikiano mkubwa na 'pacha' wake dimbani, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang.**

Ingawa ameachwa katika kikosi cha sasa cha Ufaransa kilichoitwa juzi Jumanne kujiandaa na mechi za Kundi H za kuwania kufuzu Euro, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anaamini amekuwa katika kiwango cha juu kimchezo msimu huu.

Na ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Klabu wa Mwaka, huku akiwa na ufanisi mkubwa kwenye Europa League, akifunga mabao matano katika mechi tisa wakati huu wakielekea kucheza fainali ya michuano hiyo, ingawa anahisi tuzo binafsi itakuwa si lolote kwake bila kombe.

"Nimecheza soka bora katika wasifu wangu kisoka msimu huu na kwa Arsenal, na si kwa sababu ya kufunga mabao, lakini katika mchezo wangu - ukweli nimejizatiti," alisema Lacazette.

"Kuwa tayari kuchangia bila kufunga ni muhimu kwa timu. Kwangu mimi, pamoja na sasa, ninafurahia kufanya kazi kama hivi na wachezaji wenzangu kwa sababu ninajua itakuwa rahisi kwao.

"Katika kipindi kilichopita, mara zote nimejifunza kwamba kama unafanya kwa ajili yao, watakurudishia mpira haraka, na ndiyo maana ninafuraha kuwasaidia.

"Tuzo binafsi ukweli si muhimu kabisa. Mara zote ni furaha, bila shaka, kupokea vitu kama hivi, lakini si kitu cha kwanza ninachowaza wakati ninacheza soka. Ninataka kushinda kombe, kama Europa League.

"Mara zote ninaonyesha ubora wangu hata kama sipo vizuri - lakini mara zote ninajaribu kuwa bora. Ninaipigania klabu, hivyo bila shaka, ninapigana kwa ajili yao, kwangu mimi, kwa ajili ya wachezaji wenzangu, kwa familia yangu na kwa kila mmoja.

"Ninataka tu kushinda na kila mmoja ataniunga mkono, hivyo bila shaka, nitapigana kwa ajili yao pia."

Arsenal itacheza dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa fainali ya Europa League Mei 29, mwaka huu itakayopigwa mjini Baku, Azerbaijan.

Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps mbali ya kumwacha Lacazette katika kikosi chake, kwa mara ya kwanza amemjumuisha beki wa Barcelona, Clement Lenglet na kumwacha Aymeric Laporte wa Manchester City.

Baada ya mechi yao ya kirafiki dhidi ya Bolivia, Ufaransa itasafiri kwenda Uturuki Juni 8 na kisha Andorra Juni 11, mwaka huu, wakati ikitazama kuendeleza ushindi wao kwa asilimia 100 katika mechi zake za Kundi H.

Na alipoulizwa katika mkutano na waandishi wa habari kwa nini amemchagua Lenglet badala ya Laporte, Deschamps alisema: "Uchaguzi mara nyingine ni mgumu. Siwezi kusema kila wakati, hata kama ungependa.

"Wachezaji wengine wanastahili pia na Aymeric ni kati yao. Kama nisingemchagua Clement, angestahili hilo pia.

"Ni fursa kwangu. Nina wachezaji wengi kwa kila nafasi ambao ni wagombea wa timu ya Ufaransa. "

## ZISIKUPITE

### SARRI LULU ROMA, JUVE

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, 60, anawindwa na Juventus wakati huu ikitazama mrithi wa Massimiliano Allegri, huku Roma pia ikielezwa kuvutiwa na Mtaliano huyo. ***(Sky Sports)***

### BARCA KUIUZIA UTD RAKITIC

MANCHESTER United inataka kumsajili Ivan Rakitic, 31, na Barcelona ipo tayari kumuuza kiungo huyo wa kimataifa wa Croatia. ***(Express)***

### LAMPARD KURUDI CHELSEA

KOCHA wa Derby, Frank Lampard anaweza kurudi Chelsea kumrithi Maurizio Sarri, ingawa Juventus inaweza kumteua kocha wa Lazio, Simone Inzaghi. ***(Daily Mirror, via Sky Sport Italia)***

### SCHUBERT KUMRITHI CECH

ARSENAL itatazama uwezekano wa kumsajili kipa wa Dynamo Dresden na Ujerumani U-21, Markus Schubert, 20, kwa uhamisho huru majira haya ya joto kama mbadala wa Petr Cech. anayestaafu. ***(Bild - in German)***

### BALE 'ANUKA' JUMLA MADRID

ZAIDI ya mashabiki 330,000 wa Real Madrid wamepiga kura ya viwango vya wachezaji wa klabu hiyo kwa msimu wa 2018-19, na asilimia 92 ya kura ya 'kufeli' akipigiwa mshambuliaji wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29. ***(Marca)***

### MATA ATAZAMWA NEWCASTLE

NEWCASTLE inaweza kuvutiwa kumsajili kiungo Mhispania Juan Mata, 31, ambaye amemaliza mkataba na Manchester United. ***(Sun)***

### CONTE KUJAZWA NOTI CHELSEA

ANTONIO Conte ameshinda vita vyake vya kisheria dhidi ya Chelsea, ambayo sasa italazimika kumlipa kocha huyo wa zamani wa Italia kiasi cha pauni milioni tisa kama fidia baada ya kumtimua majira ya joto yaliyopita. ***(Times)***

### WAN-BISSAKA KUITOBOA UTD

Manchester United inatarajiwa kulipa pauni milioni 50 kwa Crystal Palace ili kuipata huduma ya beki wa pembeni wa klabu hiyo na England U-21, Aaron Wan-Bissaka. ***(Mirror)***

### DE GEA AIGOMEA MAN U

KIPA wa Hispania na Manchester United, David de Gea, 28, amekataa ofa ya mkataba mpya na klabu hiyo wakati huu mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao. ***(Sun)***

### POGBA KUPOZWA NA UNAHODHA

KIUNGO wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, atapewa ofa ya unahodha lengo likiwa ni kumshawishi kuendelea kubaki Manchester United. ***(ESPN)***

### DAU LAIKIMBIZA SPURS

TOTTENHAM imehitimisha kuvutiwa kwake na winga wa Crystal Palace, Wilfied Zaha, 26, baada ya kukimbizwa na thamani ya pauni milioni 100 iliyowekwa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast. ***(Evening Standard)***

# TENGA AWATAKA STARS KUFANYA KWELI AFCON

Na Renatha Msungu, DODOMA

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limeitaka timu ya soka ya Tanzania (Taifa Stars) kwenda kupambana ili kuhakikisha inafika mbali katika Fainali za Kombe la Afrika (Afcon 2019), zitakazofanyika baadaye mwezi ujao nchini Misri.

**Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa BMT, Leodegar Tenga, katika semina ya Maofisa wa Michezo inayoendelea jijini hapa.**

Tenga alisema wachezaji wa Taifa Stars wanatakiwa kujituma katika kila mechi watakayocheza kwenye hatua hiyo ya makundi kwa lengo la kusaka ushindi utakaowapeleka hatua inayofuata.

Alisema Stars ina kila sababu ya kucheza soka la kiwango cha juu kwa sababu itakutana na timu zenye wachezaji wazoefu katika mashindano hayo.

Tenga alisema wao wakati wanacheza mpira hakukuwa na sapoti kubwa kama ilivyo sasa ambapo wanakila sababu ya kufanya vizuri katika mashindano hayo

Aliongeza kuwa kufanya vizuri katika mashindano hayo, kutawafanya wachezaji hao kujitangaza vema katika ulimwengu wa soka na hatimaye kupata timu kutoka nje ya Tanzania.

"Kikosi kilichoitwa kina wachezaji wazuri ambao wanaweza kujituma wakiwa uwanjani ili kupata matokeo mazuri na kuweza kusonga mbele, inawezekana kufika mbali," alisema nahodha huyo wa zamani wa Stars.

Hata hivyo, aliwapongeza na kuwataka kuwa na moyo wa kujituma na kusikiliza kwa umakini maelekezo ya kocha wao



wanapokuwa uwanjani na kutowahofia wapinzani wao kwa kuangalia rekodi walizonazo. Stars iliyopo Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na Kenya inatarajia kuingia kambini Juni Mosi na itaondoka nchini mapema kwenda Misri kwa ajili ya kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji hao itakayochezwa Juni 13, mwaka huu, katika mji wa Alexandria.

# Samatta apigiwa debe bungeni

Na Augusta Njoji, DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Amina Mollel, ameitaka serikali kutambua mchango wa Mbwana Samatta kutokana na mshambuliaji huyo wa timu ya Taifa (Taifa Stars) kuwakilisha vema Tanzania kimataifa.

Mbwana ambaye ni mshambuliaji wa timu ya Genk ya Ubelgiji ndiye anayeongoza kwa kufunga mabao mengi katika Ligi Kuu ya Ubelgiji kwa upande wa wachezaji wanaotoka barani Afrika.

Akiomba mwongozo wa Spika, Mollel alisema serikali ipo kimya licha ya Mbwana kuiwakilisha vema Tanzania kimataifa.

"Samatta anayecheza soka la kulipwa nchini Ubelgiji ameiwezesha timu hiyo kuchukua ubingwa na ameongoza ligi hiyo kwa kufunga mabao 23 kutokana na kazi nzuri aliyoifanya Mtanzania mwenzetu na tumeona wenzake na hasa wenyeji wakishangilia kwa kutumia bendera ya Tanzania ni dhahiri kabisa ameitangaza vema nchi yetu," alisema.

Mollel aliomba kupata kauli ya serikali kuhusiana na jambo hilo ili kutoa motisha kwa Watanzania wengine.

"Kwenye mtandao ameandikwa kwamba ni Mkenya ninaomba kauli ya serikali ili wengine waache kudandia dandia," alisisitiza.

Akijibu mwongozo huo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema watawasiliana na serikali namna ya kushughulika na jambo hilo wakati mwafaka.






Wachezaji wa timu ya soka ya DTB wakishangilia baada ya kufanikiwa kufuzu kucheza Ligi Daraja la Pili ngazi ya taifa msimu wa 2019/2020, kufuatia kuibuka washindi wa pili katika Ligi ya Mabingwa wa Mikoa (RCL) 2018/2019 mkoani Simiyu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DTB yaifikiria Ligi Kuu Bara

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya Diamond Trust Tanzania (DTB FC) ya jijini Dar es Salaam imefanikiwa kufuzu kucheza Ligi Daraja la Pili Ngazi ya Taifa msimu ujao wa mwaka 2019/2020 baada ya kushika nafasi ya pili katika Ligi ya Mabingwa wa Mikoa iliyomalizika mwishoni mwa wiki mkoani Simiyu.

DTB FC ilipoteza mchezo wa fainali dhidi ya Pan African uliomalizika kwa ushindi wa penalti 5-4 dhidi ya klabu hiyo kongwe ya jijini pia.

Ndani ya dakika 90 timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 na zilipoongezwa dakika 30 matokeo yalikuwa ni sare ya 2-2 huku mabao yote mawili ya DTB yakifungwa na Hussen Juma, hivyo hatua ya penalti kuchukua nafasi yake.

Fainali za Ligi ya Mabingwa wa Mikoa maarufu RCL iliochezwa Simiyu ilikutanisha timu nane zilizopangwa katika makundi mawili ambapo Kundi A lilikuwa na DTB, Isanga Rangers kutoka Mbeya, Top Boys (Ruvuma) na wenyeji Bariadi United.

Kundi B liliundwa na Pan African, Mbuni FC (Arusha), Mji Mpwapwa (Dodoma) na Mkurugenzi FC kutoka mkoani Katavi.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu na Meneja wa DTB FC, Michael Lugalela, alisema timu yake ilipambana hadi kufika hatua hiyo na kuweka wazi mashindano hayo yalikuwa na ushindani sana.

"Matazamio yetu ni kufika Ligi Kuu Tanzania Bara, japo tunajua ni kazi ngumu, lakini inawezekana kama tutajiandaa vema kwa kufanya mazoezi na kujituma, pia tukipata ushirikiano kutoka kwa uongozi wa benki tulianza safari hii katika ngazi ya chini sana ya Daraja la Tatu na macho yetu yanaitazama Ligi Kuu ya Tanzania. Itachukua muda kidogo, lakini tumeanza

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 36 | 29 | 4 | 3 | 76 | 14 | 91 |
| 2. Yanga | 37 | 27 | 5 | 5 | 56 | 25 | 86 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5. Mtibwa Sugar | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7. Mbeya City | 37 | 13 | 8 | 16 | 38 | 39 | 47 |
| 8. Ndanda | 36 | 12 | 11 | 13 | 23 | 33 | 47 |
| 9. Singida United | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 10. Stand United | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 11. Alliance | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 12. Coastal Union | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13. Mbao | 37 | 11 | 11 | 15 | 26 | 40 | 44 |
| 14. TZ Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15. Biashara United | 36 | 11 | 10 | 15 | 29 | 34 | 43 |
| 16. Kagera Sugar | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 17. Ruvu Shooting | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 18. JKT Tanzania | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 19. Mwadui | 36 | 10 | 8 | 18 | 41 | 51 | 38 |
| 20. African Lyon | 36 | 4 | 11 | 21 | 23 | 49 | 23 |

# Michezo

Alhamisi Mei 23, 2019

Nipashe




Lacazette aachwa Ufaransa akijisifu ametisha UKURASA 30



Baadhi ya wachezaji wa Sevilla wakijiandaa kutoa mafunzo kwa timu ya vijana ya Bom Bom FC katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam mara baada ya mkutano na waandishi wa habari jana. **PICHA: SPORTPESA**

## Makambo alinda heshima Yanga

**Na Adam Fungamwango**

YANGA jana iliwafurahisha mashabiki wake wachache waliojitokeza kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, baada ya kuichapa Mbeya City bao 1-0 na kufikisha pointi 86 hivyo kuendelea kupunguza wigo wa pointi dhidi ya mabingwa Simba wenye alama 91 na mechi mbili mkononi.

Alikuwa ni Mkongomani Heritier Makambo aliyelinda heshima ya Yanga kwa kufunga bao dakika ya 25 akiunganishwa kwa kichwa, mpira wa adhabu uliopigwa na Mwinyi Haji na kufikisha jumla ya mabao 17 sawa na John Bocco wa Simba, ikiwa ni sita nyuma ya kinara Meddie Kagere wa Wekundu wa Msimbazi hao.

Kabla ya hapo, Makambo alikosa bao akiwa peke yake, alipopigwa kichwa mpira wa krosi, lakini uligonga mwamba wa juu na kuokolewa na walinzi wa Mbeya City.

Makambo, ambaye hivi karibuni aliteka vyombo vya habari kutokana na kuonekana akisaini mkataba wa kuichezea Klabu ya Horoya ya nchini Guinea, alijitahidi kutaka kufunga mabao zaidi ili kuendelea kumfukuza Kagere mwenye mabao 23, lakini mashuti yake hayakuwa na macho.

Kipindi cha pili Mbeya City ilikuja juu kutaka kusawazisha bao, ikiwatumia mastraika wake tegemeo, Idd Suleiman 'Nado', Victor Angaya, wakisaidiwa na winga wao machachari aliyeingia kipindi cha pili, Peter Mapunda, lakini mabeki wa Yanga wakiongozwa na Kelvin Yondani walisimama imara kuondoa hatari zote golini.

Yanga iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, imebakisha mechi moja tu, dhidi ya Azam FC, itakayochezwa Mei 28, siku ya funga msimu wa 2018/19 Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Simba: Sevilla watakaa Taifa

## ●●● Wakali hao wa La Liga waipongeza, wasema hawakai leo, kukabidhiwa kombe na bodaboda...

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU ikiwa tayari imeshafanikiwa kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara, na leo ikitarajiwa kuwakaribisha mabingwa mara tano wa Ligi ya Europa, Sevilla FC kutoka Hispania katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Simba imesema lazima wakali hao wa La Liga "wakae".

**Sevilla FC ilitua nchini juzi tayari kwa mchezo huo wa kirafiki utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku, wakati mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, walirejea jijini jana mchana wakitokea mkoani Singida.**

Akizungumza jana jijini, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kuwa klabu yake imefarijika kupata nafasi ya kucheza na Sevilla na wanaamini wataitumia vema nafasi hiyo kwa kupata matokeo mazuri.

Magori alisema Simba ni klabu yenye historia na rekodi mbalimbali na fursa waliyoipata ya kucheza na Sevilla FC iliyoanzishwa mwaka 1890, wataitumia kuendelea kujiwekea rekodi za mafanikio.

Alisema kuwa timu yao inatarajia kupata matokeo mazuri katika mchezo huo kama walivyopata katika mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, ambapo walifika hatua ya robo fainali.

"Sevilla ni klabu kubwa, si Hispania tu, bali ni Ulaya kwa ujumla, na Simba ni klabu yenye rekodi na historia, kesho utapigwa mtanange ambao haujawaki kutokea hapa Tanzania, naomba niseme kwa sauti ya Manara (Haji- Msemaji wa Simba), kila anayekuja Taifa anakaa, alikuja JS Saoura akakaa, alikuja Al Ahly akakaa, alikuja AS Vita akakaa, na Sevilla atakaa," alisisitiza Magori.

Aliongeza kuwa mechi hiyo ya leo inatarajiwa kuwa ngumu, lakini yenye burudani kutoka pande zote mbili.

Rais wa Sevilla FC, Jose Castro Carmona, alisema mchezo wa leo ni muhimu kwa timu yake na anaamini watapata ushindi kutokana na kikosi chao kupata uzoefu unaotokana na ushiriki wao wa La Liga ambayo ndiyo ligi bora duniani.

"Kwetu ni heshima kubwa kuwa timu ya kwanza ya La Liga kuja Tanzania, ujio wetu utasaidia kuongeza mahusiano kati ya La Liga na Tanzania, itasaidia kupata wachezaji maarufu duniani kutoka Tanzania," alisema rais huyo.

Aliongeza kwa kuipongeza Simba kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa ni siku moja kabla ya kukutana nao.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema wanaishukuru SportPesa kwa kufanikisha ujio wa Sevilla ikiwa ni mara ya kwanza kwa klabu kubwa ya Hispania kufanya ziara Afrika Mashariki.

Karia alisema TFF ina mkataba wa miaka mitatu na La Liga na ujio huo utaongeza ushirikiano kati ya taasisi hizo na vile vile utaongeza chachu ya kukuza mpira hapa nchini.

### SIMBA KUPEWA KOMBE J'MOSI

Mwekezaji wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo' amewataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mchezo wa leo dhidi ya Sevilla pamoja na Jumamosi watakapowakaribisha Biashara United kwa sababu ndiyo siku watakayokabidhiwa kikombe cha ubingwa huku akiahidi kuwapa zawadi ya Sh. milioni tano na bodaboda aina ya boxer kila mchezaji kama zawadi ya kutwaa ubingwa.

Mo alisema pia wameshaanza maandalizi ya msimu mpya kwa kufanya mazungumzo ya awali na mabosi wa timu za DC United ya Marekani na Porto ya Ureno.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >